SUPA JACKPOT
TZS. 1,058,211,696
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MAWAKILI** Sabaya wagonga mwamba pingamizi rufani


ama
AFYA NA MAZINGIRA
DARASA LA MABOSI NEMC; Ndivyo ilivyo dhana ardhioevu, unyeti wake na inakopitia kitaifa
CT SCAN YA KWANZA MKOANI... Waziri Mkuu: Hospitali Rufani iasze Januari Mosi, leteni umeme haraka!
Wataalamu moyo waja na kampeni maalum magonjwa yasiyoambukiza

# Nipashe

Alhamisi Desemba 15, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581160
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW

# Serikali yasikia kilio cha mimba, utoro wanafunzi

UKURASA 2

UKURASA 13



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Kairuki.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla (kushoto), akipeperusha bendera pamoja Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, wakiashiria kuzindua rasmi NMB Pesa Akaunti katika stendi ya Magufuli, Dar es Salaam. NMB Pesa Akaunti ni mfumo wa kidigitali wa ufunguaji wa akaunti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 4

### WAWASHTAKI VIONGOZI KWA RAIS SAMIA MADAI YA KUPORWA MAENEO

ZAIDI ya wananchi 13,000 kutoka vijiji vinne vya Kata ya Nyatwali Wilaya ya Bunda, wameulalamikia uongozi wa wilaya hiyo wakidai unatumia jina la Rais Samia...

UKURASA WA 4

### MWEKEZAJI AONDOLEWA HOTELINI CHINI YA ULINZI

RAIA wa Uturuki, Erkan Acikel, ameondoshwa katika hoteli pamoja na vifaa vyake chini ya ulinzi wa polisi wakiwa na silaha za moto...

# Paroko kortini kwa madai wizi mil. 20/-

UKURASA 2

# Shahidi aangua kilio kizimbani kesi mauaji ya trafiki

UKURASA 3

MICHEZO MANDONGA AJA NA 'AKIPIGWA 'OYAOYA, AKISHINDA OYAOYA' UK. 28
KATUNI UK. 6



Wanafunzi wenye ualbino wa shule za msingi na sekondari wanaofadhiliwa na Shirika la Village of Hope, wakimsikiliza Mwandishi wa Habari kitengo cha digital, Carlos Banda, (hayupo pichani) akiwaelezea kuhusu uzalishaji wa magazeti ya Kampuni ya The Guardian Ltd, walipotembelea katika ofisi hizo Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Matokeo kidato cha 1 kipaumbele wa vijijini wanaokwenda bweni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imetangaza wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023, huku ikisema kipaumbele kimewekwa zaidi kwa wanafunzi wa vijijini wanaokwenda shule za kitaifa za bweni.

Kutokana na kipaumbele hicho, serikali imesikia kilio cha muda mrefu kilichokuwa kikielezwa kuwa kinakwamisha ndoto za mamia ya wanafunzi kutimiza ndoto zao kutokana na kukatisha masomo kwa sababu ya utoro na mimba za utotoni.

Sababu kubwa iliyokuwa ikitolewa ni wanafunzi wengi wa maeneo ya vijijini kuishi umbali mrefu kutoka shuleni kwa sababu ya ukosefu wa mabweni na hosteli. Hali hiyo ilikuwa ikiwalazimu kutembea umbali mrefu wakati wa kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

Matokeo yake, baadhi ya wanafunzi walikuwa wakishindwa kwenda shuleni na wale wa kike kukumbana na vishawishi mbalimbali vilivyokuwa vikisababisha kubakwa na wengine kuingia katika ndoa za utotoni na hatimaye kukatisha masomo.

Akitangaza uchaguzi wa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, aliagiza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na shule za bweni, kuripoti shuleni Januari 7, mwakani na waliochaguliwa kujiunga shule za kutwa kuripoti Januari 9.

Kairuki alitangaza uchaguzi huo wa wanafunzi kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2023, jijini hapo.

"Mwaka huu uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na kidato cha kwanza umefanyika kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa uchaguzi wa wanafunzi (Student Selection-Management Information System).

"Mfumo huu uliundwa na wataalamu wa TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) wa ofisi ya Rais TAMISEMI na Baraza la Mtihani la Tanzania na umesaidia kupunguza muda unaotumika kwenye uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Kairuki, wanafunzi 3,224 sawa na asilimia 0.39 wamechaguliwa kujiunga na shule za bweni za kitaifa, kati yao 932 wakiwamo wavulana 512 na wasichana 420, wamechaguliwa kujiunga na shule za sekondari za wanafunzi wenye ufaulu mzuri zaidi.

"Wanafunzi 1,323 wamechaguliwa kwenda shule za sekondari za ufundi, kati yao wavulana ni 1,110 na wasichana 213, sawa na asilimia 0.12. Lakini wanafunzi 1,969 wamechaguliwa kujiunga na shule za sekondari za bweni za kawaida. Kati yao, wavulana 979 na wasichana 990 sawa na asilimia 0.18

Waziri Kairuki alisema, wanafunzi 1,069,717 wamechaguliwa kwenda shule za sekondari za kutwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kati yao, wavulana 512,245 na wasichana 557,472 sawa na asilimia 99.61.

Idadi ya waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza Januari mwakani 2023, imeongezeka kwa wanafunzi 166,139 sawa na ongezeko la asilimia 18.30, ikilinganishwa na 907,802 waliopata alama za kuwawezesha kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022.

Alisema kati ya waliofaulu na kupangiwa kujiunga na kidato cha kwanza wamo wenye uhitaji maalum 2,775 sawa na asilimia 0.26 ambao kati yao wavulana ni 1,491 na wasichana 1,284.

Baada ya tangazo hilo la serikali, Waziri Kairuki, ameagiza wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri nchini, kuhakikisha wanafunzi wote 1,073,941 waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari Januari mwaka ujao, wanajiunga bila kikwazo.

# Paroko afikishwa kortini madai wizi mil.20/-

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

PAROKO wa Parokia ya Haydom kanisa katoliki Jimbo la Mbulu mkoani Manyara, Padri Baltazar Sulle (63), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Manyara, mjini hapo, akikabiliwa na madai ya wizi wa Sh. milioni 20 za kaka yake.

Padri Baltazar anadaiwa kuchota fedha hizo kwenye akaunti ya kaka yake, aitwaye Dionis Margwe.

Akisoma hati ya mashtaka inayomkabili Paroko huyo, Wakili wa Serikali, ambaye aligoma jina lake lisichapishwe gazetini, alidai kwamba wizi huo ulifanywa na paroko huyo pamoja na wafanyakazi wawili wa Benki ya NMB.

Aliwajata wengine wanaokabiliwa na kesi hiyo ni wafanyakazi wa Benki ya NMB, Cynthia Nyamtiga (27) na Winfrida Rwakilomba (30).

Kesi hiyo namba 44 ya mwaka huu inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi, Mariam Lusewa.

Katika hati ya mashtaka, mshtakiwa wa kwanza, Padri Baltazar anadaiwa kuiba fedha hizo ambazo zilitokana na mirathi ya shemeji yake na kaka yake ambaye alishafariki dunia.

Iliendelea kudaiwa mahakamani hapo kuwa, Paroko Sulle, alitenda kosa hilo Machi 3, mwaka 2021.

Anadaiwa kutenda kosa la kwanza ambalo ni wizi kinyume na kifungu cha 258 (1) na kifungu cha 265 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2022.

Shtaka la pili linalomkabili Padri Sulle, ni kugushi nyaraka kinyume na kifungu cha 333 na kifungu cha 355 (a) na kifungu cha 335 (d) (i) wakati shtaka la tatu linawakabili washtakiwa wote watatu.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Hakimu Lusewa alitoa masharti ya dhamana na washtakiwa wote watatu walitimiza vigezo na kuachiwa kwa dhamana ya bondi ya Sh. milioni saba kwa kila mdhamini. Kesi hiyo imeahirishwa hadi Desemba 21, mwaka huu, itakapotajwa tena.

## Mikononi mwa 'Pilato'madai kumuua baba

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAMA na watoto wake wawili wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kosa la kula njama na kutekeleza mauaji ya baba yao mzazi katika Kijiji cha Kiliwi, wilayani Kwimba mkoani Mwanza.

Watu hao wakiwamo wengine wawili wanaodaiwa kulipwa Sh. 800,000 kutekeleza mauaji ya Mange Washa (49), walipandishwa kizimbani kwa mara ya kwanza na kusomewa shtaka la mauaji.

Waliopandishwa kizimbani jana katika Mahakama ya Wilaya ya Kwimba ni Hoka Mazuri (48), mke wa marehemu, watoto wake wawili, Masunga Mange na Paskali Mange.

Wengine wawili wanaodaiwa kulipwa Sh. 800,000 na wanafamilia hao kisha kutekeleza mauaji ni Shija Masalu (28) na Makoye Lusana (53) ambaye ni mshtakiwa namba moja katika kesi hiyo.

Washtakiwa hao walifikishwa mbele ya Hakimu Mfawidhi wa mahakama ya wilaya hiyo, Ndeko Dastan. Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Robert Mwanakatwe, alidai mahakamani hapo kuwa Desemba mosi, mwaka huu washtakiwa hao walimuua, Mange Washa kwa kumkata kichwa akiwa amelala nyumbani kwake kisha kukitenganisha na kiwiliwili chake.

Washtakiwa wote wanakabiliwa na kosa hilo la mauaji kinyume na kifungu namba 196 na 197 cha kanuni ya adhabu marekebisho ya mwaka 2022.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, mahakama iliombwa kupanga tarehe nyingine kwa kuwa upelelezi wake haujakamilika.

Washtakiwa wote hawakutakiwa kuzungumza chochote kutokana na mahakama kutokuwa na mamlaka kisheria ya kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu Mfawidhi Dunstan, aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 28, mwaka 2022, itakapotajwa tena.

Washtakiwa hao wanadaiwa kupanga njama na kutekeleza mauaji ya mwanamume huyo ambaye ni mume wa mtuhumiwa mmojawapo na baba mzazi wa washtakiwa wawili kwa madai aliwanyima uhuru wa kutumia mali za nyumbani kwao.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na wananchi katika kijiji cha Mapili wilayani Mlele baada ya kukagua barabara ya lami ya Inyonga - Mapili yenye urefu wa kilomita 8.69. **PICHA: OWM**

# Mawakili wa Sabaya wagonga mwamba

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, imetupilia mbali hoja mbili zilizowasilishwa mahakamani na mawakili wa wajibu rufani katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 iliyokuwa ikimkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai,mkoani Kilimanjaro,Lengai Ole Sabaya na wenzake watano.

Mawakili hao waliwasilisha hoja hizo kupinga kufunguliwa kwa rufani dhidi ya uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoani Arusha ya kuwaachia Sabaya na wenzake.

Mbali na Ole Sabaya,wajibu rufani wengine ni Sylvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akitoa uamuzi mdogo jana, Jaji Salma Maghimbi, alisema baada ya kupitia mawasilisho ya hoja za pande zote mbili, mahakama imejiridhisha kwamba rufani iliwasilishwa mahakamani ndani ya muda.

Pia alisema kwa mujibu wa sheria, muda wa kukata rufani unaanza kuhesabika pale nakala ya hukumu inapokuwa imetolewa au kupokewa.

Kuhusu sababu ya pili, alisema Watson Mwahomange kutokuwamo kwenye nyaraka ya rufani, hakuwezi kumuathiri mteja wake au haki kutendeka.

Baada ya uamuzi huo mdogo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdalah Chavula, alidai kwamba shauri hilo lipo kwa ajili ya kusikilizwa lakini wajibu rufani waliokuwa mahakamani ni wa kwanza (Sabaya) na wa nne (Nyegu) wakati wa pili, wa tatu, wa tano na wa sita hawakuwapo mahakamani.

Chavula alidai kwamba kwa mujibu wa taarifa waliyopokea kwa Msajili wa Mahakama, waliwaandikia wito wa kufika mahakamani, lakini juhudi hizo ziligonga mwamba kwa kuwa hawakuwapata.

Wakili huyo alitumia kifungu namba 381(2) sura ya 20 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kuiomba hiyo kufanya chapisho la wito kwenye gazeti kuwataka kufika mahakamani.

Pia alitoa ombi kwa mahakama hiyo kuahirisha kusikiliza shauri hilo hadi Desemba 21, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa na itoe amri kwa Naibu Msajili wa Mahakama kutoa chapisho la wito huo kwenye magazeti ya serikali na binafsi yanayosomwa na watu wengi.

Akiahirisha shauri hilo, Maghimbi alisema kwa kuwa ni haki kwa kila mmoja kusikilizwa, ameagiza agizo kuchapishwa mara tatu kwa tangazo la wito wa kuitwa mahakamani kwa wajibu rufani hao kwa mujibu wa kifungu cha 381 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Juzi, Wakili Mosses Mahuna, anayemwakilisha Sabaya, alidai kuwa rufani hiyo haikuwa sawa kisheria ndiyo maana walitoa notisi ya kupinga kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) baada ya mteja wake kufikishwa mahakamani.

Alidai rufani inakinzana na kifungu cha namba 379 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Alidai kwamba kifungu namba 379(B) na kifungu kidogo cha pili kimeeleza kuwa rufani inatakiwa kufunguliwa ndani ya siku 45 tangu mahakama ilipotoa uamuzi au washtakiwa kuachiwa huru. Pia alidai kwamba uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, ulitolewa Juni 10, 2022 na rufani iliwasilishwa mahakamani Oktoba 28, miezi minne baadaye.

Wakili huyo alidai kwamba masharti ya kifungu cha 379(A) yameweka wazi kwamba DPP alipaswa kutoa notisi ya kukata rufani ndani ya siku 30 na notisi hiyo ilitolewa June 24, ikiwa tayari zimeshapita siku 40.

Kwa mujibu wa nyaraka za DPP, alidai zinaonyesha kuwa alipokea nakala ya hukumu Septemba 14, 2022, lakini rekodi za mahakama zinaonyesha nakala ya rufani hiyo walipatiwa Septemba 13.

Wakili Mahuna alidai sababu ya pili, DDP ameeleza kwamba kwa mujibu wa kifungu namba 379, kifungu kidogo cha 1 (A), ameweka kusudio la kukata rufani kwa waliokuwa washtakiwa saba akiwamo Watson Mwahomange, lakini wakati rufani inawasilishwa, ilionyesha amewakatia watu sita badala ya saba, hivyo wanashangaa kuona hakujumuishwa kwenye rufani hiyo.

Akijibu hoja hizo, Wakili Mwandamizi wa Serikali, Patrick Mwita, alidai ni kweli hukumu ilitolewa Juni 10, 2022 na waliwasilisha kusudio la kukata rufani Juni 24. Pia alidai kwamba hakuna ubishi kwa mleta rufani alileta sababu za kukata rufani Oktoba 28, 2022.

Hata hivyo, alidai kuwa tofauti iliyoko ni ndogo sana ambayo ni tafsiri ya kisheria kwa kuwa wanadai tangu kutolewa hukumu, zilianza siku kuhesabika na zilisimama tangu walipopeleka nia ya kukata rufani Juni 10 na ndio sababu wanadai ni nje ya muda.

Pia alidai kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 379, kifungu kidogo 1(A) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, vikisomwa kwa pamoja, hoja za wajibu rufani si sahihi.

Alidai kuwa kifungu cha 3791 (B) kimeelekeza kuwa huwezi kukata rufani bila ya kutoa sababu ya kukata rufani na kwamba iko wazi kwa kuwasilisha sababu za kukata rufani ndani ya siku 45 baada kupokea nakala ya hukumu.

Kuhusu ukomo wa muda, alidai imefafanuliwa katika Sheria ya Ukomo wa Muda Sura ya 89 kifungu cha 19(2), hivyo

tafsiri ya Mahuna kwamba inaanza kuhesabika tu baada ya hukumu si sahihi na huenda amechanganya mambo. Kutokana na hoja hizo aliomba mahakama kutupilia mbali hoja hizo na kuruhusu kesi hiyo kuendelea.

Kutokana na hoja za pande zote, Jaji Maghimbi aliahirisha kesi hiyo jana ili kutoa uamuzi wa kusikilizwa kwa rufani hiyo au la.

# Shahidi aangua kilio mahakamani

**Na Grace Gurisha**

SHAHIDI Samwel Thomas ameangua kilio ndani ya kizimba cha mahakama wakati akimtetea rafiki yake, Amani Filipo (38), anayedaiwa kumuua askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Sajenti Mensah, kwa kumpiga risasi huku akidai kuwa wao hawajaua.

Hali hiyo ilitokea jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakati Thomas akitoa ushahidi wake huku akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Hassan Kiangio.

Baada ya shahidi huyo kuanza kulia huku akidai kuwa wao hawajaua mtu, rafiki yake ambaye ni mshitakiwa katika kesi hiyo, naye alianza kulia huku akiwa ameinamisha kichwa chake chini, wote wakiwa ndani ya vizimba vya Mahakama.

Kutokana na hali hiyo, Wakili Kiangio alimsogelea karibu na kuanza kumbembeleza shahidi kwa sababu alikuwa amesimama akamtaka akae kwanza na pia ajitahidi kujikaza na anyamaze. Thomas alitoa kitambaa chake na kuanza kujifuta machozi huku akiendelea kulia.

Hali hiyo ilisababisha Hakimu Mbuya asimamishe usikilizwaji wa kesi kwa muda kuanzia saa 6:09 mchana hadi saa 6: 18 ili mshitakiwa na shahidi warudi katika hali za kawaida.

Hakimu Mbuya aliagiza maji chupa mbili ili wapewe marafiki hao na karani alimpa shahidi Thomas maji na mshtakiwa alipewa na askari Magereza.

Kwa sababu mshitakiwa alikuwa analia huku akiwa ameinamia chini, askari Magereza alimshtua ili anywe maji aliyoletewa kwa lengo la kumuweka sawa. Kulipita ukimya wa dakika kadhaa, Hakimu Mbuya alimuuliza shahidi kama yuko vizuri, akamjibu kuwa yuko sawa wanaweza kuendelea. Kabla ya kuendelea, Wakili Kiangio alimwomba aachane na mambo yaliyopita yeye ni shahidi anatakiwa kuzungumza.

Hayo yote yalitokea, wakati Thamos alikuwa anaelezea kwamba alifikishwa Kituo cha Polisi Oysterbay na askari polisi Ben Magufuli ili kumsaidia rafiki yake Amani ambaye anatuhumiwa na kesi ya mauaji.

Alidai kuwa alipofika kituoni hapo, aliingizwa kwenye chumba cha upelelezi na kukutana na askari anayeitwa Ndege ambaye alitoa gazeti na akalifunua na kumuonesha picha Thomas na kumweleza" "Unaona mmeua nyie?" Hapo ndipo shahidi akaanza kulia.

Baada ya kumaliza kulia, Thomas alidai kuwa aliwekwa mahabusu na huko alikutana na watu watano ambao alikwenda nao Hospitali ya Taifa Muhimbili Julai 22, 2016 kwa ajili ya kuangalia wagonjwa siku ambayo tukio la mauji lilitokea.

Alidai kuwa alikaa mahabusu mwezi mmoja kuanzia Julai 23, 2016 akiwa na Stewart Mang'ombe, Amani Filipo, Michael Marwa na Samwel Thomas na kwamba hadi anaachiwa, hakuwahi kuandika maelezo na pia hajui sababu ya yeye kuachiwa katika kesi hiyo.

Alidai kuwa mke wake, Felister Emmanuel, baada ya kupata taarifa kuwa yuko mahabusu kwa tuhuma za mauaji, alikatiza likizo yake na kwenda Dar es Salaam, alifikia kituoni kwa sababu yeye ndiye alikuwa na ufunguo wa nyumbani kwao.

"Lakini polisi walikataa kumpatia funguo kwa sababu walitaka kwenda kupekua nyumbani kwangu. Walinifunga kitambaa cheusi usoni na kuniweka kwenye gari nikiwa na mke wangu. Waliponifungua nilikuwa nyumbani kwangu wakapekua hawakukuta kitu," alidai Thomas.

Filipo anadaiwa kumuua Sajenti Mensah kwa kumpiga risasi baada ya kumvamia katika kibanda cha askari polisi cha kupumzikia kilichoko maeneo ya Sayansi Kijitonyama, Dar es Salaam, kwa lengo la kutaka kupora.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru (wa tatu kushoto), akiwa na maofisa wa benki hiyo, wawakilishi kutoka Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) wakionesha takwimu za mafanikio yaliyopatikana kwenye mauzo ya hati fungani ijulikanayo NBC Twiga Bond, jijini Dar es Salaam jana. NBC ilikusanya Sh. bil. 38.9 ikilinganishwa na Sh. bil. 30 zilizotarajiwa kukusanywa hapo awali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wawashtaki viongozi wilaya kwa Rais Samia madai kuporwa maeneo

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wananchi 13,000 kutoka vijiji vinne vya Kata ya Nyatwali Wilaya ya Bunda, wameulalamikia uongozi wa wilaya hiyo wakidai unatumia jina la Rais Samia Suluhu Hassan kutaka kuwapora maeneo yao.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, wawakilishi wa wananchi hao walisema Katibu Tawala wa Wilaya, Salim Cherera, amewaagiza wananchi hao waondoke katika maeneo yao kwa madai kuwa amepokea waraka kutoka kwa Rais Samia kuwataka waondoke haraka.

Diwani wa Nyatwali, Malongo Mashimo, alisema: "Katibu Tawala Cherera alikuja kama mlivyoshuhudia kwenye kikao akasema kuwa Rais ameandika waraka wa kutaka wakazi wa vijiji vinne vya Kata ya Nyatwali ambavyo ni Kariakoo, Tamau, Serengeti na Nyatwali kuondoka mara moja."

Malongo alisema Katibu Tawala huyo aliendesha kikao na ajenda kuu ilikuwa ni Rais Samia ameagiza watu wote wa Kata ya Nyatwali kuondoka mara moja katika maeneo yao.

"Baada ya tamko hilo, uongozi wa kata ulianza kuhoji kwa nini Katibu Tawala aendeshe kikao kwa niaba ya



Diwani wakati si utaratibu. Pia kwa nini polisi wengi kiasi hiki kwani kuna vita?," alisema Malongo.

Alisema katika kikao hicho, wananchi waliomba kuonyeshwa waraka huo unaodaiwa umetoka kwa Rais Samia, lakini katibu tawala huyo aliwaambia kuwa hawaruhusiwi kuonyeshwa nyaraka za serikali.

Diwani Malongo alisema Desemba 12, mwaka huu, kilifanyika kikao cha viongozi wa kata alichokiandaa yeye kwa agizo la DAS ambaye alifika na timu yake na baadhi ya maofisa aliodai wametoka Ikulu na wametumwa na Rais Samia.

Wazee wa Kata ya Nyatwali wakiongozwa na Mwenyekiti Mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Bunda, Alfred Malagira, walisema watapigania haki ya wakazi wa Nyatwali mpaka mwisho kwa kuwa jambo hilo lilianza tangu mwaka 2002 lakini dhuluma hiyo ilidhibitiwa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda.

Malagira alisema wanaushangaa uongozi wa wilaya kuja na suala hilo kwa kutumia nguvu kubwa ya Jeshi la Polisi na maneno ya kumsingizia Rais Samia kuwa amewaagiza kuwaondoa wananchi wa eneo hilo.

"Kutokana na hali hiyo tumefunga safari kutoka Bunda kuja Dar es Salaam kumwona Makamu Mwenyekiti wa CCM, Abdulrahman Kinana, ili atupeleke kwa Rais Samia kufikisha kilio chetu hiki," alisema Malagira.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Bunda, Cherera, alipoulizwa suala hili kwa njia ya simu, alisema wanaendesha vikao na wananchi wa eneo husika na kwamba hazungumzi na watu wengine.

"Sisi tunaheshimu sana vyombo vya habari. Kama unataka kujua suala hili funga safari kuja Bunda, tutakupa ufafanuzi kwanini tunataka kuwahamisha," alisema.

## Mwekezaji aondolewa hotelini chini ya ulinzi

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

RAIA wa Uturuki, Erkan Acikel, ameondoshwa katika hoteli pamoja na vifaa vyake chini ya ulinzi wa polisi wakiwa na silaha za moto baada ya kushindwa kuheshimu mkataba wa uendeshaji wa hoteli tangu alipokodishwa Mei, mwaka jana.

Kazi ya kumwondosha pamoja na wafanyakazi wote, ilisimamiwa na ushirika wa mnada wa Kumekucha wakiongozwa na Msaidizi wa Katibu wa Ushirika huo, Mansab Alawi Abdalla, baada ya mwekezaji huyo kushindwa kesi mara tatu mahakamani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kuondoshwa kwa mwekezaji huyo, mmiliki wa Hoteli ya Sipano Beach Lodge, iliyoko Kiwengwa, Peter Sipano, aliwataka wamiliki wa hoteli wazalendo kuwa makini katika kukodisha watu kutoka nje baada ya kujitokeza wimbi la wawekezaji matapeli visiwani hapo.

'Tulifunga mkataba wa uedeshaji wa hoteli na Kampuni ya Zan Food, Mei mwaka jana kabla ya kuibuka mgogoro baada ya Erkan Alikel kuwa mzito kulipa gharama za uendeshaji wa hoteli.

Sipano alisema mkataba wa ukodishwaji ulimalizika Novemba, mwaka jana lakini mwekezaji huyo na mdogo wake, Erdal Acikel pamoja na Firat Dag, waligoma kuondoka na kuanza kuvunja masharti ya mkataba kwa kuvunja sehemu ya hoteli na kukata miti ya minazi na mivinje.

"Wamesababisha uchakavu mkubwa sehemu ya juu. Hoteli imeanza kuvuja. Kwa muda mrefu wameshindwa kufanya matengenezo kinyume cha masharti ya mkataba wa ukodishwaji, alisema.

Sipano alisema baada ya kuanza kudai kurejeshewa hoteli yake, Alikel alianza kufungua kesi za uongo dhidi yake kwa kushirikiana na baadhi ya viongozi wa serikali na kulazimika kukaa mahabusu zaidi ya miezi mitatu baada ya kubambikiwa kesi ya kuteka nyara na kuiba kwa kutumia silaha kikiwamo kirungu cha Mmasai. "Kwa kweli nashukuru sana mahakama kesi zote za uongo nimeshinda kabla ya Mahakama Kuu kutoa amri ya kuwataka kuondoka katika hoteli baada ya kushindwa kuheshimu masharti ya ukodishwaji kinyume cha mkataba," alisema.

Alisema hoteli yake ina sehemu mbili ikiwamo hoteli na myumba ambayo anaishi na familia yake lakini baada ya kukodisha waturuki hao, walimzuia kutumia sehemu ya mbele ya uwanja na kuanza kumsingizia amewateka nyara na kuwaibia kwa kutumia silaha akiwa na kundi la watu jambo ambalo ni uongo.

Sipano, maarufu kama Mmasai, alisema anajiandaa kufungua kesi ya madai dhidi ya raia hao wa Uturuki baada ya kusababisha hasara ya karibu Sh. bilioni moja pamoja na mateso yaliyotokana na kesi za uongo kabla ya kufutwa na Mahakama Kuu ya Zanzibar

Katibu Msaidizi wa Ushirika wa Mnada wa Kumekucha, Mansab Alawi Abdalla, alisema wamelazimika kuwaondoa kwa nguvu wawekezaji hao baada ya kupokea amri ya Mahakama Kuu.

Mahakama imekuwa ikiwataka kuondoka lakini wamekuwa wazito ndiyo maana ushirika wa mnada wa kumekucha kwa kushirikiana na polisi tumelazimika kuwaondosha kwa nguvu wafanyakazi na kufunga hoteli yote, baada ya vifaa vyao kutolewa na kuwekwa nje," alisema Mansab.

Sheha wa Shehia ya Kiwengwa, Machano Pandu Machano, alisema mwekezaji huyo tangu kukodishwa hoteli, ameshindwa kuheshimu masharti ya mkataba na kusababisha mgogoro.

TRA

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA
## MATUMIZI YA NAMBA YA UTAMBULISHO (TIN) SAHIHI KWA WAAJIRIWA NA AINA YA AJIRA

Mamlaka ya Mapato Tanzania (“TRA” au “Mamlaka”) inapenda kuwakumbusha waajiri wote kuhusu uzingatiaji wa matumizi ya TIN sahihi kwa waajiriwa wote katika uwasilishaji wa ritani za Pay as You Earn (PAYE). Mamlaka imefanya maboresho katika mfumo wa uwasilishaji ritani ambapo kushindwa kutumia TIN sahihi kutakwamisha uwasilishaji wa ritani sahihi kwa waajiri katika mfumo huo na hivyo kupelekea usumbufu usio wa lazima ikiwemo riba na adhabu.

Ikumbukwe kuwa, Mamlaka imekuwa ikuwakumbusha waajiri wote kuhakikisha kuwa waajiriwa wao wana TIN na zinatumika kikamilifu sawa na matakwa ya **kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438.** Pamoja na ukweli kwamba waajiri wengi wameonesha mwitikio chanya bado kuna baadhi ya waajiri ambao wameshindwa kusimamia matakwa hayo ya kisheria kwa kuendelea kuwasilisha ritani za PAYE bila kutumia TIN sahihi za waajiriwa au kutumia **TIN 999 999 999**.

Kufuatia hilo, Mamlaka inapenda kuwakumbusha waajiri na waajiriwa wote kuhakikisha kuwa wanazingatia takwa hili la kisheria la kuhakikisha matumizi sahihi ya TIN katika uwasilishaji wa ritani ya **PAYE** kuanzia mwezi **Disemba, 2022**. Mfumo wa uwasilishaji ulioboreshwa ***(Upgraded e-filing)*** utashindwa kupokea majina ya waajiriwa wasio na TIN sahihi na hivyo kuathiri usahihi wa ritani husika. Sambamba na matumizi ya TIN sahihi, waajiriwa wanakumbushwa kuhakikisha wanaweka rekodi sahihi za ajira za waajiriwa wao kati ya ***ajira ya msingi (Primary Employment) au ajira ya ziada (Secondary Employment).***

Ikumbukwe kuwa TIN hutolewa bure na upatikanaji wake ni rahisi ambapo kwa waajiriwa wenye namba za usajili inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), wanaweza kuomba TIN kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa **Online TIN Registration** kupitia tovuti ya TRA (www.tra.go.tz). Waajiriwa wasio na namba ya NIDA wanakumbushwa kutembelea Ofisi za TRA ili kupatiwa TIN.
Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia:

| | |
|---|---|
| **Tovuti** | : **www.tra.go.tz** |
| **Namba za Simu bila malipo** | : **0800 750 075 au 0800 780 078** |
| **WhatsApp** | : **0744 23 33 33** |
| **Barua pepe** | : **huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz** |

***“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”***

Imetolewa na;

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

17195002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wamachinga wasikilizwe kilio chao

**JUZI** Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA), ilitangaza kuanza msako kwa wafanyabiashara wanaouza bidhaa bila kutoa risiti na wateja wanaonunua bidhaa hizo ambao hawadai risiti ikiwalenga zaidi wanaofanya biashara eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam.

Mkakati huo pia unahusisha kuwabana wafanyabiashara ndogondogo (wamachinga) wawe na mashine za kutoa risiti za mtandao kwa kila bidhaa wanazouza katika maeneo yao.

Hata hivyo, hatua hiyo ya TRA kuangalia eneo moja pekee imepingwa na wafanyabiashara hao ndogondogo na kuitaka Mamlaka hiyo kuangalia wafanyabiashara maeneo yote nchini.

Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA), limesema ni muhimu kwa TRA kutoza kodi wamachinga wote nchini badala ya Kariakoo pekee.

Shirikisho hilo limesema halina tatizo katika kulipa kodi, lakini kuwe na utaratibu shirikishi ambao utawalipisha kodi wote badala ya kuwalenga wachache.

Mwenyekiti wa umoja huo, Steven Lusinde, aliomba TRA kuondoa utaratibu wa kuwataka wafanyabiashara hao wadogo kuwa na mashine za risiti za kielektroniki (EFD) kutokana na gharama ya kuzipata kutoendana na mitaji yao.

Vilevile, alidai utunzaji wa kifaa hicho na mazingira wanayofanyia kazi utakuwa mgumu.

Mamlaka husika inapaswa kusikiliza hoja zinazotolewa na machinga hao ili kuwapo na maelewano badala ya kutumia nguvu ambayo inaweza kuleta madhara.

Pande mbili zitakapokutana na kusikilizana bila shaka hakuna kitu kitakacho haribika kwa sababu pale ambapo hapakueleweka patatolewa ufafanuzi ili mambo yaweze kwenda sawa.

Hoja ya kutaka wamachinga wanaofanya biashara maeneo yote nchini kulipa kodi ni ya msingi ili kusionekane eneo moja kuumizwa na mengine yakiachwa bila kulipa kodi na kukosesha mapato kwa serikali.

Kadhalika, kwenye suala la mashine za EFD ni muhimu kukatolewa elimu ya kutosha ili kuepusha malalamiko ya gharama na utunzaji.

TRA iliamua kuja na mkakati wa kuwabana wafanyabiasahra hao baada ya kubaini kuwa kuna udanganyifu unaofanywa na baadhi yao kupitia wamachinga kwa kuwatumia kuuza bidhaa bila kulipa kodi inavyotakiwa.

Kwa mujibu wa Mamlaka hiyo wafanyabiashara wakubwa wanakwepa kodi kupitia wamachinga na katika kufanikisha mikakati waliyojiwekea wameshafanya usajili wa wamachinga 5,373 ambao wamepewa TIN namba na kupewa mashine.

Ambao hawajasajiliwa wametakiwa kujisajili haraka.

Kwa wastani katika eneo la Kariakoo TRA wamekuwa wakikamata wafanyabishara na wateja wasio waaminifu kati ya 50 hadi 60 kwa mwezi na waliowafungulia mashtaka ni wafanyabishara 13, baada ya kuonesha usugu wa udanganyifu huo baada ya kuwakamata mara kadhaa na kuwaonya.


Uamuzi huo wa kuwanasa wateja na wafanyabiashara wasiotoa risiti unatokana na juhudi za awali walizofanya za kuweka mabango ya elimu ya kukumbusha umuhimu wa kuchukua risiti halali.

Pia, Mamlaka hiyo itahakikisha inabandika stika zenye kuonesha TIN namba za mwenye duka kwenye kila duka Kariakoo ili kila mteja aweze kuhakiki taarifa zilizopo kwenye risiti ya EFD wanazopewa.

TRA inaamini kupitia mkakati huo wataboresha usimamizi wa kodi katika eneo hilo na wanakusudia katika kipindi cha Desemba watakukusanya mapato ya Sh. bilioni 19.

Ukusanyaji wa mapato uwe rafiki ili hata anayelipa kodi atoe kwa moyo asijisikie kuonewa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Halfani Chusi

# Ukamataji bodaboda staili hii ukemewe

**UKIWA** kwenye usafiri wa umma yaani daladala, ndani ya Dar es Salaam, unapopita kwenye taa za eneo Tazara, kinachoonekana hapo ni misuguano katika kukamatana askari na waendesha bodaboda.

Ukitega sikio unanasa minong'ono ya waendesha bodaboda hao wakipabatiza jina la 'Machinjioni' wakimaanisha kwamaba, lile eneo huwezi ukapita salama kama sehemu zingine. Ni maungio ya barabara zenye taa, ambazo husababisha magari na bodaboda kusimama kusubiri kuruhusiwa, hivyo wanadai askari waliovaa nguo za kiraia hutumia nafasi hiyo kuwakamata na kuwachomolea funguo, ili wasiweze kukimbia.

Lakini, utaratibu mwingine wanaotumia unaolalamikiwa ni kumfuatilia mwendesha bodaboda kwa nyuma na pikipiki yake, baada ya hapo wanamkalia kwa mbele na kumkamata.

Ni ukamataji ambao staili yake inatia shaka na hata kuwa sababu ya bodaboda, wengi kushindwa kusimama mataa, lakini unahatarisha maisha ya mtumiaji wa chombo. Nikiwa maeneo hayo, nilishuhudia mmoja ya waendesha bodaboda baada ya kushtukia kuwa anaviziwa na askari aliyekuwa amevaa kiraia, akaanza kuhaha hali iliyomlazimu kuvuka na taa nyekundu.

Baadaye kidogo, nikashuhudia ugomvi mkubwa kati ya askari na mmoja wa bodaboda aliyekamatwa, ugomvi huo ulitokana na dereva huyo kudai hawezi kukamatwa na askari aliyeva kiraia.

Bodaboda huyo aliongea kwa sauti kubwa: "kwanini unanikamata wewe nani? Mmezoea nyie vya bure kwanza hujavaa sare kama mwizi mimi ntakujuaje? hapa barabarani sitoki na siendi kokote kwanza nipe funguo ya pikipiki yangu unanichelewesha!"

Basi lile zogo lilidumu kwa muda baadaye askari yule akamrudishia yule dereva funguo yake na akaendela na safari yake kama kawaida.

Kibaya zaidi, wanapomkamata bodaboda wanamuamuru kumshusha yule abiria aliyempakia bila kujali atapataje usafiri wa kufika anako kwenda. Hali hiyo imekuwa, ikisababisha mtafaruku mkubwa kwa kuwa askari hao, hawajali haki ya abiria wala dereva kwa muda huo kitu ambacho ni kinyume cha utaratibu.

Hili suala linapaswa kukemewa kwa sababu katika ukamataji kama huo hapakosekani madhara ikiwamo ajali kwa sababu hiyo, sio njia rasmi ya kumkamata dereva bodaboda mwenye makosa.

Mbali na hivyo, pia unahatarisha usalama wa wasafiri waliopo katika usafiri wa umma kwa sababu bodaboda wengi huwa ni wabishi wanapotiwa nguvuni na askari.

Kuna haja ya askari kikosi cha usalama barabarani kuangalia njia nyingine, ya kuwakamata bodaboda, lakini sio kuwavizia maeneo ya taa kwa sababu athari yake ni kubwa hata kwa miundombinu ya barabara.

Na utaratibu huo sio kwa mataa ya eneo hilo tu bali hata maeneo mengine kama vile mataa ya veta, bado utaratibu huo, unatumika kwenye kuwakamata madereva hao.

Ni wajibu kwa askari kukamata chombo cha usafiri na kukifanyia ukaguzi lakini katika njia ambayo haitomuathiri mtu wala kuharibu miundombinu ya chombo chake. Michael Mnyawami, dereva bodaboda Tazara, anasema kinacho fanyika pale ni ukatili kwa bodaboda kwa sababu wanakamatwa kama majambazi.

"Ule ukamataji sio mzuri kabisa, huna hili wala lile unaona pikipiki imekukalia mbele huwezi kwenda ghafla funguo inachomolewa hawajali kama unaabiria au umetoka mbali wao wanacho angalia pale ni kukuwajibisha tu.

"Kwa hiyo, kwangu huo sioni kama ni utaratibu unaotakiwa kwa sababu wapo walio pigana na polisi kwa ajili ya huo ukamataji , nakumbuka serikali iliwahi kuzuia ukamataji wa aina hiyo," alisema .

Naona kwa sasa tena wamerudia ile tabia, hili jambo linatupa shida sana sisi madereva, sio kwamba huwa hatupendi kusimama mataa sasa kwa hali kama hiyo unanzaje kusimama?"alihoji dereva huyo.



Mkazi wa Nanyumbu mkoani Mtwara, Selemani Mpepe (wa pili kulia), akiwa na rafiki zake baada ya kukabidhiwa hundi ya Sh. milioni 4 alizoshinda kama sehemu ya bonasi ya Bonge kwa kubashiri matokeo ya michezo mbalimbali duniani kwenye BikoSports. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwamko chanjo Uviko-19 waongezeka

**Na Elizabeth Zaya**

MGANGA Mkuu Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, amesema mwamko wa wakazi wa mkoa wa huo chanjo ya Uviko-19 umeongezeka tofauti na ilivyokuwa awali wakati chanjo zinaletwa nchini.

Dk. Mfaume alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na Nipashe hivi karibuni, ofisini kwake mkoani Dar es Salaam.

Alisema ni vyema kama kuna wengine ambao hawajachanja ikiwamo kwa makundi ya wenye magonjwa yasiyoambukizwa kujitokeza kwa hiari kuchanja.

"Tunawashauri wafanye hivyo, kwa sababu chanjo inawasaidia hata kujikinga na magonjwa mengine ambayo ni hatarishi kwao," alisema Dk. Mfaume.

Alisema mwanzoni watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi pamoja na magonjwa yasiyoambukizwa walikuwa na hofu kwamba huenda wakapata athari kubwa baada ya kuchanja, lakini hakuna aliyepata athari hata baada ya kuchanja.

"Kwa hiyo hata ukiangalia kwenye kumbukumbu zetu, hakuna kundi ambalo liko nyuma kwa sasa katika chanjo kwa mkoa wa Dar es Salaam, yote yalijitokeza kwa wingi baada ya kupata elimu sahihi na baada ya kuona shuhuda kwa wenzao walioanza kufanya hivyo. Mwanzoni kundi kubwa ambalo lilionekana kusita ni la wanawake, huku wanaume ndio walikuwa mstari wa mbele kujitokeza kuchanja, lakini kwa sasa wote wanachanja," alisema Dk. Mfaume.

Alisema lengo kwa mkoa huo ni kuchanja watu milioni 3.8, lakini mpaka sasa watu milioni 3.2 wamechanjwa na mpaka mwisho wa mwezi Desemba watakuwa wamekamilisha.

"Tumebakiza asilimia chache wakazi wa Dar es Salaam wote wawe wamechanjwa na uzuri wa lengo letu kufikia mwisho wa mwezi huu tutakuwa tumekamilisha wote asilimia 100. Na sayansi inatuambia kwamba asilimia kubwa wakichanja wanawasaidia na wengine ambao hawajachanja, japo tunataka wote wachanje," alisema Dk. Mfaume. Vile vile, baada ya kukamilisha lengo, wanaendelea kuhamasishana kuhakikisha watu wote katika mkoa huo wa Dar es Salaam wanachanja.

Lengo walilojiwekea kuchanja ni endelevu kwa sababu watu wanazaliwa, wanakua na kuongezeka kila siku.

"Hatujasema ugonjwa umekwisha, kikubwa zaidi tunachosisitiza ni watu kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga kama ambavyo wamekuwa wakishauriwa na wataalamu," alisema Dk. Mfaume.

# Canada yamwaga mabilioni kuimarisha usawa wa jinsia

**Na Sabato Kasika**

CANADA imetenga Dola za Kimarekani milioni 450 kwa ajili ya usawa wa kijinsia kama njia ya uwezeshaji endelevu wa mradi wa Sauti ya Wanawake Katika Uongozi (WVL) ili kusaidia taasisi za ndani za haki za wanawake katika nchi 30 zinazoendelea ikiwamo Tanzania.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Operesheni za Maendeleo katika Ubalozi wa Canada hapa nchini, Brownwyn Cruden, Dar es Salaam jana, katika mkutano wa Wanamtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania.

Mkutano huo ulifanyika katika viwanja vya makao makuu ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Mabibo, na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wanaopinga vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Alisema katika fedha hizo, Dola milioni 300 ni kwa ajili ya mfuko wa usawa zikilenga uwezeshaji endelevu na kwamba Dola zingine milioni 150 ni kwa ajili ya mradi wao pendwa wa Sauti ya Wanawake Katika Uongozi (WVL) ili kusaidia taasisi za ndani zinazotetea haki za wanawake.

"Canada inafurahi kuwa moja ya nchi chache duniani zilizopitisha sera ya mambo ya nje ya usawa wa kijinsia na sera ya usaidizi wa kimataifa ya wanawake. Tunajua jamii inakuwa na mafanikio zaidi amani, usalama na umoja pale haki za wanawake zinapoheshimiwa na wanawake wanathaminiwa na kuwezeshwa katika jamii," alisema Brownwyn.

Aliongeza kuwa nchi yake inasaidia pia miradi katika ngazi ya jamii na taifa kwa ajili ya kutokomeza ukatili wa kijinsia, kuhamasisha usawa kwa wanawake na kuwasaidia kupata ujuzi wanaouhitaji.

"Aidha, katika kazi zetu kwenye sekta ya elimu, huduma ya afya, utawala bora na ukuaji wa uchumi shirikishi, tunawaweka wanawake kuwa ni kipaumbele cha jitihada zetu," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Women Fund Tanzania (WFT), Prof. Ruth Meena, alisema rushwa ya ngono inadhalilisha na inaua, hivyo jamii nzima inapaswa kuingia vitani kupambana nayo.

Prof. Meena aliomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), isiichanganye rushwa ya ngono na zingine na itafutiwe njia nyingine ya kupambana nayo ili waathirika wawe huru kutoa taarifa.

Mkurugenzi wa Elimu Kwa Umma wa TAKUKURU, Joseph Mwaiswelo, alitaka jamii kuwa huru kutoa taarifa za rushwa ya ngono kuanzia ngazi ya chini hadi ofisi za taasisi zilizo karibu.

"Lakini pia mtu akifika kutoa taarifa, asiseme kokote, iwe ni siri yako, kwani kufanya hivyo wakati mwingine kunaweza kukwamisha uchunguzi wa kesi husika," alisema Mwaiswelo.

Alisema mtu anapotoa taarifa za rushwa hiyo na kisha kwenda kuzungumza kwingine mtaani au kwa ndugu, anaweza kukutana na vitisho na kusababisha aogope kwenda kutoa ushahidi.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **BROVITAS COMPANY LIMITED,MANGWEMBE 2011.CO.LTD na MASE INTERNATIONAL LIMITED** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD**. Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | BROVITAS COMPANY LIMITED | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | STEVEN JOVINUS NGONYANI | NYUMBA YENYE HATI YA MILIKI NO.515 KITALU Y | MFARANYAKI - SONGEA |
| MANGWEMBE 2011.CO.LTD | | | |
| 2 | SHABAN S MAGANGA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIBAHA - PWANI |
| 3 | HAJI A SILAYO | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO, MALI YA KHAMBI SUDI RAMADHANI | KIBAHA - PWANI |
| 4 | FERDINAND H MOSHI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO, MALI YA MARY SEVERIN NJAU | MAPINGA - BAGAMOYO |
| MASE INTERANATIOL LIMITED | | | |
| 5 | CHARLES J WANKOREGE | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | NYAROMA - SIRARI |
| 6 | NYAMAHEMBA W NGENGE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | REMBIRWI - TARIME |
| 7 | CHARLES G MGESI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KINYAMBI - NKENDE |
| 8 | KULWA W NYANGURU | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | GASAMARA -TARIME |
| 9 | PETER CHACHA NYAWAMBURA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | SIRARI - GWITIRYO |
| 10 | HUSEIN HAMAD NKUNGU | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KISHIRI – IHUSHI - MWANZA |
| 11 | KUBIA J WILLSON | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIMUSI - TARIME |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo mahali ilipo.
3. Mnunuzi atakayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipwa kulingana na makubaliano ya benki na mnunuzi.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA

17195302

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Mase International Limited**
**S.L.P Mwanza**
**Namba za simu:**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Mangwembe 2011.CO.LTD**
**S.L.P Mwanza**
**Namba za simu: 0713203040 /0752632033**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Brovitas Company limited**
**S.LP Songea**
**Namba za simu; 0763801591**

**NA**

**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Namba za simu: 0768790399, 0754774949**


## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# PM aagiza watumishi kuhamia nyumba za serikali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ameagiza watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele mkoani Katavi, kuhamia mara moja kwenye nyumba 11 zilizokuwa za wajenzi wa barabara ya Inyonga-Mlele ambazo zimekabidhiwa kwa halmashauri hiyo.

Watumishi ambao ameagiza wahamie kwenye nyumba hizo ni Ofisa Usalama wa Wilaya (DSO), Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Mlele {OCD}, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini {TARURA}, Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO) na watumishi wengine wa hospitali ya wilaya.

Majaliwa (pichani) alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo baada ya kujiridhisha kuwa zimetelekezwa na zinaharibika kwa kukosa uangalizi.

"Watumishi wanahangaika hawana makazi. Nyumba zimeachwa nyasi zimeota hadi kwenye korido. Watumishi wote wanaopaswa kuhamia katika nyumba hizi baada ya kumaliza mkutano huu kila mmoja aende kwenye yake na ahamie. Mkurugenzi naomba orodha ya majina ya watakaohamia," alisema.



Nyumba hizo 11 zenye ukubwa tofauti, mbili zina uwezo wa kuchukua familia nne kila moja ni za kisasa na zilikabidhiwa kwa mkurugenzi mtendaji wa halmashauri Novemba, mwaka huu na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) baada ya kukamilika kwa mradi wa barabara.

Aidha, Majaliwa aliutaka uongozi wa halmashauri kuweka utaratibu wa kushirikisha wadau wa sekta binafsi katika kuleta maendeleo kwenye wilaya. Pia aliwataka watumishi hao kuhakikisha kila kazi wanazozifanya zinakuwa na matokeo chanya kwa jamii.

Awali, Waziri Mkuu alikagua barabara ya lami ya Inyonga-Mapili yenye urefu wa kilomita 11.7 iliyogharimu Sh. bilioni 8.69. Barabara hiyo ni sehemu ya barabara ya Inyonga-Ilunde-Kishelo inayokwenda hadi kwenye mpaka wa mkoa wa Katavi na Tabora ikiwa na urefu wa kilomita 96.

Wakizungumza baada ya ukaguzi huo, baadhi ya wakazi wa Mapili walimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo ambayo kukamilika kwake kutaimarisha huduma za usafiri wa watu na mizigo.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA HUDUMA YA MPITO KWA WAGUSWA WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA KUMBUKUMBU NA: REQ-00000075**

EACOP Ltd Tanzania, Kampuni ya Mafuta na Gesi inakaribisha Kampuni zinazojihusisha na Kilimo, Usambazaji wa Chakula zenye uzoefu, na ambazo ziko tayari kutoa Huduma za Usambazaji wa Chakula kwa Waguswa wa Njia ya Bomba katika Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

Bomba hilo litapita kwenye jumla ya Mikoa nane (8) ambayo ni **Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga.** Pia linagusa **Halmashauri za Wilaya 27** na **vijiji 231.**

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA**

Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (hapa ikijulikana kama "Mradi") unahitaji Ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Bomba pamoja na miundombinu mingine. Kwa sababu hiyo, Mradi unaratibu zoezi la Utwaaji wa Ardhi kwa waguswa walioguswa makazi na kiuchumi.

Ili Kupunguza athari za Uhamishaji wa Watu na Makazi, mradi unatarajia kutoa huduma ya mpito kwa waguswa wa Njia ya Bomba na miundombinu ya juu. Huduma ya chakula inatolewa kama nyongeza ya Fidia katika kusaidia Jitihada za Kaya iliyoguswa na Mradi kumudu kupatikana kwa chakula katika kipindi cha mpito (baada ya eneo la ardhi kutwaliwa na hadi urejeshaji wa hali za maisha ya mguswa kufikiwa). Chakula kitakachosambazwa kinajumuisha: Mahindi, Maharage, Mchele, Mafuta ya Kupikia na Chumvi.

Mradi unahitaji Kampuni zenye sifa, na uzoefu katika kutoa huduma ya usambazaji wa chakula kutoa huduma ya usambazaji wa Chakula katika vipenGele vitatu: 1) Ununuzi wa bidhaa za chakula, 2) Uhifadhi na Ufungashaji wa bidhaa za chakula , na 3) Usambazaji wa chakula kwa waguswa/Kaya zilizoguswa kila mwezi. Makadirio ya kiwango kinachohitajika ni kama inavoonekana hapo chini:

**Kipengele 1a: Ununuzi wa bidhaa za Chakula kwa waguswa/kaya zilizoguswa wenye athari zaidi kwa kipindi cha miezi 12**

| Mkoa | Idadi ya Vijiji | Makadirio ya Kiwango kwa Miezi 12 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mahindi (kg) | Mchele (kg) | Maharage (kg) | Mafuta (lt) | Chumvi(kg) |
| Kagera | 34 | 39,840 | 39,840 | 39,840 | 9,960 | 1,992 |
| Geita | 40 | 47,336 | 47,336 | 47,336 | 11,834 | 2,367 |
| Shinyanga | 16 | 14,280 | 14,280 | 14,280 | 3,570 | 714 |
| Tabora | 30 | 51,240 | 51,240 | 51,240 | 12,810 | 2,562 |
| Singida | 31 | 42,900 | 42,900 | 42,900 | 10,725 | 2,145 |
| Dodoma | 23 | 17,280 | 17,280 | 17,280 | 4,320 | 864 |
| Manyara | 11 | 25,740 | 25,740 | 25,740 | 6,435 | 1,287 |
| Tanga | 46 | 83,820 | 83,820 | 83,820 | 20,955 | 4,191 |
| **JUMLA** | **231** | **322,436** | **322,436** | **322,436** | **80,609** | **16,122** |

**Kipengele 1b: Ununuzi wa bidhaa za chakula kwa waguswa/kaya zilizoguswa wenye athari za wastani kwa kipindi cha miezi 6**

| Mkoa | Idadi ya Vijiji | Makadirio ya Kiwango kwa Miezi 6 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mahindi (kg) | Mchele (kg) | Maharage (kg) | Mafuta (lt) | Chumvi(kg) |
| Kagera | 34 | 224,280 | 224,280 | 224,280 | 56,070 | 11,214 |
| Geita | 40 | 240,366 | 240,366 | 240,366 | 60,092 | 12,018 |
| Shinyanga | 16 | 86,020 | 86,020 | 86,020 | 21,505 | 4,301 |
| Tabora | 30 | 98,140 | 98,140 | 98,140 | 24,535 | 4,907 |
| Singida | 31 | 167,700 | 167,700 | 167,700 | 41,925 | 8,385 |
| Dodoma | 23 | 89,640 | 89,640 | 89,640 | 22,410 | 4,482 |
| Manyara | 11 | 44,070 | 44,070 | 44,070 | 11,018 | 2,204 |
| Tanga | 46 | 104,170 | 104,170 | 104,170 | 26,043 | 5,209 |
| **JUMLA** | **231** | **1,054,386** | **1,054,386** | **1,054,386** | **263,597** | **52,719** |

- Muombaji anapaswa kuonyesha mnyororo wa utoaji huduma **uliopo** wenye uahkika wa kusambaza kiawango kinachohitajika wakati wote wa utekelezaji wa Mradi.
- Muombaji anapaswa kuonyesha **uthibitisho** wa Usajili katika mamlaka zinazohusika na afya na usalama wa chakula.

**Kipnegele 2: Kuhifadhi na Kufungasha bidhaa za chakula kwa kipindi cha miezi 12**

- Waombaji wanapaswa kuonyesha **Uthibitisho** wa Ghala analomiliki au alilokodi kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa.
- Waombaji wanapaswa kuonyesha **Uthibitisho** wa eneo la kufungashia bidhaa, teknolojia na vifaa vinavyotumika katika kufungasha bidhaa.

**Kipengele 3: Usambazaji wa bidhaa kwa waguswa/kaya zilizoguswa kwa kipindi cha miezi 12**

- Waombaji wanapaswa kuonyesha **Uthibitisho** wa vyombo/vifaa pamoja na mtandao wa Usafirishaji/Usambazaji wa bidhaa za chakula
- Waombaji wanapaswa kuonyesha **Uthibitisho** wa mfumo wa usambazaji, ugawaji, uhakiki wa wanufaika, pamoja na ufwatiliaji wa kiwango cha chakula kilichogawiwa kwa waguswa, pamoja na mbinu za kuzuia udanganyifu.

Waombaji wanapaswa kuleta maombi kwa Vipengele vyote. Waombaji ambao wangependa kutoa huduma kwa kipengele kimoja watapaswa kutoa sababu mahsusi za kufanya hivyo.

**VIGEZO MUHIMU**

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa Usajili wa Kampuni Kutoka katika Mamlaka zinazohusika na Usajili wa shughuli za Makampuni(BRELA, TBS, OSHA)
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni.
- Kampuni zinazotumia wasambazaji wa kutoka maeneo yaliyoguswa na mradi ziwasilishe taarifa za wasambazaji wao pia.
- Inashauriwa, muonyesha nia awe amekwisha jisajili au ametuma maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoajina msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Uthibitisho wa mtandao wa wasambazaji wa maeneo yanayopitiwa na mradi, ikielezea miundombinu muhimu kuwezesha usambazaji wa huduma ya chakula. Taarifa zionyeshe mawasilaino na eneo analopatikana msambazaji.
- Uthibitisho wa vifaa/maeneo ya kuhifadhia, kufungasha, na kusambaza chakula na hali ya ubora wa vifaa Pamoja na maeneo ya kutolea huduma
- Uthibitisho wa uwezo wa kukusanya na kutunza kiwango cha chakula kinachotakiwa kwa waguswa muda wote wa utekelezaji wa Mkataba.
- Uthibitisho wa mfumo na taratibu za kiafya na kiusalama unaotumiwa na Kampuni.

217196102

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (Ukubwa Usiozidi **MB20**) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **02/01/2023**. Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **REQ-00000075** HUDUMA YA MPITO KWA WAGUSWA.

**Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.**
**Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.**

**Muhimu:** EACOP itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP Ili kubaini makumpuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.





Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, akikagua daladala baada ya kulisimamisha eneo la Sinza Mugabe Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wasaidizi wa kisheria wahimizwa kutokomeza ukatili jinsia, migogoro

**Na Frank Monyo**

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amewataka watoa huduma za msaada wa kisheria kuwa mstari wa mbele kuwaelimisha wananchi na kuungana na serikali kutokomeza udhalilishaji, migogoro ya ardhi na usajili wa matukio ya kijamii hususani vyeti vya kuzaliwa.

Hayo aliyasema jana visiwani humo wakati wa kongamano la pili la mwaka la msaada wa kisheria mwaka 2022 lenye kaulimbiu 'Utumiaji Sahihi wa Njia Bora za Utatuzi wa Migogoro katika Masuala ya Msaada wa Kisheria.'

"Kwa kuwa mnafanya kazi karibu na watendaji wa serikali za mitaa, wakiwamo masheha, basi ni vyema mkashirikiana kuwasaidia wananchi kupata haki zao," alisema Abdulla.

"Niwatake masheha na watendaji wengine wa serikali, mwendelee kushirikana na watoaji msaada wa kisheria pamoja na kutambua kazi na juhudi zao kubwa kwani wanafanya kazi bila malipo yoyote ila wamejikubalisha kuisaidia jamii," alongeza.

Makamu wa Pili wa Rais aliwataka watoa msaada wa kisheria wote kuendelea kuitumikia jamii kuhakikisha upatikanaji haki na kuwa wabunifu katika kuhakikisha taasisi zao zinakuwa na nyenzo za kujiendesha kwa kutafuta miradi mbalimbali badala ya kila siku kusubiri kusaidiwa.

Aliongeza kuwa serikali kupitia uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, imejizatiti vya kutosha katika kuhakikisha wananchi wanapata haki lakini pia wanafuata Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na sheria zilizopo.

Abdulla aliwahakikishia watoaji msaada wa kisheria Zanzibar kuwa serikali kwa kushirikiana na Shirika la Msaada wa Kisheria (LSF) kuhakikisha watoaji msaada hao wanafanya kazi zao bila usumbufu wowote na kufanya jitahada mbalimbali za kuwasaidia ikiwamo kuwapatia mafunzo kadri hali itavyoruhusu.

# Wamshukuru mkandarasi kuwatatulia tatizo la maji

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

BAADHI ya wakazi wa Kata ya Vigwaza katika Halmashauri ya Chalinze, wakimamo wafugaji, wamekutana na kuishukuru kampuni ya ujenzi ya Estim kutokana na kuwasaidia kupata maji ili kukabiliana na ukame kwenye eneo lao.

Wamefikia hatua hiyo baada ya mkandarasi huyo kuanzisha utaratibu wa kuwapelekea maji kila siku kwa ajili ya kunywesha mifugo yao, majani, pumba na kuwachimbia visima.

Akizungumza kwenye shughuli hiyo iliyoambatana na maombi kwa mkandarasi huyo, iliyofanyika juzi katika Shule ya Msingi Mnindi, Diwani wa Vigwaza, Mussa Gama, alisema mkandarasi huyo ambaye amejenga barabara ya Vigwaza -Kwala amekuwa tofauti na wengine waliowahi kufanya kazi kwenye kata hiyo. Gama alisema kipindi cha kiangazi, wafugaji walikuwa wakisumbuka kutafuta maji na majani tofauti na ilivyo sasa kwa kuwa mkandarasi anawasaidia mahitaji hayo ili kukabiliana na ukame.

"Tunamwomba Rais (Samia Suluhu Hassan) mkandarasi huyu aangaliwe kwa jicho la tofauti. Zinapotokea kazi apewe kipaumbele kwani amekuwa akifanya mambo mengi ya kijamii kutatua vikwazo kwenye jamii jambo ambalo ni la fahari kwetu kujivunia uwapo wake," alisema Gama.

Gama alisema mbali na kufanya shughuli hizo, mkandarasi huyo amekuwa akitoa mashine yake kwa ajili ya kuchimbia barabara na kufanyia shughuli zingine za maendeleo ya wananchi na amejenga vyumba vya madarasa vya kisasa katika Shule ya Msingi Mnindi.

Mhandisi James Obeid wa Kampuni ya Estim, alisema mkurugenzi wao alifikia hatua ya kusaidia wananchi hao kutokana na kwamba kila magari yao yalipokuwa yakipita yakiwa kwenye ujenzi wa barabara, yalikuwa yakisimamishwa na wananchi wakiomba msaada wa kupatiwa maji.

Mhandisi Obed alisema kutokana na hali hiyo ya uhitaji wa maji, walilazimika kuanza utaratibu wa kuwapelekea wananchi maji kila siku pamoja na majani ili mifugo isife.

Katibu mstaafu wa Chama cha Wafugaji Tanzania, Magembe Makoye, alimpongeza mkandarasi huyo kwa anachokifanya kwa jamii kuwasaidia kuondokana na kikwazo cha maji na majani. Aliiomba serikali kumpa kipaumbele cha kazi pale zinapotokea.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Pwani, Ngobere Mfamau, alisema kitendo anachofanya mkandarasi huyo kinastahili kuigwa na makandarasi wengine kwa kusaidia wananchi mambo ya kijamii kwenye maeneo wanayofanyia kazi.

# Anayedai talaka ya mwanawe akwama kufika mahakamani

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA imekwama kuanza kusikiliza shauri la Rosemary Mayunga, anayetaka binti yake atoke kwenye ndoa kutokana na mdai huyo kutofika mahakamani.

Shauri hilo lilikuwa lianze kusikilizwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Francis Mhina.

Rosemary Mayunga alimfikisha mahakamani mkwewe Godwin Mmbaga, akiomba mahakama iamuru amchukue binti yake kwa ajili ya usimamizi na kumtunza kwa madai ana matatizo ya afya ya akili.

Mahakama ilipanga kuanza kusikiliza baada ya pande zote mbili kuwasilisha hoja zao na shauri liliahirishwa hadi Januari 9, 2023.

Rosemary anamtaka mwanawe Kuyega Mmbaga (48) awe chini yake na katika madai yake anaomba mahakama itoe amri ya kuteuliwa kumsimamia Kuyega anayeishi katika ndoa maeneo ya Upanga kwa madai anasumbuliwa na tatizo la afya ya akili.

Mwombaji anadai ni mama mzazi wa Kuyega Mmbaga na alimzaa mtoto huyo akiwa kwenye ndoa na mume wake Mayunga ambaye alifariki dunia.

Alidai mwaka 2002 Kuyega aliolewa na Mmbaga, walijaaliwa kupata watoto watatu, lakini mmoja alifariki dunia.

Alidai maisha ya Kuyega kwenye ndoa yametawaliwa na matatizo hakuna maelewano na mumewe Mmbaga hali inayosababisha aishi kwa mateso. Mama huyo alidai sababu za kuomba amri ya mahakama ni kutokana na matatizo yanayomkabili Kuyega ambaye mara kadhaa amekuwa akitaka kujiua.

Mwombaji aliambatanisha ripoti ya Dk. Frank Masao, ambaye ni Mkuu wa Kitengo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili inayoonesha Kuyega anasumbuliwa na afya ya akili.

Alidai Kuyega kwa tatizo alilokuwa nalo hawezi kusaini nyaraka yoyote kisheria na kwamba tatizo lake kwa asilimia kubwa lilichangiwa na mumewe Mmbaga.

Alidai Mmbaga amekuwa akimtishia kumuua kwa bastola mkewe na taarifa hizo waliziwasilisha Kituo Kikuu cha Polisi.

"Amekuwa akimkataza kusoma Biblia badala yake anamlazimisha kusoma Kuran tukufu, kanisani haendi," alidai Rosemary katika hati yake ya madai.



Goodlucky Busago kutoka Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), akielimisha wanafunzi kuhusu madhara ya rushwa ya ngono, Kigogo Luhanga Dar es Salaam juzi. Kwa sasa shirika hilo linafanya kampeni ya kupinga rushwa hiyo mtaa kwa mtaa mkoani Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ndejembi awapa mbinu waajiri uhaba watumishi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewataka waajiri katika taasisi za umma kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi katika baadhi ya kada.

Katika kufanya hivyo, amewataka kuwabaini watumishi wenye ujuzi wa kada hizo na kuwaendeleza kielimu ili wapate sifa ya kuziba nafasi zilizo wazi badala ya kusubiri serikali kutatua changamoto hiyo.

Akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni jana, Ndejembi alisema waajiri wanapaswa kubaini watumishi wenye ujuzi na sifa ili kuwajengea uwezo kiutendaji kupitia programu za mafunzo kwa kuwa watakapohitimu watarejea katika vituo vyao vya kazi wakiwa na ujuzi na elimu itakayowawezesha kutekeleza majukumu kikamilifu.

Ndejembi aliomgeza kuwa serikali inaajiri watumishi kulingana na bajeti iliyopangwa katika mwaka wa fedha husika na kwamba bajeti hiyo inaweza kushindwa kuajiri watumishi kulingana na uhitaji, hivyo waajiri wanayo nafasi ya kuisaidia serikali kutatua changamoto hiyo.

Naibu Waziri pia aliwataka waajiri kutowakaimisha nafasi watumishi wasio na sifa na utaalamu wa kazi katika kada wanazotakiwa kuzisimamia na kuongeza kuwa ni muhimu kwa watumishi wanaokaimishwa kuwa na sifa na uwezo.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni, Erasto Kiwale, alimshukuru Ndejembi kwa kufanya ziara ya kikazi katika halmashauri hiyo na kuhimiza uwajibikaji, kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kiutumishi, kutatua kero na changamoto zilizokuwa zikiwakabili watumishi wa halmashauri yake.

Naibu Waziri Ndejembi anaendelea na ziara ya kikazi mkoa wa Dar es Salaam yenye lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma na kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kuzinusuru Kaya Maskini unaoratibiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

# RC aagiza ukamilishaji matumizi dampo la Manga

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameiagiza Halmashauri ya Manispaa ya Singida kuharakisha utekelezaji wa kulibadilisha matumizi dampo la Manga lililoko kijiji cha Mtipa kandokando ya barabara kuu ya Singida-Mwanza, kuwa eneo la maegesho ya malori na kujenga hoteli na baa.

Akizungumza jana baada ya kutembelea dampo hilo, alisema eneo yatakapojengwa maegesho, hoteli, baa na vituo vya mafuta kitakuwa chanzo kizuri cha mapato ya Manispaa ya Singida kwa kuwa magari yatatoa ushuru na watu watakaowekeza hapo watatoa kodi.

Serukamba aliagiza wilaya zote kuanza mkakati wa kupanda miti kandokando ya barabara na kufanya usafi kila siku ya Jumamosi kuanzia mwakani ili kutunza mazingira na kupendezesha miji.

Naye Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu, alisema maelekezo ya Mkuu wa Mkoa wa Singida yatazingatiwa na manispaa ilikuwa imeshaanza kubadilisha matumizi ya dampo hilo.

Alisema wakati linaanzishwa mji wa Singida ulikuwa haujapanuka, hivyo limetafutwa eneo la Mwankonko nje kidogo ya mji ambalo limeanza kutumika dampo jipya.

"Mpango wa manispaa eneo lote la dampo la Manga litapimwa kujua ukubwa wake na baadaye itapitishwa michoro inayokidhi eneo hilo na baada ya hapo tutajenga hoteli, nyumba za kulala wageni, maegesho ya magari, baa na eneo la mama lishe ili wanaoegesha magari yao waweze kupata huduma," alisema.

Kiaratu alisema Manispaa ya Singida itashughulika na suala la ujenzi wa maegesho ya magari, lakini huduma nyingine zitafanywa na wawekezaji watakaopewa eneo hilo kuwekeza.

Alisema sheria ndogo za manispaa zilizoko zitahuishwa zianze kutumika haraka na atakayepatikana akitupa taka ovyo atakamatwa na kutozwa faini kati ya Sh. 50,000 hadi 300,000.

Meya alisema manispaa itaanza kuvitumia vikundi kazi vilivyo kila mtaa kwa ajili kukamata watu wanaochafua mazingira ili wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.



Mbunge wa Jimbo la Ilala ambaye ni Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri wa Tanzania, Mussa Azan Zungu (katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa vyoo vya Shule ya Sekondari ya Dar es Salaam ambavyo vimekarabatiwa na Benki ya BancABC Tanzania kwa Sh. milioni 18. (Wa tatu kushoto) ni Mkurugenzi Mtendaji wa BancABC, Imani John, (wa pili kulia) ni Diwani wa Kata ya Gerezani, Fatuma Abubakari na (kushoto) ni Katibu wa CCM Kata ya Gerezani, Blandina Sinah. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ABC yatumia mil.18/ kukarabati vyoo sekondari

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya BancABC Tanzania imefanya ukarabati wa vyoo katika Shule ya Sekondari ya Dar es Salaam, ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu katika mazingira bora na rafiki.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam wakati wa kukabidhi vyoo hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Imani John, alisema ukarabati huo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 18, utawafaidisha wanafunzi 600 wa shule hiyo.

Alisema ukarabati wa vyoo hivyo utawawezesha wanafunzi wa shule hiyo iliyopo jijini la Dar es Salaam Wilaya ya Ilala kupata elimu bora kwa maisha yao ya baadaye.

John alisema ukarabati huo ni mwendelezo wa kuunga mkono juhudi za serikali kutoa huduma bora za kijamii na kuboresha maendeleo ya elimu kwa Watanzania.

"Hii siyo mara ya kwanza kwa BancABC Tanzania kushiriki katika shughuli za kijamii kama hizi, sisi kama taasisi ya kifedha tunatambua ya kuwa tuna mchango mkubwa katika kusaidia jamii yetu inayotuzunguka, hivyo tumekuwa tukijikita katika matukio mbalimbali ya kijamii ili kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali," alisema.

Aliongeza kuwa BancABC iliona ni vyema kuboresha sekta ya elimu nchini kupitia ukarabati wa vyoo vya shule hiyo, wanaamini ili mtoto aweze kujifunza vyema lazima apate mazingira rafiki yanayomzunguka.

Alisema wamefanya maboresho ya vyoo 27 pamoja na ukarabati wa mfumo wa majitaka.

"Benki ya BancABC kama taasisi ya fedha tunafanya juhudi za kusogeza huduma za kifedha ili kuwafikia Watanzania wengi kupitia mawakala zaidi ya 700 tulionao nchi nzima na satellite zaidi ya 100 katika wilaya mbalimbali nchini.

"Tunazo akaunti za kuwainua wajasiriamali wadogo kwa kuwapatia mikopo ya biashara, pia tuna huduma ya mikopo tunayoitoa kwa wafanyakazi wa serikalini kupitia satellite zetu nchi nzima. Mikopo yetu ina riba nafuu na inapatikana ndani ya muda mfupi sana," alisema John.

Mbunge wa Jimbo la Ilala ambaye ni Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azan Zungu, alisema msaada wa kukabarati vyoo hivyo umedhihirisha uhusiano mzuri uliopo kati ya serikali na sekta binafsi.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Salaam Mwalaba, alisema mchango huo umekuja wakati mwafaka kwa sababu ya wingi wa wanafunzi darasani, vyoo hivyo vitakuwa msaada mkubwa sana kwa wanafunzi.

## Madarasa 10 kupunguza mrundikano

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

UJENZI wa madarasa 10 ya sekondari yenye thamani ya Sh. milioni 200 wilayani Ludewa, utapunguza mrundikano wa wanafunzi darasani.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Wise Mgina, aliiambia Nipashe.

"Kimsingi madarasa yote na madawati yamekamilika yamekuja wakati sahihi ili kusaidia tatizo la mrundikano kwa wanafunzi, kila darasa linatarajiwa kubeba wanafunzi 40 maana yake tayari tutatatua tatizo la watoto 400 sio suala dogo ni msaada mkubwa," alisema Mgina.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Mkufwe, alisema kwa upande wake wamekamilisha madarasa 12 yenye thamani ya Sh. milioni 240 tangu Novemba 28.

"Sisi tumepewa madarasa 12 tumeshakamilisha toka tarehe 28 mwezi wa 11, wanafunzi madarasa yao yako tayari tunawasubiri wao tu muda ukifika," alisema Makufwe.

Ofisa Mipango Halmashauri ya Mji Makambako, Emmanuel Steven, alisema walipata madarasa 21 ya sekondari yenye thamani ya Sh. milioni 420 na wanafunzi wanatakiwa kujiandaa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Erasto Mpete, alisema walipokea Sh. milioni 520 kwa ajili ya madarasa 26 na tayari yamekamilika.

"Madarasa haya ni kivutio kwa watoto kusoma kwenye madarasa mazuri na ya kisasa kwa hiyo tunamshukuru rais kwa kuwa ametia chachu ya kuongeza ufaulu," alisema Mpete. Alitoa wito kwa wananchi kutambua na kuona mchango wa serikali wa kuboresha masuala ya elimu.

"Wazazi sasa wapeleke watoto shule kwa sababu urithi namba moja ni elimu sasa kama serikali inatoa mchango mkubwa wa kujenga madarasa halafu wewe hupeleki mtoto shule hiyo ni shida," alisisitiza.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Lauter Kanoni, alisema ujenzi wa madarasa 14 ya sekondari yenye thamani za zaidi ya Sh. milioni 200 tayari yamekamilika pamoja na madawati.

Nao wananchi wa mjini Njombe wamesema ujenzi wa madarasa hayo umewasaidia kuondokana na michango ya mara kwa mara pamoja na kupunguza utoro.

"Tulikuwa na utaratibu wa kuchangishana wenyewe kwa wenyewe ili kuanza majengo ndipo serikali kuu ituunge mkono, lakini sasa hivi tunamshuru Rais Samia kwa kuleta hela hizi zimekua msaada mkubwa pia tuna uhakika sasa watoto wetu watakwenda sekondari bila tatizo," alisema Mary Mwalongo, mkazi wa Njombe mjini.

Samwel Mgaya alisema hapo awali wanafunzi walikuwa wakisoma kwa mrundikano na kusababisha utoro, madarasa hayo yataondoa tatizo hilo.



# Bil. 271/- kupandisha elimu jumuishi nchini

**Na Mwandishi Wetu**

SHILINGI bilioni 271 zilizotokana na ufadhili wa Mfuko wa Serikali ya Uingereza ukihusisha mradi wa ujenzi wa shule bora umelenga kuiunga mkono serikali kupandisha kiwango cha elimu jumuishi nchini.

Mradi huo pia, umelenga kuweka mazingira salama ya kujifunzia kwa wanafunzi wa kike na wa kiume kuanzia shule za awali, msingi na sekondari nchini.

Mratibu wa mradi wa shule bora, Mkoa wa Tanga, Thomas Aikaruwa, aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo ya siku moja ya mradi huo kwa waandishi wa habari.

Alisema mradi utahakikisha kuwa elimu jumuishi inaboreshwa na itatolewa kwa watoto wote.

"Kwa ushirikiano wa serikali yetu, mradi huu utafanya maboresho yatakayowezesha kila mtoto kupata msingi mzuri katika elimu ya awali, ili kutoa fursa na mchango katika ukuaji wa nchi na maendeleo kwa ujumla wake," alisema. Aidha, alisema watafanya kazi katika mikoa tisa ukiwamo wa Dodoma, Katavi, Kigoma, Mara, Pwani, Rukwa, Simiyu, Singida na Tanga na makao makuu yatakuwa Dodoma. "Mradi unalenga katika maeneo manne ambayo ni kujifunza kwa watoto wote shuleni, kujifunza na ufadhili huu, ni kwa hisani ya Mfuko wa Serikali ya Uingereza na utasaidia kuimarisha kazi ya ufundishaji.

"Utajenga mfumo imara, utaunga mkono juhudi za serikali katika kuimarisha na kupata thamani ya fedha katika utoaji wa elimu katika ngazi zote kuanzia chini hadi taifa," alisema.

Kipaumbele cha mradi huo ni wanafunzi wenye mahitaji maalumu na wanaotoka katika mazingira magumu ili kuwawezesha kuwa shuleni na kujifunza katika mazingira bora na salama hadi kufikia elimu ya sekondari.

"Pamoja na kuwashirikisha wazazi na jumuiya kuboresha usalama wa shule na kuondoa migogoro, tutahakikisha walimu wanazungumzia mambo ya jinsia na upatikanaji wa mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

"Pia kutayarisha mazingira salama na kuwaunga mkono wasichana kushiriki na kujadili mambo yanayowahusu, na kuwasaidia kipindi wakiwa kwenye hedhi," alisema.

Mwenyekiti Msaidizi wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Tanga, Burhani Yakubu, alishukuru kwa waandaaji wa mafunzo hayo ambayo yataleta tija kwa waandishi katika kutekeleza majukumu yao kwa umma.

"Tatizo ni kwamba wananchi wengi wanaona shule haziwahusu ni ya mwalimu na mwenyekiti wa kijiji na hii inatokana na kukosekana kwa uwazi na ushirikishwaji, unaweza kukuta hata hizo fedha zinazoletwa kutoka serikalini hawapati taarifa na ndio maana wanaona hakuna umuhimu wa kuchangia hata chakula shuleni," alisema.

Mafunzo hayo yalitolewa kwa waandishi wa habari 30 na maofisa habari wa halmashauri za wilaya tisa na ofisa habari wa mkoa huo.

## Shirika kuwafuta machozi wanafunzi familia maskini

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SHIRIKA la Uweza Foundation limeahidi kuwafuta machozi kwa kuwashika mkono wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wanaotoka kwenye familia zenye mazingira magumu mkoani Kilimanjaro, kujiajiri katika sekta ya ujasiriamali na programu za uanagenzi.

Aidha, limesema kuwa hivi sasa liko katika mchakato wa kutafuta fedha za ruzuku kwa ajili ya ufadhili wa bima ya afya, kwa watoto wanaotoka mazingira hayo.

Jana Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Esther Simba maarufu 'Hekima' alitangaza neema hiyo, wakati wa hafla ya kukabidhi taulo za kike (sodo) kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, wanaolelewa Kituo cha Tuleeni Ophance Home kilichoko Kata ya Uru Kaskazini, Moshi Vijijini.

"Ninyi ni mashahidi kwamba wasichana wengi, hasa walioko vijijini na maeneo ya pembezoni, wazazi wao wana uwezo mdogo kiuchumi na wasichana wadogo kama hawa hupata mtihani mkubwa wanapokuwa hedhi.

"Sasa mara nyingi wanakosa taulo za kike za kuwasaidia wakiwa katika mazingira hayo na kujikuta wakitumia matambara wakati mwingine. Kwa kuwa jambo hili linahitaji uwekezaji wa fedha, kama shirika tumewasaidia kwa kuanza na wanafunzi 20.

Zaidi aliongeza: "Kwa kufanya hivyo tuna hakika kwamba wanafunzi wataweza kwenda shuleni bila kukosa masomo kutokana na hali yao ya jinsia."

Pia alieleza kuhusu mpango wao wa ufadhili wa bima ya afya akisema: "Kilichoko jikoni ambacho hivi sasa kinapikwa ni jinsi gani ambavyo tunaweza kupata bima ya afya kwa ajili ya kuwasaidia hawa watoto wanaolelewa na Kituo cha Tuleeni. Hatujui ni lini litakamilika lakini litakapokuwa limekamilika tutakuja tena kwenu."

Kabla ya makabidhiano ya taulo hizo, mwazilishi wa kituo cha Tuleeni Ophafance Home, Flavia Faraji, alieleza kuwa kituo chake kinahudumia watoto 86, kwamba kati ya hao watoto wanaolala kituoni hapo ni 53.

"Tunapokea watoto wanaoanzia miaka miwili mpaka miaka 17 na pengine zaidi kwa wale ambao tunaendelea kuwasaidia kielimu. Wakati wa likizo, watoto wanaolelewa na kituo hiki huwa tunawaunganisha na familia zao, na kuna wale ambao hawawezi kwenda nyumbani kutokana na sababu zilizosababisha wakaletwa kwetu, ambazo hizo hali pamoja na vitendo vya ukatili wa kijinsia waliofanyiwa.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Moshi, Habiba Bhou, alisema ili kuwa na kujenga kizazi cha uwajibikaji katika jamii hapo baadaye ni lazima wadau wa maendeleo kama UWEZA Foundation, wajikite pia kutoa elimu ya hedhi salama kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Takwimu zinaonyesha kuwa wanafunzi wa kike walio katika mazingira hayo hukosa masomo kwa muda wa siku tano hadi saba kila mwezi, sawa na siku 60 hadi 70 kwa mwaka kutokana na kukosa taulo za kike kwa ajili ya kujisitiri wakati wa hedhi.




Mkurugenzi wa Shirika la AKO Tanzania Community Support, Hilda Kimath (kushoto), akizungumza baada ya kukabidhi vyoo vya kisasa kwa thamani ya Sh. milioni 68 katika Shule ya Msingi Kambi ya Chokaa Kata ya Naisinyai wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali kuanza kuwapika wasanifu madini ya vito wazawa

**Novatus Makunga,** ARUSHA

WIZARA ya Madini imetangaza mkakati mpya wa kuanza kuzalisha wataalamu vijana wenye uwezo wa kusanifu madini ya vito, ili kupunguza idadi kubwa ya wageni wanaoajiriwa kwa fani hiyo nchini.

Jana Kamishna Msaidizi wa Madini, anayeshughulikia uongezaji thamani ya madini wa wizara hiyo, Bather Luzabiko, alisema uamuzi huo unatokana na kukosekana kwa wataalamu wa kutosha ambao ni wazawa.

Alisema tayari Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC), kilichoko chini ya Wizara ya Madini, kimeongezewa uwezo wa kutoa mafunzo ya ukataji na ung'arishaji madini ya vito yanayopatikana nchini ili kuongeza thamani madini.

"Thamani ya madini ya vito, huongezeka zaidi pale yanapokuwa na uwezo wa kupitisha mwanga, umbo linalovutia na rangi yenye kung'aa yanapoingia sokoni. Ndiyo maana tumeamua kuja na mkakati huu, ambao umechukuliwa ili kuinua uchumi, kuongeza soko na kuwezesha vijana kujiajiri," alisema Kamishna Luzabiko.

Inaelezwa kuwa wataalamu wengi wanaokuja nchini kwa ajili ya ukataji, ung'arishaji na usanifu wa madini, wanatoka nchi zenye wabobezi zaidi kama Sri- Lanka na Thailand.


Sheria ya Madini Namba 14 ya Mwaka 2010, pamoja na mambo mengine inaelekeza kuwa madini yote yanayopatikana nchini ni lazima yasanifiwe kabla ya kusafirishwa na kuuzwa nje ya nchi.

Vilevile inaelezwa kuwa hivi sasa kwa nchi zima, kuna mashine za kukata na kusanifu madini zisizozidi 300, ambazo kwa wastani zina uwezo wa kusanifu madini yasiyozidi kilogramu moja kwa siku.

Alipotafutwa kutoa maoni yake kuhusu mkakati huo, mwanafunzi wa usanifu wa madini ya vito anayesoma katika Kituo cha TGC jijini Arusha, Jackline Joseph, alisema madini kama rubi na sapphire, yanahitaji utaalamu wa hali ya juu na mashine za kipekee hasa katika uchomaji.

"Uchomaji wake unahitaji nyuzi joto zaidi ya 1,000 na umeme wa uhakika kwani kitendo chochote cha kukosea ni moja kwa moja kwa moja unaingia katika hasara kwa madini kuharibika na kutokuuzika,"alisema.

Madini ya vito yanayopatikana zaidi Tanzania ni tanzanite, almasi, rubi, sapphire, emarald, tourmaline, aguamarine, zircon, garnet, arnethyst, rhodolite, alexandrite mapambo ya nyumbani, aina ya mawe yenye rangi na nikeli.





# Waziri atangaza kibano halmashauri wezi fedha

**Na Cynthia Mwilolezi,**

ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amesema kibano dhidi ya halmashauri zilizochepusha fedha za miradi ya uboreshaji wa elimu ya awali na msingi kinanukia

Aidha, ameagiza sekretarieti za mikoa na wilaya, kuhakikisha zinasimamia kwa ufanisi, utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa elimu ya awali na msingi ili kufikia malengo ya serikali ya kutatua tatizo la elimu nchini.

Aliyasema hayo alipokuwa akifunga kikao kazi cha kuwajengea uwezo makatibu tawala wa mkoa, maofisa elimu wa mkoa na wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa, kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Boost.

"Zingatieni sheria, kanuni na miongozo katika utekelezaji wa mradi huu, ili thamani ya fedha iliyotolewa iendane na majengo yatakayojengwa na mjitahidi sana kuepuka hoja za ukaguzi,"alisema.

Pia alionya tabia ya baadhi ya halmashauri kubadilisha maeneo ya ujenzi au kukarabati shule kwa kuwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI, ilishafanya tathmini na kugundua kuwa zipo shule ambazo zinahitaji ukarabati wa miundombinu kutokana na uchakavu.

"Hivyo maamuzi ya serikali yamezingatia viashiria vya msongamano wa wanafunzi, vijiji vyenye ukosefu wa shule za msingi na maeneo ambayo wanafunzi wanatembea umbali mrefu," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2022/2023, serikali imepanga kutoa Sh. bilioni 240 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo ya ujenzi na uboreshaji wa shule.

Kutokana na umuhimu huo, alisema ni vyema viongozi hao wakajikita kuimarisha ushirikiano na taasisi na idara mbalimbali katika utekelezaji wa baadhi ya afua za mradi wa Boost ili kufanikisha malengo ya mradi yaliyowekwa.

# Kilio cha wanafunzi kulala madarasani chafika kwa RC

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

KILIO cha wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita wa Shule ya Sekondari Hai, kutumia vyumba vya madarasa kwa ajili ya kulala kutokana na upungufu wa mabweni, kimetua kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Edmund Rutaraka, aliwasilisha ombi maalum la kuomba Mkoa wa Kilimanjaro uongeze nguvu ya fedha, kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili ya kidato cha tano na cha sita.

Rutaraka jana alimuomba Babu kuwapiga jeki ili kumaliza tatizo hilo wakati alipokwenda kwenye ukaguzi na makabidhiano ya vyumba 10 vya madarasa vilivyojengwa kwa gharama ya Sh. milioni 200.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa baada ya kukamilika ujenzi huu tatizo kubwa sasa ni mabweni na uzio hakuna.

Tuna wanafunzi takribani 30 na kuna mabweni mawili ya kidato cha tano na sita.

"Wengine wanalazimika kulala kwenye madarasa. Tunakuomba ulisukume mbele ili kumaliza adha hii ya wanafunzi kulala darasani. Lakini shule hii haina uzio, tusaidie kupata fedha ili wanafunzi wapate masomo bila usumbufu," alisema.

Kabla ya ombi hilo kuwasilishwa kwa Babu, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Juma Irando, alimwahidi Mkuu huyo wa Mkoa, kwamba wako makini na wataendelea kusimamia miradi yote na fedha zinazopelekwa na serikali kuu ili miradi iendane na thamani ya fedha.

Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Sekondari ya Wilaya hiyo, Julius Mduma, alisema vyumba 10 vya madarasa katika shule mbalimbali za sekondari vimekamilika na viko tayari kwa matumizi ifikapo Januari mwakani.

Akijibu ombi hilo, Babu, alisema ameliona tatizo kwa macho yake mwenyewe na atalifanyia kazi haraka iwezekanavyo, kwa kuhakikisha fedha zinapatikana za ujenzi huo wa mabweni pamoja na uzio.

"Tumepokea Sh. bilioni 2.5, kwa maana ya kujenga madarasa 125 kwa Mkoa wa Kilimanjaro. Fedha hizi tumeletewa na Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye anahangaika kuhakikisha kwamba Watanzania na watoto wao wanapata elimu bora.

Alisema: "Fedha hizi siyo za kufanyia mchezo, na siyo fedha za kupanga matumizi mengine. Ni kwa ajili ya madarasa yaliyokamilika kama yalivyokuwa yameelekezwa na TAMISEMI (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)."



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la UWEZA Foundation, Mwalimu Esther Simba (katikati), akizungumza jana na wasichana wanaotoka katika mazingira magumu, kuhusu matumizi ya taulo za kike na hedhi salama. Wasichana hao wanalelewa na Kituo cha Tuleeni Ophance Home kilichoko Uru Kaskazini, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Hospitali ya Mawenzi kuwafikia wanaougua kisukari, presha

**Na Mary Mosha**, MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi, imepanga kuwafikia watu 2,500 ndani ya saa 72, wanaosumbuliwa na magonjwa yasiyoambukiza ya shikizo la damu na sukari.

Hadi kufikia jana tayari wataalamu wa hospitali hiyo walikuwa wamewafikia na kuwafanyia uchunguzi wa afya watu 800.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Mawenzi, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mawenzi, Dk. Edna Munisi, alisema uamuzi huo wa kutoa elimu na uchunguzi wa afya, unalenga kupunguza ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza, ambayo yamekuwa yakihatarisha afya na uchumi wa jamii.

"Katika Wiki ya Mawenzi iliyoanza Desemba 12 na kufikia kilele chake Desemba 16 mwaka huu, tutatoa huduma za uchunguzi wa afya kwa wananchi bure kwa siku tatu.

"Kwa haya magonjwa yasiyo ya kuambukiza, ili yasiendelee kuongezeka wananchi wanapaswa watumie vyakula vya asili na kufanya mazoezi na usipofanya hivyo utajikuta umepata magonjwa hayo na kuanza kutumia fedha nyingi kujitibu,"alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Meno wa Hospitali hiyo, Dk. Thomas Mushi, alisema bado wakazi wengi wa Mkoa wa Kilimanjaro, hawana elimu ya kutosha kuhusu afya ya kinywa na meno.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa kati ya wagonjwa 100 wanaofikishwa hospitali kwa ajili ya kupatiwa huduma mbalimbali za afya, 30 kati yao wana meno yaliyotoboka.

Akifungua maadhimisho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema kutokana na umuhimu wa wiki hiyo, iko haja ya hospitali hiyo kuona umuhimu wa kutoa huduma hiyo mara mbili kwa mwaka badala ya ilivyo.

ama

ALHAMISI DESEMBA 15, 2022

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 15

## DARASA LA MABOSI NEMC; Ndivyo ilivyo dhana ardhioevu, unyeti wake na inakopitia kitaifa



## CT SCAN YA KWANZA MKOANI... Waziri Mkuu: Hospitali Rufani ianze Januari Mosi, Ieteni umeme haraka!

Ukurasa 16

# Wataalamu moyo waja na kampeni maalum magonjwa yasiyoambukiza

**Na Pilly Kigome**

IMEZOELEKA tabia ya kuwapo makundi ya mitaani na kuzunguka maeneo mengi mijini na vijijini, wake kwa waume wanaodhani wanajifurahisha nafsi au wengine kudhani wanahitaji kupungua ukubwa au uzito wa mwili.

Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), iliyopo Muhimbili jijini Dar es Salaam, imebuni na kuendesha kampeni ya kurekebisha dhana hiyo, ikizundua harakati maalum ya kukimbia kupita mitaa baadhi, lengo ni kuhamasisha jamii ifanye mazoezi na kuepukana na maradhi ya moyo, kisukari na mengine yasiyoambukiza, wakilinda afya.

Zama zilizopita kukadiria miaka 30 sasa au zaidi, ilizoeleka kwamba magonjwa ya shinikizo la damu, kisukari na unene uliokithiri wanapata watu wenye uchumi bora na wenye umri mkubwa katika jamii nchini.

Kadri muda unavyosonga na mifumo ya maisha inavyozidi kubadilika, magonjwa hayo yanazidi kuonekana kwa jamii yote, pasipo kujali umri na ngazi ya kifedha kila kukicha, yakiwa na sura ya hatari.

Nipashe imeshuhudia madaktari wa ngazi mbalimbali, wauguzi wa madaraja na wafanyakazi wa kada ya afya, kwa pamoja wakikimbia kuanzia kutoka katika viwanja hivyo vya Muhimbili na kukimbia mitaa mbalimbali ya Dar es Salaam, umbali wa kilomita tano, lengo ni kuweka sawa afya zao na kuhamasisha jamii iige mfano huo wa kuimarisha afya.



Madaktari na wataalamu wa afya katika jamii ya hospitalini Muhimbili, jijini Dar es Salaam, waliojumuika katika mazoezi ya pamoja kujenga afya. **PICHA: PILLY KIGOME.**

Naibu Spika wa Bunge nchini, Mussa Zungu, akiwa mstari wa mbele akiongoza madaktari na wafanyakazi wa hospitalini Muhimbili wakikimbia katika kampeni hiyo maalum iliyozinduliwa na taasisi hiyo ya Jakaya Kikwete.

Zungu anasema, magonjwa hayo yasiyoambukiza kwa sasa yanakua kwa kasi ndani ya jamii, yakiongezeka kwa asilimia 40, kutokana na ulaji holela wa vyakula, uvutaji sigara (na tumbaku) na kuendekeza pombe.

Watanzania hutakiwa kutambua ulaji wa kienyeji, usio na mpangilio na matumizi makubwa ya vyakula vya kemikali, kunywa pombe kulikozidi, kipimo kinaleta madhara makubwa kiafya na kwa kiasi kikubwa.

"Tunapozungumzia ulaji mbaya unaenda sambamba na ulaji hovyo kusipokuwa na mpangilio maalum wa makundi ya vyakula stahili na mpangilio wa masaa kinyume na utaratibu," anasema.

Pia, anataja wanaokula sana vyakula vya mafuta, ambavyo ndivyo vyenye thamani kubwa, vinafanana na hadhi za kifahari na wanaacha kula vyakula vya kawaida kama michemsho, wakiwa katika mitazamo wataonekana masikini, kumbe hilo linawaumiza kiafya.

Vyakula vyenye uwezekano wa kuepusha magonjwa mwilini hutajwa ni vya gharama nafuu na vina ufanisi mkubwa mwilini, zikiwemo mboga, vyakula vya kuchemsha jamii ya mizizi na hata matunda makundi yanayoleta tija katika ufanisi na kutenda kazi mwili.

Hapo anawakumbusha Watanzania kutambua kufanya mazoezi, kwamba ni muhimu katika maisha yao ya kila siku, kwa kuwa kunaepusha magonjwa ya moyo na yasiyoambukiza kwa kiasi kikubwa sana.

Ni magonjwa yasiyoambukiza na yanazuilika, hasa watu wakijikita kufuata kanuni za afya na maelekezo kutoka kwa wataalamu wa afya nchini kote, ikiwemo kujitahidi kubadilisha mfumo wa maisha. Inatajwa ni chanzo kimojawapo cha kuyafuta magonjwa yasiyoambukiza.

**BOSI JKCI**

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, anabainisha magonjwa yasiyoambukiza yakiwemo ya moyo, yamekuwa yanasababisha vifo vya watu wengi duniani na takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuwa watu milioni 17.3 duniani kote, ikiwemo Tanzania, wanapoteza maisha kila mwaka kutokana na magonjwa ya moyo.

Utafiti uliofanyika nchini mwaka 2012 kuhusu mambo hatarishi yasiyo ya kuambukiza, ulionyesha kati ya watu wazima asilimia 15.9 walikuwa wanatumia tumbaku au sigara, asilimia 26 walikuwa na viwango vya juu vya lehemu yaani mafuta yaliyozidi mwilini.

Pia, Dk. Kisenge anataja asilimia 97.2 walikuwa hawatumii mboga angalau siku tano kwa wiki, chini ya asilimia tano walikuwa wanakula matunda angalau siku tano kwa wiki.

Dk. Kisenge anasema asilimia 29.3 walikuwa wanakunywa pombe na asilimia 26 walikuwa na uzito uliozidi, huku kiwango cha ongezeko la wagonjwa wa kisukari kilikuwa asilimia 9.1, shinikizo la damu asilimia 25.9.

Taasisi hiyo ya moyo, sasa imeamua kukabili hayo kwa kampeni maalumu ya kuihamasisha jamii kushiriki mazoezi, kwamba kutawawezesha kuondokana na magonjwa hayo yasiyoambukiza na waone mazoezi, ikiwa sehemu ya maisha yao.

Kiafya, inaelezwa kwamba kufanya mazoezi mtu akitoa jasho ndiyo anaondoa sumu mwilini na magonjwa mengine nyemelezi hayamsogelei. Hapo, inaendana na ushauri wa kitaalamu kila mtu atenge muda walau dakika 10 za mazoezi ili atoe jasho na kama muda si rafiki atembee umbali mrefu kidogo.

AFYA

SHIDA AINA YAKE...

# Inapogeuka mtindo, vichanga wafiwa na mama wanatelekezwa penye vituo malezi

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

TATIZO la wazazi na walezi kutelekeza watoto wao katika ngazi ya familia na katika vituo vya kulea watoto linaendelea kushika kasi katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Kagera.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Idara ya Ustawi wa Jamii mkoani humo, katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba 2022, watoto 271 wameripotiwa kutelekezwa.

Sista Penina Kaimukirwa ni Mkuu wa Kituo cha Ntoma, kinachomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, anasema wapo baadhi ya wazazi na walezi wanaowatelekezea watoto na hawapatikani wanapofuatiliwa.



Baadhi ya watoto wanaolelewa katika Kituo cha Kulea Watoto, wakiwa wamebebwa na wasaidizi wao.

"Watoto tulio nao katika kituo hiki ni wale ambao mama zao hufariki muda mfupi baada ya kujifungua. Hawa huletwa na baba zao au walezi wengine, pia tunao wanaotelekezwa na mama zao baada ya kuzaliwa, hawa huokotwa na wasamaria wema na kuletwa kituoni kwa ajili ya kupata malezi," anasema.

Sista Penina, anasimulia kwamba wazazi na walezi wanaopeleka watoto katika kituo hicho, hukubaliana kimaandishi kipindi gani watapaswa kuwachukua, lakini baadhi wanakaidi makubaliano.

Mkuu wa kituo hicho anasema, huwa wanapokea watoto wenye umri wa kuzaliwa hadi miaka miwili, mtoto anapozidi umri anachukuliwa na wazazi au walezi wake akalelewe na familia au kupelekwa vituo vinavyolea watoto wakubwa zaidi ya hapo.

Katika lugha ya kulalamika, anasema wazazi na walezi wengi wakiondoka, hawarudi hata kuwasalimia watoto. Hapo Sista Penina anaeleza: "Wazazi wengine wanawakwepa, lakini wakati wa kuwaleta huja kwa kunyenyekea wakipiga magoti na kubembeleza, ili watoto wao wapokelewe."

Analalamika kuwa wazazi na walezi wanawakatisha tamaa katika hatua yao hiyo kujitoa kwenye kituo hicho chenye watoto 33 hivi sasa, akiwataka watu waache tabia hiyo wabadilike akihimiza kuna wakati wanalazimika kushirikiana na Idara ya Ustawi wa Jamii na Jeshi la Polisi, kwenda kuwatafuta watelekezaji hao.

"Wengine wanaandikisha taarifa za uongo, tukienda tukafika huko tunaambiwa huyo mtu hawamfahamu. Wengine utakuta wanafahamika, lakini tunaambiwa walikwishahama muda mrefu, hawajui walipo au wengine tunaambiwa walihamia visiwani, tunashindwa kuwapata," anafafanua.

Anasema, kutokana na miundombinu ya kituo hicho chenye watoto 33 sasa kutoruhusu kuendelea kuishi na watoto waliozidi miaka miwili, huwa wanashirikiana na Idara ya Ustawi wa Jamii inayowatafutia nafasi katika vituo vya kulelea watoto wakubwa.

### KITUONI NGARA

Mhudumu wa Watoto katika Kituo cha Nyumba ya Malaika kilichoko wilayani Ngara, mkoani Kagera, Sista Mariagoreth Felix, anasema tatizo la wazazi na walezi kutelekeza watoto, nalo limekikumba kituo chake, akitoa rai kuachwa tabia hiyo inayoathiri watoto kisaikolojia.

Sista Felix mwenye kituo chenye watoto 35, anasema wapo watoto wachanga waliopatikana kwa kuokotwa baada ya kutelekezwa mitaani, pia wana watoto waliopelekwa na wazazi au walezi na wakawatelekeza kituoni.

"Baadhi ya wazazi hawana uchungu na watoto, wamekosa ubinadamu na hata hawana hofu ya Mungu. Hapa kituoni kuna fomu wakiwaleta watoto zinajazwa, zikionyesha mhusika wapi ametokea, lakini tunapoona hawaji tukaenda kuwafuatilia vijijini, tunaambiwa huyo mtu alikwishahama siku nyingi," anafahamisha.

Mlezi huyo anatoa mfano wa watoto pacha wawili waliopelekwa kituoni hapo na baba yao mzazi kutoka eneo la Nyamigeli wilayani Ngara, wakiwa na siku moja ya kuzaliwa, sasa wana takribani miaka minne, baba yao hajarudi, walau kuwatembelea.

### HALI INAYOTAWALA

Ofisa Ustawi wa Jamii mkoa wa Kagera, Rebeca Gwambassa, anasema suala la wazazi au walezi kutelekeza watoto, ni sehemu ya ukatili na kwamba katika kipindi kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu, watoto 271 wameripotiwa kutelekezwa.

Gwambasa anasema, katika kipindi hicho watoto 1,414 walifanyiwa ukatili, ukiwamo 84 waliofanyiwa ukatili wa kingono, 859 waliofanyiwa ukatili wa kihisia au kisaikolojia na 208 wa kimwili.

"Vitendo vya ukatili kwa watoto vinaendelea kuongezeka katika jamii, mfano kumekuwepo utelekezaji wa watoto kwenye ngazi ya familia, pia kwenye vituo vya kulea watoto ambavyo sisi hupenda kuviita makao ya watoto" anasema.

Rebecca ana maoni kwamba, malezi ya kitaasisi ni uamuzi wa mwisho, akiwa na ufafanuzi: "Tunapenda alelewe kwenye familia, hata kama hatalelewa na baba au mama, kuna ndugu wengine walioko kwenye hiyo familia ni bora wamlee. Hii inasaidia mtoto kujifunza mila na desturi za familia au jamii husika."

Anaeleza kuwa, mtoto anapokosa kumfahamu baba yake, pia wanafamilia wengine, huathirika katika makuzi yake kisaikolojia, kwani huwa wanahoji na hatimaye huwa inawaathiri kisaikolojia.

"Tena akisikia alipelekwa na mzazi au mlezi na kupata taarifa kuwa wako hai na walimtelekeza huko, athari inakuwa zaidi kwake," anaeleza na kuendelea: "Pia, anaweza kujifunza vitu vingi vibaya kutokana na kulelewa nje ya familia."

Anasema ama wazazi au walezi wanaotelekeza watoto kwa makusudi, hatua za awali zinazochukuliwa kisheria ni kutumia polisi kuwasaka, ambako kunakuwapo ugumu wa kuwapata.

"Wazazi na walezi wanaofanya hivyo wafahamu kwamba kuna Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009, Kifungu cha Nane, Kifungu Kidogo cha Kwanza A mpaka G kinaeleza mzazi au mlezi anapaswa kumlea mtoto wake na kumpa huduma zote ikiwamo chakula, mavazi, malazi na malezi. Hivyo, wafahamu kuwa wanaweza kukamatwa, kupelekwa mahakamani na kupewa adhabu," anasema.

### PICHA YA JINAI

Taarifa kutoka Ofisi ya Waendesha Mashitaka Mkoa Kagera, inaeleza kesi za ukatili kwa watoto zilizoko mahakamani hadi kufikia Oktoba 15, 2022 ni 93. Mwaka 2018 ina kesi moja; mwaka 2020 iko 1 na mwaka huu una jumla ya kesi 91 hadi mwezi uliopita.

Katika kesi hizo zilizoko katika hatua mbalimbali katika mahakama za wilaya za Bukoba, Muleba, Ngara, Biharamulo na Karagwe, kesi 75 ni za kubaka; mbili kulawiti; shambulio la aibu mbili; kujeruhi nane; kuzini na maharim (baba kuzini na mwanae wa kuzaa) mbili; kujaribu kubaka kesi moja; na shambulio la kudhuru mwili tatu.

Kwa mujibu wa Takwimu za Jeshi la Polisi Tanzania, katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2021, kuna matukio 11,499 ya ukatili dhidi ya watoto yalitolewa taarifa katika vituo mbalimbali vya polisi nchini na yaliyoongoza kwa idadi ni ubakaji (5,899), mimba kwa wanafunzi 1,677 na ulawiti1, 114.



Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa Kagera, Rebecca Gwambasa. **PICHA ZOTE: LILIAN LUGAKINGIRA.**

MAZINGIRA

# Ndivyo ilivyo dhana ardhioevu, unyeti wake na inakopitia kitaifa

**Na Joseph Mwendapole**

UNAIFAHAMU ardhi oevu? Kwa lugha ya kitaalamu inaitwa 'wetland'. Kimsingi, ni maeneo ambayo kwa msimu wote wa mwaka, huwa na uoto na unyevu au chepechepe. Ni maeneo yenye umuhimu wa pekee duniani katika suala la uhifadhi wa mazingira.

Edika Mmasi, ni Meneja wa Maeneo Maalum na Mabadiliko ya Tabianchi wa Baraza la Taifa na Hifadhi na Usimamizi wa Maazingira (NEMC) anayeyataja maeneo hayo, kwamba yana mchango mkubwa katika kuongeza uchumi wa nchi.

Kuhusu umuhimu wa maeneo oevu, anasema ni nyenzo muhimu sana kiikolojia, kijamii na kitaifa kwa ujumla, kwani yana baioanuwai adimu duniani, ambazo hupatikana maeneo hayo pekee.

Edika anayataja kwamba, hayo ni maeneo yenye vyanzo vikuu vya maji na katika maeneo mengi duniani, yanatumika kuzalisha umeme,kunywesha mifugo, kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya nyumbani.

Anasema maeneo oevu yanatumika kwa shughuli za kimila na kiutalii, kukipatikana nyenzo za ujenzi, chakula na dawa za asili kupata vyanzo kwenye maeneo oevu. Ni chanzo kikuu cha nishati ya umeme na ardhi oevu zinasaidia kuchuja maji yanayokusanyika wakati wa mvua nyingi na kudhibiti mafuriko.

Pia, anaeleza kuwa maeneo hayo yanasaidia kurekebisha hali ya hewa na miamba ya maji, pakiwa ni makazi kwa viumbe hai. Ardhi oevu inasaidia kuchuja uchafu na sumu kwenye maji na inasaidia kuhifadhi rutuba na maji.



Bonde la Mto Rufiji, eneo la Ikwiriri, mkoani Pwani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### UTUNZAJI WAKE

Meneja Edika anasema, kwa umuhimu wake, maeneo oevu ni lazima yatunzwe na kulindwa kwa karibu, kuhakikisha yanabaki endelevu, kwani katika kutekeleza azma hiyo wizara, kwa maana ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha maeneo hayo yanatunzwa na kulindwa kikamilifu.

Anasema Tanzania ni miongoni mwa nchi 152 duniani zilizotia saini Mkataba wa Kimataifa wa Ramsar (Ramsar Convention) wa Februari 2, 1971 katika mji wa Ramsar nchini Iran wa kuhifadhi na kulinda ardhi oevu.

"Hapo ndipo yalipofanyika maamuzi ya kulinda maeneo ya ardhi oevu dhidi ya uharibifu, ili yaweze kutumika katika shughuli endelevu, kama vile vyanzo vya maji. Mpaka leo nchi zote mwanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Ramsar ifikapo tarehe mbili Juni kila mwaka, wanaadhimisha Siku ya Ardhi Oevu Duniani, Tanzania ikiwa moja wao," anasema.

Meneja Edika anaeleza kuwa, katika maeneo tengefu 1,608 duniani yanayochukua ukubwa wa hekta milioni 140, Tanzania ina maeneo manne tu yanayotambulika katika mkataba huo wa kimataifa.

Anayataja maeneo ya ardhi oevu kuwa ni; Muyovozi katika mto Malagarasi-Kigoma, bonde la Ziwa Natron-Manyara, Bonde la Mto Kilombero- Morogoro na Bonde la Rufiji-Mafia hadi Kilwa-Pwani.

Pia, ana ufafanuzi kwamba, maeneo hayo yanalindwa na mikataba ya kimataifa, ambako hayaruhusiwi kufanya shughuli zozote za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji, uvuvi, uwindaji na ukataji miti.

Anasema, pia kuna maeneo mengine ya ardhi oevu nchini, ambayo hayajaingizwa katika orodha ya maeneo tengefu chini ya usimamizi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

### PROGRAMU ILOYOBUNIWA

Anasema, mnamo mwezi Machi, 1990 NEMC kwa kushirikiana na Mfumo wa Hifadhi ya Wanyamapori Duniani (World Wildlife Fund - WWF) na taasisi ya kimataifa, International Union Conservation (IUCU), walianzisha programu ya kuhifadhi na kutunza maeneo oevu.

Edika anafafanua kwamba, kupitia programu hiyo walitoa ripoti iliyoainisha maeneo yote oevu ya Tanzania na kutoa mwongozo wa kitaifa wa programu ya ardhi oevu.

"Baada ya ripoti hiyo kuthibitishwa na kutambuliwa na serikali ya Tanzania, ikapewa mamlaka ya kuendelezwa programu ya kitaifa ya utunzaji na uhifadhi wa ardhi oevu," anasema Meneja Edika.

Anasema, Tanzania baada ya kuwasilisha ripoti inayohusu programu ya kutunza na kuhifadhi ardhi oevu katika mkutano mkuu wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu kuhifadhi na kutunza ardhi oevu, ulitolewa uamuzi kwa kila nchi mwananchama wa jumuiya hiyo kuanzisha programu yake ya kutunza na kuhifadhi ardhi oevu

### SERA NA SHERIA

Rose Mtui, ni Meneja wa Tafiti za Mazingira (NEMC), anasema kuna sheria na sera mbalimbali zinazosaidia kusimamia utunzaji ardhioevu, akizitaja kujumuisha Sera ya Wanyamapori ya Mwaka 2009; Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997; Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002; Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995.

Zingine anazitaja kujumuisha maeneo kama: Sheria ya Taifa ya maji ya mwaka 1999; Sera ya taifa ya Misitu ya Mwaka 1998; Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002; na Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 1997, pia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, imegusa suala la utunzaji na hifadhi ya maeneo oevu.

"Pia, Ajenda ya Taifa ya Utunzaji Mazingira ya Mwaka 2018-2022 (National Environmental Management Agenda (NERA), pia imewekea kipaumbele suala la Kutunza na Kulinda Mazingira, pamoja na kuutambua mkataba wa Ramsar wa Kutunza na Kuhifadhi Ardhi Oevu," anasema.

### CHANGAMOTO ZILIZOPO

Rose anataja shughuli za binadamu zinazofanyika kwenye maeneo oevu ni changamoto kubwa ya kimazingira katika kuhifadhi ardhi oevu. Hapo anafafanua:

"Hii ni kwa sababu maeneo haya ni mazuri yanayofaa kwa shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji, kwa mfano ardhi oevu ya Kilombero. Kwa sababu ya kuwepo shughuli hizi ujenzi wa makazi, unafanyia kuwa na ongezeko kubwa la watu."

Rose anasema kwamba, matokeo yake yamekuwa uharibifu wa maeneo kwa kiasi kikubwa, akitoa mfano wa maeneo oevu ya Mto Pangani, Bonde Kilombero na milima ya Usangu mkopani Mbeya katika ukanda wa juu wa Mto Ruaha, uharibifu umehusishwa moja kwa moja na binadamu, kupitia shughuli zao za kiuchumi mahali hapo.

Anahitimisha kuwa, uharibifu katika maeneo oevu Tanzania ni zao la matumizi mabaya ya ardhi oevu na kutokuwapo elimu kuhusu umuhimu wake katika sura za; thamani,matumizi na faida ya kutunza maeneo hayo.



Ukanda wa Ziwa Natron, mkoani Manyara.

AFYA

## CT SCAN YA KWANZA MKOANI...

# Waziri Mkuu: Hospitali Rufani ianze Januari Mosi, leteni umeme haraka!

**Na Neema Hussein, Mpanda**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokagua ujenzi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Katavi, katika eneo la Rungwa Mpanda, Agosti, 2021. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwananvua Mrindoko. **PICHA: MAKTABA.**

NI hali inayotuma salam za hamasa ya maendeleo na katika namna ya pekee, ujumbe ukifikia zaidi sekta ya afya, pale mkazi wa mkoa na hususan mji wa Mpanda, pale anapooanisha ziara ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na sekta ya afya.

Mzizi unaanzia Agosti mwaka jana alipotembelea na kukagaua ujenzi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Rukwa, mjini Mpanda, akaona mambo kadhaa, ikiwamo kasoro za ujenzi. Hakuondoka hivi hivi, akaacha maagizo yake, ambayo leo yanazalisha mambo kadhaa.

Katavi ni mkoa wenye wilaya tano na ulianzishwa miaka 10 na miezi minane iliyopita, ukimeguliwa kutoka Rukwa. Sasa rasmi unapata hospitali yake ya rufani, kupumzisha tegemeo lake la awali linalobaki katika hadhi, Hospitali ya Manispaaa (wilaya) Mpanda.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Afya (MMAM), ambao ndio mwongozo mkuu, ulianzishwa mwaka 2007 na kuanza kutumika mwaka mmoja baadaye, ukiwa na muundo; kila kijiji au kitongoji kinapaswa kuwa na zahanati, ilhali kata inakuwa na kituo cha afya.

Pia, ngazi ya wilaya kama ilivyo Mpanda, inakuwa na hospitali na mkoani kunakuwapo hospitali ya rufani, kama ilivyo kwa inayokaguliwa sasa kwa matarajio ya kuanza mwakani mjini hapa, yaani wiki mbili zijazo.

### ZIARA YA MAJALIWA

Kuanzia Jumatatu iliyopita, Waziri Mkuu Majaliwa akatia mguu tena kwenye Uwanja wa Ndege Mpanda, akiwajibikia ukaguzi wa maendeleo, ila kwa nafasi ya kipekee akirejesha jicho katika Hospitali ya Rufani, ambayo anakiri si haba, kuna jambo la faraja limefanyika.

Waziri Mkuu Majaliwa, baada ya kuwasili siku ya Jumatatu iliyopita, alitembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi Hospitali ya Rufani Mkoa Katavi, hata akaeleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi wake, akitamka sasa imefika asilimia 92, ikiwa ni zaidi ya mara mbili ya mwaka mmoja na robo uliopita, alipokuwa mahali hapo.

Anataja kasoro iliyochangia kusuasua, ni kwamba awali ujenzi ulionyesha kusuasua, kutokana na kusimamiwa na watu kutoka wizarani, wakiwa jijini Dar es Salaam.

"Tulikuwa tunachelewa sana maana hata manunuzi yanafanywa Dar es Salaam wakati vifaa vyote viko hapa mjini, nikawambia hapana! Jengo hili liwe chini ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala Mkoa ndio asimamie.

"Kamati ya Manunuzi ikaundwa na wakanunua bidhaa kutoka kwa wafanyabiashara wa hapa hapa Katavi, tutaagiza Dar es Salaam kama vifaa hivyo havipo Mpanda, ili tutekeleze maagizo ya serikali ya kusema miradi mikubwa iwanufaishe wananchi.

"Nilikuja nikapata ndani nikakuta asilimia 45, leo hii nimepita nimekuta asilimia 92. Maana yake nini? Tunaenda kuanza kutoa huduma! Nilikuwa namuuliza Mganga Mkuu, hapa asilimia 92 tunachelewa nini kuanza?," akasema Waziri Mkuu, aliyemalizia ziara jana.

Ni swali ambalo Majaliwa, akajibiwa shida iko katika upatikanaji huduma ya umeme, ambao haujafika mahali. Hapo akahoji zaidi: "Meneja wa TANESCO yupo hapa! Meneja wa TANESCO njoo hapa utuambie mkandarasi yupo, umeme wewe unao, hapa unakuja lini? Tunataka tuanze huduma za hospitali si umeme unao?"

Ni swali ambalo Waziri Mkuu akajibiwa na Meneja wa TANESCO Mkoa Katavi, akitamka:"Mheshimiwa Waziri Mkuu, mpaka kufika Desemba 23 mwaka huu, tutakuwa tumefikisha huduma ya nishati ya umeme hapa."

Hapo ndipo Majaliwa akaendelea kutoa maagizo kimkoa kwamba hadi kufikia Januari Mosi 2023, hospitali hiyo inatakiwa kuwa imeanza kutoa huduma kwa wananchi wa mkoa wa Katavi.

"Daktari wa Mkoa asije akashindwa kuleta vifaa vya umeme hapa umekwishaniahidi hapa, tumemaliza maneno hapa na mkandarasi popote alipo ajipange katika hili, alete umeme hapa asije kuingia kwenye matatizo bure, tumekwishakubaliana hapa!

"Pesa ya mkandarasi ipo, umeme upo mjini, nguzo zipo tena zimeishafika hapa. Kwa hiyo jipange popote ulipo na Katibu Tawala Mkoa, lisimamie hili," anaagiza Waziri Mkuu Majaliwa.

Waziri Mkuu anasema imekwishafika wakati si wa umma kufunga safari tena za kwenda kutibiwa katika miji ya Dar es Salaam, Dodoma na Mbeya kutokana na vifaa vya kisasa kama vile 'CT-Scan' kufikishwa katika hospitali hiyo.

"Spidi iongezwe, tumalize lile jengo la mama na mtoto ili mama na mtoto wasiendelee tena kurundikana tena pale chini ya manispaa, waje hapa mkoani," anaeleza Majaliwa.

### WAHUSIKA SERIKALINI

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Profesa Abel Makubi, alifika katika hospitali hiyo mwaka jana pia na yeye alitoa maelekezo kwa ofisi ya mkoa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu.

Anasema, hospitali hiyo itagharimu kiasi cha shilingi bilioni 12.4 na kati ya hizo tayari bilioni 9.6 zimekwishatolewa na serikali.

"Tuishukuru sana serikali ya Mheshimiwa Samia, kwa kuleta hizo fedha na kuufikisha huu mradi hapa ulipo, anasema na kuendelea:"Waziri Mkuu, itakapokamilika hii hospitali ambayo tunaitegemea Desemba 30, mwaka huu huduma zitaanza kutolewa."

"Hapa kila kitu kitakuwa kimekamilika, ambapo kwa mara ya kwanza katika mkoa huu, wananchi wa mkoa wa Katavi watapata huduma ya CT-SCAN," anaeleza Profesa Makubi, kwamba matarajio ni kuhudumia wagonjwa 170 kutoka wagonjwa 140 waliotibiwa kwenye hospitali ya zamani.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) Dk. Festo Dugange, anasema hospitali iliyotumika kama ya mkoa, sasa itatumika kwa ajili ya Manispaa Mpanda na tayari Rais Samia ameshatoa shilingi milioni 900 kwa ajili ya kuikarabati.

"Waziri Mkuu, katika mwaka huu wa fedha serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuleta vifaa tiba katika vituo vya afya vitano vinavyojengwa katika Manispaa ya Mpanda. Pia, imetenga shilingi milioni 150, kwa ajili ya kujenga zahanati tatu, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma karibu na makazi yao.

"Kwa maelekezo ya Rais, vituo vyote vilivyokamilika vianze kutoa huduma kwa wananchi na tayari vituo hivyo vimeanza kutoa huduma ya OPD (wagonjwa wa nje), vifaa vinaletwa kwa ajili ya kulaza na kuanza kufanya upasuaji," anasema Dk. Dugange.

Anasema kwa mwaka uliopo wa fedha, serikali inatarajia kuleta gari jipya la wagonjwa kwa ajili ya rufani za wagonjwa wa Manispaa ya Mpanda, pamoja na gari la usimamizi wa huduma za afya.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiongozwa kushoto kwake na Dk. Serafini Patrice, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Katavi, alipokagua majengo mapya yanayotarajiwa kuzinduliwa wiki mbili zijazo. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**.

AFYA

UKATILI WA KIJINSIA...

# Simulizi mithili ya kusadikika mke katika kipigo na akafungiwa porini

**Na Zanura Mollel, Arusha**

BADO ni ndani ya msimu wa kupaza sauti dhidi ya ukatili wa kijinsia. Ndani yake kuna ushuhuda mpana, kila mmoja unajitegemea. Moja ya maeneo hayo ukatili huo unahusu kuoa au kuolewa katika umri mdogo, katika jina rasmi 'ndoa za utotoni.'

Je, ndoa hizo za utotoni ni nini? Msingi wake ni pale msichana au mvulana anapoingia katika ndoa akiwa chini ya umri. Huwa kati ya msichana na mvulana na mwenza anayemzidi umri.

Sababu zake kuu ni mila, pia desturi au mawazo kongwe hasa kwa mtoto wa kike jukumu lake ni kuolewa na kuzaa na hana haki nyingine ya msingi kuamua, bali kuamriwa.

Wasichana wengi huolewa baada ya kupata mimba wakiwa na umri mdogo, wakati mwingine nako kuna shinikizo la familia kutaka aolewe. Hata kama si wajawazito, huangukia uhusiano chini ya miaka 18, ambako utu uzima unaanza. Umasikini kifamilia nao unachangia.

Ndoa hizo tayari zina ishara ya madhara mbalimbali ndani ya jamii, ikiwamo watoto wa kike kukosa haki ya elimu, kupata mimba katika umri mdogo, huku miili yao ikishindwa kuhimili hatari ya maambukizi kama ya virusi vya Ukimwi (VVU), kwa sababu haijajengeka kikamilifu kukabili usalama wa afya yao.

**MHANGA WA TUKIO**

Mwanamama (jina tunalo) kutoka kijiji cha Gelailumbwa wilayani Longido, ni msichana anayeishi maisha ya ndoa za utotoni takribani miaka miwili, akidai kupitia mateso mengi.

Anasimulia zama za ndoa yake kila alipofanyiwa ukatili, alikuwa anarejea nyumbani kwa wazazi, ila hakupata msaada na akaambulia kurejeshwa kwa mume bila ya kupapo suluhu.

Mama huyo anasema alipigwa na rafiki wa mume huyo, kwa 'kosa' la kumwaga dawa ya mifugo iitwayo taramaisine, miezi miwili iliyopita. Ni dawa aliyopewa na mume ihifadhiwe na ikatolewa na ikatokea bahati mbaya akajikwaa na chupa ikaanguka na kupasuka.

Baada ya kuhofu mume angecharuka, akaenda kwa rafiki wa mume amuombee msamaha kwa mkasa huo, mama huyo akifafanua alichoambulia ni kipigo kutoka kwa rafiki ambaye akamrejesha kwa mama mkwe.




Sehemu ya kampeni dhidi ya ndoa za utotoni mkoani Arusha, ambazo huendana na uonevu kwa mabinti wanaoolewa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Anasimulia namna mama mkwe wake akaenda ndani na kuleta kamba afungwe, ili aendelee kupigwa, akiendeleza simulizi: "Nikafungwa kamba na kutundikwa kwenye mti, huku nachapwa nguo zangu zikiwa zimechanika. Rafiki wa mume wangu akiniambia ananipiga ili nikashitaki katika ofisi ya kijiji na mama mkwe akasema, nipigwe ili nirudi nyumbani kwetu mahari yao irudishwe.

"Wakati napigwa, mume wangu hakuwepo, alikuwa machungani na aliporejea alikuta nimefungwa kwenye miti na yeye akaanza kunipiga na walipoona wamechoka kunipiga wakanifungua kamba, mama mkwe akaniletea mfuko wa salfeti nikalala nje.

"Asubuhi mume wangu akaniambia niende machungani, nikamwambia naumwa, nilikuwa siwezi hata kusimama! Akasema nina kiburi, wakanichukua na rafiki yake wakanipeleka porini nikafungwa kamba miguu na mikono ikakutanishwa, nikaanza kuchapwa huku sina nguo ya aina yoyote mwilini.

"Waliniacha porini nikiwa sina nguo bado nimefungwa, nilikaa kwa siku tatu porini,vijana waliokua wakichunga waliniona walinisaidia kunifungua kamba, lakini sikuwa na nguvu ya kutembea nikabaki pale.Akatokea baba mmoja akanisaidia kwa kunibeba hadi nyumbani kwake.

"Tulipofika nyumbani kwake




alimuita mama yake akamwambia mama lete mafuta ya kondoo tumpe huyu mtoto hali yake ni mbaya sana. Nimemuokota porini amepigwa ni ndugu na mama yangu. Hivyo, namuita mjomba!

"Alimpigia simu baba yangu akamweleza kuwa ameniokota porini na hali yangu ni mbaya, hivyo alimuita kuja kuniona. Baba yangu alipofika alianza kulia baada ya kuniona na hali ile, akanibeba mgongoni kwa sababu hali yangu haikuwa nzuri.

"Ilibidi aite pikipiki ili aweze kunipeleka hospitali, tukiwa njiani baba yangu alikuwa analia sana, akachukua simu na kupiga ofisi ya kata akiomba watu walionipiga wakamatwe."

***KAULI YA WADAU***

Mkurugenzi wa shirika la Tembo lililopo wilayani Longido, Paulina Sumayani, anasema shirika hilo limejikita kusaidia maisha ya watoto wa kike walioko kwenye mazingira hatarishi na mwaka jana, waliokoa wasichana 42 waliomaliza darasa la saba, kwa kuwapeleka shule za sekondari, wasiolewe.

Pia, anasema mwaka huu unaoisha, kuna watoto 38 waliopo kwenye nyumba salama, wakisubiri matokeo ya darasa la saba waweze kuwaendeleza na elimu ya sekondari.

Atuganile Chisunga, ni Ofisa Ustawi wa Jamii wilayani Longido, anasema wilayani humo ukatili ni mkubwa wanaofanyiwa watoto kuingia katika ndoa, wanakokumbana na vipigo, pia ukeketaji kutoka kwa wanajamii wenyeji.

Anaeleza ripoti inaonyesha mwaka jana ukatili wa kingono pamoja na ndoa za utotoni ziliripoti matukio 53, pia walifanikiwa kunusuru ndoa za utotoni 11, huku ukatili wa vipigo ukiripotiwa matukio 17.

Kwa mwaka uliopo hadi sasa, mimba za utotoni zilizoripotiwa kutoka shuleni ni 25 na watoto wasichana tisa walinusuriwa kutoka ndoa za utotoni na analalamika kwamba kesi nyingi hazifanikiwi, kutokana na kukosekana ushahidi na wanajamii kutokubali kutoa ushirikiano.

**SHERIA INAVYOTENDA**

Rebecca Gyumi, ni Mkurugenzi Mtendaji wa asasi Msichana Initiative, pia mdau mtetezi anayefuatilia kesi zinazohusiana na ndoa za utotoni akitetea mabinti. Alifungua kesi katika mahakama kuu ya Tanzania dhidi ya vipengele vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inayoruhusu ndoa chini ya miaka 18 kwa wasichana.

Mahakama Kuu ilikubaliana na hoja yake, ikitaka Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ifanyiwe mabadiliko kwa kuwa kuna vipegele haviendani na katiba ya nchi.

Pia, hukumu hiyo iliona katika vifungo hivyo vinabagua haki za mtoto wa kike, ikilinganishwa na wavulana. Binti kuruhusiwa kuolewa katika umri huo mdogo, kwa ridhaa ya mzazi.

Sheria ya mtoto ya mwaka 2009, kimsingi inamtambua mtoto kuwa ni mtu mwenye umri chini ya miaka 18.

AFYA

## KISHINDO CHA AWAMU ZA UVIKo – 19...

# Jinsi wagonjwa walivyomaliza mitungi gesi, serikali ilivyoelemewa gharama

**Na Elizabeth Zaya**

***Alhamisi iliyopita, safu hii ilikuwa na sehemu ya kwanza ya makala ya mazungumzo kati ya Nipashe na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, akiainisha walivyopokea kishindo cha maradhi Uviko 19, milima na mabonde katika kuikabili, ikiwemo chanjo. Leo, endelea na simulizi ya vita vilivyoendelea. Fuatilia;***

==

INAPOTAJWA mradi, vita, tukio au kampeni yoyote ya umma, daima huangukia gharama. Je ujio wa ugonjwa Uviko 19 ulikuwaje? Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume anasimulia namna serikali ilivyobeba mzigo kugharimia hewa tiba kwa wagonjwa, katika wimbi la kwanza na la pili la mlipuko huo.

Anasema idadi ya wagonjwa waliolazwa na hawakuwa na uwezo wa kugharimia hewa tiba ilikuwa kubwa, hata serikali ikalazimika kubeba mzigo huo, ili kuwanusuru, baada ya wengi wao kushindwa kumudu gharama.

Dk. Mfaume anasema wengi walikuwa wakipelekwa katika vituo vya kutoa huduma hiyo ya Uviko-19 wakiwa katika hali mbaya na hawakujiandaa, huku hali halisi ya wagonjwa wenyewe, ilikuwa vigumu kuwaacha badala yake walilazimika kuokoa maisha, pasipo kujali hatima ya mwajibikaji wa gharama za huduma.

"Katika wimbi la kwanza na la pili la Uviko-19, kuna eneo ambalo ndilo lilitugharimu na ilitumika gharama kubwa ambayo hatujawahi kutumia kabla ya hapo, ni la matumizi makubwa ya hewa tiba," anasema Dk.Mfaume.

"Gharama hii ilitufilisi pia kwenye mzigo wa gharama kwa vituo tulivyokuwa tukitolea huduma, pia mzigo wa gharama kwa jamii iliyokuwa inakuja kupata huduma," anasema na kutoa ufafanuzi kwamba wengi waliolazwa mahali hapo kwa uhitaji wa hewa tiba, iliwachukua wastani saa 24 hadi kati ya siku tatu na wiki moja au zaidi, kukihitajika mitungi mikubwa.

"Watu wengi waliokuwa wakilazwa kwenye wodi ya wagonjwa mahtuti, walikuwa wakitumia mitungi mikubwa kabisa. Kuna watu walikuwa wanatumia mitungi minane mpaka 10 na mtungi mmoja ulikuwa unagharimu mpaka Sh.40, 000. Kwa hiyo unapotumia mitungi 10 kwa saa 24 ambayo tunahesabu ni siku moja ni karibu Sh.400,000," anaeleza Dk.Mfaume.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alipotoa neno la kitaifa kuhusu maradhi Uviko – 19. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

"Sasa ni Mtanzania gani ambaye anaweza kumudu kila baada ya saa 24 au siku moja atumie kiwango hicho cha fedha, tena katika eneo moja tu la hewa tiba, hapo bado hajajigharimia katika huduma nyinginezo," anahoji na kujipatia jibu, kwamba ndio ilikuwa shinikizo iliyorejeshwa kwa vituo vya kutoa huduma vya kiserikali kuubeba mzigo huo.

"Kwa hiyo, ni lazima tuishukuru serikali kwa kugharimia kwa ukubwa matibabu bila malipo, kwa sababu tungesema tuweke msimamo kwamba ni lazima kila mtu alipe, wengi wasio na uwezo ingekuwa hatari sana kwao.

"Hapo ninazungumzia hewa tiba pekee, bado sijazungumzia zile dawa nyinginezo walizokuwa wakipatiwa na katika kipindi hizo baadhi ya wagonjwa walikuwa wanapelekwa kwenye vituo wakiwa katika hali ambayo si rahisi kuwaacha.

"Hivyo, iliwalazimu wahudumiwe kwanza kabla hata hawajachangia chochote na hata baada ya kupona, hawakumudu maana unakuta mwingine ametumia mitungi hata 30 au zaidi ya hapo. Baadhi ya gharama walikuwa wanatakiwa kugharimia kidogo, lakini wengi walikuwa wanakuja hawana hata cha kuchangia na sisi kutokana na hali walizokuwa nazo, ilikuwa inatuwia vigumu kuwaacha. Tulibeba mzigo kwa kusaidiwa na serikali.

**KINACHOENDELEA SASA**

Dk. Mfaume anasema, bado kuna kazi inafanyika kubaini gharama halisi ambazo serikali imetumia kuhudumia wagonjwa wa Uviko -19, vilevile kujua gharama halisi ya kumtibu tangu mgonjwa anapolazwa, hadi kutoka.

Je, pesa za kugharamia zilipatikanaje? Mganga wa Mkoa anafafanua: "Rasilimali fedha ambayo ilikuwa inatakiwa iende sehemu nyingine, ilikuwa inatumika zaidi kwenye kutibu wagonjwa wa UVIKO 19, kitu ambacho ni hatari. Lakini, tuishukuru sana serikali kwa kuleta chanjo na hii tuone nia yake ya dhati katika kupambana na ugonjwa huu, la sivyo hatari ingekuwa kubwa."

Mganga huyo Mkuu wa Dar es Salaam, anasema mpaka sasa idadi ya wananchi waliochanja kwa mkoa huo ni milioni 3.2 na kwamba lengo lao mpaka mwisho wa mwezi huu watakuwa wamechanja wote.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Afya mnamo Desemba 5, mwaka huu kuhusu mwenendo wa Uviko-19, mikasa mipya ya ugonjwa imeongezeka kutoka 272 ya Oktoba 29 hadi 442 mnamo Desemba 2 mwaka huu, huku kukiwa hakuna aliyelazwa au kuripotiwa kifo.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa hadi kufikia Desemba 2, mwaka huu jumla ya watu 29,123,387 kati ya walengwa 30,740,928 ambao ni sawa na asilimia 94.7 wamepata dozi kamili ya chanjo yaUviko-19.



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume.

Mgonjwa wa kwanza kuripotiwa nchini kuugua ugonjwa wa Uviko-19 ilikuwa ni Machi mwaka 2020 na ndipo serikali ilichukua hatua mbalimbali za kupambana nao, ikiwamo kuleta ya hiari.

USHUHUDA KILICHOJIRI

Mkazi wa Kilongawima, Kata ya Kunduchi, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, anasimulia namna baba yake alivyokumbwa na ugonjwa huo katika wimbi la kwanza na walihangaika kupata nafasi katika vituo vya kuhudumia wagonjwa wa Uviko-19, kwa sababu vilikuwa vimejaa.

"Ilitusumbua sana mpaka kupata kituo kwanza kwa ajili ya kumpima na hivyo kumpatia kitanda. Aliugua nyakati za usiku kama saa sita hivi, tukawasha gari kumkimbiza hospitali, jamani tulizunguka mpaka tukachoka, kila kituo tulikuwa tukienda tunaambiwa pamejaa.

"Usiku ule tulikata tamaa, tukamuomba daktari wake mmoja alikuwa anamtibu aje amwangalie ndiye akamsaidia, lakini akatushauri twende tena kesho yake hospitali tusikate tamaa. Kwa hiyo, kulipokucha tukambeba tena, bahati nzuri tukaja kupata kituo kama saa nne hivi asubuhi ambako palikuwa na nafasi na walivyompima na matokeo kutoka, ikabainika kwamba ana dalili zote za Uviko-19.

"Baada ya kupata, shida nyingi tuliyokutana nayo ni oksijeni (mtungi wa gesi), yaani ilikuwa ya shida, lakini tulipambana mpaka tukapata ya kuanzia, halafu kesho yake kituo kikawa kimepata nyingine. Tukashukuru Mungu ila gharama tuliyotumia ilikuwa ni kubwa sana, kiasi kwamba kama angeugua kipindi ambacho hatuna fedha sijui ingekuwaje," anasimulia.

Anasema, ni aina ya uzoefu uliowafanya hata pale serikali ilipotangaza kuleta chanjo ya ugonjwa huo, wao hawakusita kuwahi kwenda kuchanja.

"Yaani unajua mwanzo tu pale Rais alipozindua chanjo, sisi tulikuwa wa kwanza kusomba familia nzima kwenda kuchanja wala hatukujiuliza mara mbili, maana tulishuhudia baba alivyohangaika. Ni mzazi wetu, lakini tulikuwa tunaogopa hata kumsogelea. Yaani, kwa sasa tunajiamini kabisa, hatuna hofu na ugonjwa tena kama ilivyokuwa awali."

MAZINGIRA

# Haya hapa usiyoyajua kuhusu Mto Ruvuma

**Na Mwandishi Wetu, Songea**

MTO Ruvuma ni miongoni mwa vivutio vitano vya utalii vinavyoubeba mkoa Ruvuma. Vingine ni Ziwa Nyasa, Makumbusho ya Taifa ya Majimaji, Ushoroba Selous-Niassa, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Utalii wa Kiutamaduni na Kihistoria.

Mratibu wa Utalii Kanda ya Kusini, Deborah Mwakanosya, anasema Mto Ruvuma unaubeba mkoa kwa kupita katika wilaya zote tano; Songea, Mbinga,Nyasa, Namtumbo na Tunduru.

Anasema ni mto mrefu kuliko yote Afrika Mashariki na miongoni mwa mito maarufu Afrika, ukianzia kwenye misitu ya milima ya Matogoro Manispaa ya Songea na kumwaga maji yake Bahari ya Hindi.

"Katika Milima ya Matogoro Manispaa ya Songea, tunakutana na chanzo cha mto Ruvuma. Ukiona chanzo hicho, ni mfano wa kisima kidogo sana, ambacho kimetoa mfereji mdogo, lakini kazi yake huko mbele huwezi kuongelea katika hali ya kawaida na kueleweka kwa jamii," anafafanua Deborah.

Anasema, kisima hicho kidogo chenye mfereji mdogo kwenye Milima ya Matogoro kipo umbali wa mita 1500, kukiwa na urefu kilomita zaidi ya 800 na upana wa kati ya mita 300 hadi 500, kutegemea na eneo.

Kwa mujibu wa mhifadhi huyo, Mto Ruvuma umebeba fukwe mbalimbali zinazovutia wageni wengi ambapo anazitaja fukwe nyingi za kuvutia zinapatikana kwa wingi katika hifadhi ya Taifa ya mazingira asilia ya Mwambesi iliyopo wilayani Tunduru.

Anasema katika hifadhi hiyo, Mto Ruvuma umetengeneza visiwa na fukwe nzuri za kuvutia ambazo zinamwezesha mtalii kuogelea na kuona wanyama wengi ambao wapo katika hifadhi hiyo kando kando ya Mto Ruvuma wakiwemo tembo, mamba, simba, jamii ya suala na samaki wa aina mbalimbali.

Hata hivyo, Mratibu huyo wa Utalii Kanda ya Kusini, anasema msukumo wa mto kufika katika Bahari ya Hindi na kumwaga maji yake, unaanzia wilaya ya Songea milima ya Matogoro, ukipita katika shamba maarufu la Aviv, ambalo wanaendesha kilimo cha umwagiliaji wa zao la kahawa, kupitia mto Ruvuma ambao wameajiriwa watumishi zaidi ya 3000.



Uhalisi wa mto Ruvuma.

### PENYE MRADI

Kutokea hapo, anasema mto huo umepita hadi katika eneo la Tulila wilayani Mbinga, ambako Shirika la Watawa wa Katoliki wa Mtakatifu Agnes, wameweka mradi mkubwa wa umeme wa maji, kwenye maporomoko ya Mto Ruvuma.

Mkuu wa Shirika hilo, Sista Richards Chiwinga, anasema kuna mitambo miwili, yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya umeme megawati tano. Analitaja Bwawa la Tulila kuwa lina ukubwa wa mita za ujazo milioni 1.14.

Nipashe imeshuhudia maporomoko ya Mto Ruvuma katika eneo la Tulila, yana mandhari ya kuvutia utalii, hata shughuli za kuogelea na kuendesha mtumbwi. Hadi sasa, Mto Ruvuma una umaarufu barani Afrika.

Mto Ruvuma katika Wilaya ya Nyasa umepita kwenye Pori la Akiba la Liparamba na inasonga hadi eneo la Mkenda mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, kulikojengwa daraja kubwa la mita 98, linalogawa Tanzania na Msumbuji kupitia Mto Ruvuma.

Deborah anabainisha, Mto Ruvuma unasonga hadi wilayani Namtumbo kwenye Jumuiya za Uhifadhi Wanyamapori Vijijini, ambazo ni Kimbanda, Kisungule na Chingoli na kwamba Mto Ruvuma unaendelea hadi Msitu wa Hifadhi ya Mazingira asilia Mwambesi wilayani Tunduru.

"Mto Ruvuma katika hifadhi ya Nwambesi, kuna vivutio vya aina zote ikiwemo michezo ya kuendesha mitumbwi, ambayo kwa mara ya kwanza Tanzania mchezo wa kuendesha mitumbwi ulizinduliwa mwaka 2019 katika eneo la Wenje, Mto Ruvuma na watalii 22 ambao walitoka nchi 16 duniani walishiriki," anasimulia.

### YA KIPEKEE

Mratibu huyo wa Utalii Kanda ya Kusini, anabainisha historia, maji ya Mto Ruvuma yalitumika katika Vita ya Majimaji, kuanzia mwaka 1905 hadi 1907. Anafafanua: "Eneo la Mwambesi kuna maporomoko ya Sunda, ambako anahifadhiwa ndege mdogo zaidi duniani anaitwa 'Pantiole' ambaye anakula Samaki akiwa hai, hivyo anaogelea kwenye maporomoko hayo kujipatia samaki."

Anasema maporomoko ya Sunda ndiyo eneo pekee ambalo lilitumika kama darubini ya watu waliopigana vita ya porini nchi jirani ya Msumbiji na wananchi walipotoroka vita, waliutumia Mto Ruvuma kuvuka kupata mapumziko.

Mtalamu na mbobevu huyo wa mazingira, anasema safari ya mto huo ukishapita katika wilaya zote za mkoa Ruvuma, unasonga katika daraja la Umoja wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara na kuendelea hadi mkoani Mtwara.



Shuguli zikiendelea ndani ya Mto Ruvuma. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### MTAALAMU UHAMIAJI

Mwamba Lihami, ni Ofisa Uhusiano katika Kituo cha Uhamiaji Mtambaswala wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara, kulikojengwa Daraja la Umoja katika Mto Ruvuma, lenye urefu wa zaidi ya mita 700 kuunganisha Tanzania na Msumbiji, anasema katikati ndiyo mpaka wa nchi hizo mbili.

Anafafanua kuwa, Mto Ruvuma unaanzia milima ya Matogoro Songea na kushoto ni Mto Rujenda, umeanzia Ziwa Kihuta nchini Msumbiji na kwamba kuwapo mito hiyo miwili, inaonyesha umuhimu wao.

Anataja lingine la kujifunza, ni mwonekano wa majimbo mawili ya nchini Msumbiji, Niassa na Delgado Msumbiji. Hapo anafafanua, jimbo la Niassa kupitia Mto Ruvuma ni hifadhi kubwa ya Wanyama nchini Msumbiji inayoitwa Hifadhi ya Taifa ya Niassa, ikiwa katika orodha ya hifadhi 11 ya nchi hizo, Niassa ni ya pili, ikitanguliwa na Limpopo.

"Baada ya udhibiti wa majangili na wawindaji haramu nchini Msumbiji na Tanzania, hivi sasa wanyama wanazaliana kwa wingi kwenye Hifadhi ya Niassa na Tanzania pia inanufaika kwenye hifadhi zinazopakana na Hifadhi ya Niassa, ambazo ni Lumesule, Mwambesi na Ushoroba wa Selous – Niassa, ambako wanyama wamezaliana kwa wingi hasa tembo,"anasema Lihami.

Anakitaja Kijiji cha Negomano nchini Msumbiji, kinapakana na Mto Ruvuma kupitia Daraja la Umoja, ambalo neno ' Negomano' kwa kireno lina maana 'makutano ya mito miwili ya Ruvuma na Rujenda', hivyo wakoloni wa Kireno waliamua kuweka ngome yao katika eneo la Negomano.

Anasema ndani ya Mto Ruvuma katika eneo la Daraja la Umoja, wapo wanyama wengi wa majini kama viboko na mamba na kwamba wanyama katika eneo hilo, wanaonekana kirahisi na kwamba Mto Ruvuma kutoka eneo la Mtambaswala, unaambaa kupitia wilayani Masasi, Mtwara hadi eneo la Msimbati kufika Bahari ya Hindi.

Hata hivyo, anasema Mto Ruvuma kama ulivyo mkoa Ruvuma, una manufaa mengi katika mkoa jirani wa Mtwara, katika Kijiji cha Masuguru wilayani Nanyumbu ambapo kunatarajiwa kuanzishwa mradi mkubwa wa maji, ambayo chanzo chake ni Mto Ruvuma, ukitarajiwa kuwanufaisha wananchi wilayani Nanyumbu na vijiji vyake vingi.

Anasema katika wilaya ya Masasi, pia wananchi wananufaika katika kijiji cha Chipingo, penye mradi mkubwa wa maji unaofanya kazi sasa.

### OFISA HIFADHI

Devis Orio ni Mhifadhi, katika Hifadhi za Bahari ya Ghuba ya Mnazi na penye maingilio ya Mto Ruvuma, anasema hifadhi hiyo ilianzishwa mwaka 2000 na anaitaja kuwa eneo la kilometa za mraba 650, kati yake kilomita 220 ni nchi kavu na zilizobaki ni maji, kukiwapo rasilimali nyingi

Kwa mujibu wa Orio, Mto Ruvuma unamwaga maji yake katika Bahari ya Hindi kwenye eneo la Msimbati mkoani Mtwara nchini Tanzania na Rasi ya Delgado nchini Msumbiji.

# Wanafunzi watafiti na kuibuka na majibu ya shida maji Mto Ruvu

**Na Elizabeth Zaya**

WANAFUNZI wawili Halima Muhunzi na Gloria wameibuka kutoka shule ya sekondari ya wasichana Kibaha washindi wa jumla wa Tuzo ya mwaka ya Wanasayansi chipukizi Tanzania (YST)ambayo hufanyika kila mwaka.

Wanafunzi hao waliibuka kidedea, baada ya ugunduzi wao wa kisayansi ulioonyesha angalizo na hatari ya chanzo cha maji cha Mto Ruvu kuwa hatarini, kushindwa kusambaza maji kwa miaka mitano ijayo, endapo uharibufu wa mazingira unaofanywa katika chanzo hicho hautadhibitiwa.

Pia, wanafunzi hao walitoa angalizo kwa Mamlala ya Majisafi na Majitaka (DAWASA) kuacha kutumia njia aina moja katika usambazaji maji katika mikoa hiyo mitatu kutokana na uharibifu unaofanywa katika chanzo hicho.

"Tulifanya utafiti ambao ulilenga kujua kwa undani athari zinazochangia chanzo cha maji cha Mto Ruvu kupungua kila mwaka na kusababisha adha ya maji kwa wananchi wa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro," anasema Halima.



Halima Muhunzi na Gloria Tibaijuka, wakipokea tuzo baada ya kuibuka washindi wa jumla katika Tuzo za kisayansi za YST, kulia ni Ofisa Mtendaji wa Shirika la Karimjee Jivanjee Foundation(KJF), Caren Rowland, kushoto aliyevaa koti ni mshirika wa Shirika hilo la KJF, Vinoo Soimaya.
**PICHA: ELIZABETH ZAYA**

Anafafanua, baada ya kutafiti kwa kutembelea kila mara eneo la Mto Ruvu, walibaini ipo hatari ya chanzo hicho cha maji kinachotegemewa na wakazi wa mikoa mitatu kushindwa kusambaza maji hayo kwa miaka mitano ijayo kama uharibiru huo utaendelea kufanyika na endapo DAWASA wataendelea kutumia njia zile zile katika usambazaji wao wa maji.

"Baada ya kufanya utafiti wa kina, tumebaini kwamba upo uwezekano mkubwa wa Mto Ruvu kukauka au kutokuwa na uwezo wa kusambaza maji katika mikoa hiyo mitatu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu,"anasema Halima.

"Katika utafiti wetu, tumebaini kwamba baadhi ya wananchi wanaoishi karibu na mto Ruvu wanakata miti hovyo, wanalima na wengine wanapitisha mifugo yao humo humo na hivyo kuharibu chanzo hicho cha maji ambacho ni muhimu na kinachotegemewa katika mikoa hiyo mitatu."

"Lakini pamoja na uharibifu huo unaofanyika kandokando ya chanzo hicho muhimu cha maji na pamoja na idadi ya watu wanaozidi kuongezeka kila siku wanaotegemea chanzo hicho, bado DAWASA hawabuni njia na mbinu nyinginezo za kusambaza maji, wanatumia zile zile za miaka yote na hili ni mojawapo ya vitu vinavyochangia adha ya maji kwa wananchi kila mwaka."

"Tukabaini kwamba kama uharibufu huo utaendelea kwa namna hiyo na endapo Dawasa nao wataendelea kutumia njia na mbinu zile zile katika usambazaji maji, uwezekano wa kusambaza maji kwa miaka mitano ijayo itakuwa ngumu kidogo."

Wanafunzi hao katika utafiti wao wanapendekeza serikali kutafuta chanzo kingine cha maji cha kuaminika kitakachosambaza maji kwa mkoa wa Dar es Salaam pekee na hivyo kupunguza mzigo kwa mto huo ili utumike kusambaza kwa mikoa ya Morogoro na Pwani pekee.

"Tunaona kwamba endapo mkoa wa Dar es Salaam una idadi kubwa ya watu na shughuli za kiuchumi zinazotegmea maji kutoka mto Ruvu ni nyingi kiasi ambacho unaelemewa na kuuweka katika hatari ya kushindwa kwa siku za usoni endapo hali itaendelea kuwa kama ilivyo,"wanashauri wanafunzi hao.

Pia, wanafunzi hao wanaishauri serikali kujenga sehemu kubwa za kuhifadhia maji na kuacha kutegemea mito pekee kusambaza maji.

Ushauri mwingine ni kwa wakulima, kwamba wanatakiwa kutumia teknolojia ya kilimo cha kuhifadhi maji ili kunapotokea upungufu wa rasilimali hiyo kwenye mito, wanatumia hayo yaliyohifadhiwa.

Mbali na kupata medali, fedha tasilimu baada ya kuibuka na ushindi huo wa jumla, pia wamepata udhamini wa masomo ya chuo kikuu.

Mwanzilishi mwenza wa YST, Dk.Gozibert Kamugisha, anasema idadi ya wanafunzi waliowasilisha maombi ya kufanya kazi za ugunduzi za kisayansi ambazo huratibiwa na Shirika hilo la Wanasayansi Chipukizi imeongezeka kutoka 579 mwaka jana hadi kufikia 1143 mwaka huu.

Anasema kazi hizo za ugunduzi hufanywa na wanafunzi kutoka shule mbalimbali za Tanzania Bara na Zanzibar ambazo hushindanishwa na washindi kupewa zawadi za fedha taslimu, medali pamoja na kufadhiliwa masomo ya vyuo vikuu.

Ofisa Mtendaji wa Shirika la Karimjee Jivanjee Foundation ambao ni wadhamini wakuu wa maonyesho hayo, Caren Rowland, anasema mpaka mwaka jana shirika hilo limedhamini wanafunzi 37 kwenda vyuo vikuu na mwaka huu wataongeza wengine wanne walioshinda mwaka huu kwenda kusoma katika vyuo mbalimbali vya elimu ya juu masuala ya sayansi.

Rowland anasema Shirika hilo limepanga kuendelea kutoa udhamini kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika maonyesho hayo na kwamba lengo ni kujenga msingi kwa wanafunzi hao kuwa na ari ya kitaaluma na kupenda masomo ya sayansi pamoja na kuongeza idadi ya wanasayansi na wabunifu nchini.

---

## CHEMSHABONGO NA -00 31 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. gandamiza, fyanda
3. koma
7. jongea mahali
8. pesa ya Afrika kusini
9. kitu cha thamani kubwa
12.elezwa
13.taifa lililoasisiwa na Kwameh Nkrumah
14.mzazi wa kiume
16.Jimbo kubwa Marekani ambalo Urusi ililiuza
17.Walau

Chini:
1. nyumba ya wanyama
2. toa fedha kulipia bidhaa
4. tolewa mchango kwa ajili ya jambo 5. rasimu
6. kipawa
10.janibu
11.tunda lenye mibamiba
14.balaa
15.umoja wa neno mabua

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | 2 | | ■ | 3 | 4 | | 5 |
| | ■ | | ■ | 6 | ■ | | ■ | |
| 7 | | | | | ■ | | ■ | |
| | ■ | | ■ | 8 | | | | |
| 9 | 10 | | 11 | | ■ | | ■ | |
| ■ | | ■ | 12 | | | | | |
| 13 | | | | | ■ | | ■ | ■ |
| ■ | | ■ | | ■ | 14 | | 15 | |
| 16 | | | | | | ■ | | ■ |
| ■ | | ■ | | ■ | 17 | | | |

Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| BATA | MAU |
| ADAMU | ARI |
| TAMA | KAA |
| AMIRI | ADA |
| MTEMI | AMI |
| ASILI | AMA |
| UMEME | AU |
| UDENDA | AMRI |
| TAMATI | AMI |
| MSAMBA | EDA |
| GITAA | BATI |
| CHANA | CHUI |
| ELIMU | PAKA |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ■ | | A | | |
| | | | | | ■ | M | | |
| | | | | ■ | | R | | ■ |
| | ■ | | ■ | | | I | | |
| ■ | | | | | | ■ | | ■ |
| | | | | | ■ | | ■ | |
| ■ | | ■ | | ■ | | | | |
| | | | | | ■ | | ■ | |
| ■ | | ■ | | | | | | |
| | | | ■ | | ■ | | ■ | |

Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | A | J | I | S | I | ■ | K | ■ |
| A | D | A | M | U | ■ | B | A | A |
| N | A | N | A | S | I | ■ | T | ■ |
| I | B | A | R | A | ■ | S | A | A |
| ■ | U | ■ | I | ■ | U | H | A | I |
| M | ■ | M | S | I | B | A | ■ | N |
| A | ■ | ■ | H | ■ | A | B | R | A |
| T | A | P | A | N | Y | A | ■ | ■ |
| A | ■ | U | ■ | O | A | N | A | ■ |
| A | G | A | N | A | ■ | I | ■ | ■ |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| D | U | N | I | A | ■ | T | ■ | T |
| U | ■ | A | ■ | ■ | K | A | D | A |
| N | E | N | O | ■ | ■ | N | ■ | N |
| I | G | I | Z | A | ■ | G | ■ | D |
| ■ | E | ■ | A | N | D | A | Z | I |
| A | S | A | ■ | Z | ■ | Z | ■ | K |
| C | H | I | N | A | ■ | A | D | A |
| H | A | B | A | ■ | I | ■ | ■ | ■ |
| I | ■ | U | N | I | T | A | ■ | ■ |
| A | ■ | ■ | I | ■ | A | U | L | A |



## Wauzaji viuatilifu wadaiwa kufanya kazi hiyo bila mafunzo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wauzaji wa maduka ya viuatilifu katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wanadaiwa kufanya kazi hiyo bila kupata mafunzo ya matumizi sahihi ya viuatilifu hali inayosababisha wakulima kutopata taarifa sahihi kuhusu matumizi ya bidhaa hizo.

Hayo yalisemwa juzi na baadhi ya wauzaji wa maduka hayo kutoka mikoa ya Mbeya, Songwe na Katavi wakati wa mafunzo maalumu ya matumizi sahihi ya viuatilifu yaliyoandaliwa kwa ushirikiano kati ya Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHRA) na Shirika lisilokuwa la kiserikali la HELVETAS Tanzania.

Mafunzo hayo yalishirikisha washiriki 44 kutoka katika mikoa hiyo na 12 pekee walijilipia gharama za mafunzo na wengine 32 walilipiwa na Shirika la HELVETAS ambalo ni miongoni mwa watekelezaji wa programu ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya bustani, AGRI-CONNECT.

Akisoma risala ya wahitimu wa mafunzo hayo, Mataliwa Rubuye, alisema kutokana na hali hiyo, kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi mabaya ya viuatilifu hali inayosababisha madhara mbalimbali.

"Athari zinazotokana na hali hii ni pamoja na uharibifu wa mazingira, wanyama pamoja na mazao ya uvuvi, hii inasababishwa na matumizi holela ya kemikali zilizomo kwenye viuatilifu hivi, tunaomba udhibiti uongezeke," alisema Rubuye.

Mkuu wa TPHRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Emmanuel Mausa, alisema wanatoa mafunzo hayo kwa wauzaji wa maduka hayo kila mwaka ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya viuatilifu hivyo.

Alisema wauzaji wa maduka hayo wanatakiwa kuifikisha elimu kwa wakulima ili kupunguza madhara yanayotokana na kemikali zilizomo kwenye viuatilifu na kuhakikisha uzalishaji wa mazao mbalimbali unaboreshwa.

Alisema wafanyabiashara hao pia wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka ili kuhakikisha kila anayefanya kazi hiyo amepata mafunzo na ana cheti kilichotolewa na taasisi hiyo.

# Wazee washauri h'shauri Mbeya kuanzisha shule nyingi sekondari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZEE mkoani Mbeya, wameshauri serikali ya mkoa wa huo kuzielekeza halmashauri zake zote kuanzisha shule nyingi za sekondari za kidato cha tano na sita ili watoto wote wanaofaulu kidato cha nne wanufaike na elimu bila malipo inayotolewa na serikali.

Wazee hao wamependekeza kila halmashauri kujenga shule hizo zisizopungua 10 kufikia mwaka 2025 ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na ngazi mbalimbali za elimu baada ya serikali kuanzisha sera ya elimu bila malipo.

Wlitoa ushauri huo juzi walipozungumza na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Dk. Steven Mwakajumilo, walipomtembelea ofisini kwake kumshauri kuhusu mambo mbalimbali ya maendeleo.

Mwenyekiti wa wazee hao, Mwaiseje Polisya, alisema kuanzishwa kwa shule hizo kutasaidia wanafunzi wote wanaohitimu kidato cha nne na kufaulu kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu kama ilivyo lengo la serikali.

Alisema umoja wa wazee unaamini kwamba mwenyekiti huyo wa chama tawala ana uwezo mkubwa wa kuisimamia serikali na kuibua miradi ya maendeleo.

"Pia tunashauri vijengwe vyuo vingi vya ufundi stadi ndani ya mkoa wetu ili wale vijana wanaoshindwa kuendelea na masomo ya elimu ya juu wapate ujuzi wa kuwawezesha kujiajiri, hii itatusaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu," alisema Polisya.

Alisema vyuo hivyo vitasaidia pia kuzalisha nguvukazi ya kufanya shughuli za ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo itakayokuwa inatekelezwa ndani ya mkoa huo na hata katika maeneo mengine nchini.

Alisema umoja wa wazee unashauri kila halmashauri ya mkoa huo kununua hisa katika kampuni zinazochimba madini katika wilaya zake ili kushiriki katika usimamizi wa rasilimali hiyo na kupata faida kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Alishauri pia CCM kuimarisha maridhiano na ushirikiano miongoni mwa vyama vya siasa mkoani humo ili kuimarisha amani na mshikamano utakaochochea maendeleo ya mkoa.

Dk. Mwakajumilo, aliwashukuru wazee hao kwa ushauri walioutoa ambao utasaidia kuboresha baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa hayatekelezwi vizuri.

Alisema uwapo wa wazee hao unawaongezea maarifa viongozi huku akisisitiza kuwa ushauri waliotoa utazingatiwa na chama hicho.

Aliwataka wazee hao kuendelea kushirikiana na chama ili kuuletea maendeleo mkoa huo na taifa kwa ujumla.

"Sisi viongozi wa chama tuko tayari kushirikiana nanyi wazee, ushauri wenu ni mzuri sana na niwahakikishie kwamba tutauzingatia, yote mliyoyasema yana viashiria vya kuleta maendeleo," alisema Dk. Mwakajumilo.

Aliwaomba wazee hao kuendelea kutoa ushauri kwa viongozi wa serikali wanapobaini kuwa kuna mambo hayaendi sawa ikiwamo utekelezaji na usimamizi wa miradi.

Aliwataka viongozi wa serikali katika mkoa huo kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kutekeleza miradi na kuisimamia ili wananchi waone thamani halisi ya miradi hiyo.



Wahadhiri na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) wakifuatilia mhadhara uliokuwa unatolewa na Prof. Livin Mushi wa Chuo Kikuu cha Ardhi (hayupo pichani), mhadhara huo ni sehemu ya matukio yanayofanyika chuoni hapo kuelekea kwenye mahafali ya chuo hicho. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Operesheni ukaguzi, uhakiki silaha kudhibiti uhalifu

**Na Nebart Msokwa** ,CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, imetangaza kuanza operesheni maalumu ya kukagua na kuhakiki silaha zote zinazomilikiwa na wananchi wilayani humo ili kudhibiti matukio ya uhalifu ambayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara.

Mkuu wa wilaya hiyo, Mayeka Simon Mayeka, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu operesheni hiyo itakayodumu kwa muda wa mwezi mmoja.

Alisema ukaguzi huo utaanza leo na kufikia ukomo Januari 15, 2023, kila mwananchi anayemiliki silaha atatakiwa kuiwasilisha kwa ukaguzi.

Alisema vitu vitavyoangaliwa kwenye uhakiki ni pamoja na uhalali wa umiliki wa silaha hizo na matumizi yake huku akisisitiza kuwa jambo hilo linafanyika kutokana na makubaliano ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya.

"Ni utamaduni wetu kila mwaka hasa tunapoelekea mwisho wa mwaka kufanya uhakiki wa silaha za moto, lengo huwa ni pamoja na kukumbushana matumizi sahihi ya silaha hizo, kwahiyo wananchi wote wanatakiwa kuwasilisha ili zikaguliwe," alisema Mayeka.

Alisema wameshatoa taarifa kwa wananchi katika maeneo yote ya wilaya hiyo kuanza kuwasilisha silaha hizo kwa ajili ya kuzikagua na zitakaguliwa kila siku kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa.

Mayeka alisema baada ya ukaguzi kufikia ukomo, operesheni nyingine itafanyika ya kufanya msako wa silaha zote ambazo zitakuwa hazijahakikiwa.

Alisema wamiliki wa silaha watakaobainika kuwa hawakuziwasilisha kwa ajili ya ukaguzi, watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani.

Aidha, kuelekea sikuu za mwisho wa mwaka, Mayeka aliagiza Jeshi la Polisi kitengo cha Usalama Barabarani kuongeza umakini wa kukagua magari yote na kuwachukulia hatua madereva watakaobainika kuwa wanakiuka sheria za usalama barabarani.

Alisema magari yote ya abiria yatakayobainika kuwa ni mabovu yaondolewe barabarani.

Katika hatua nyingine Mayeka alipiga marufuku wafugaji kutoka katika maeneo mbalimbali kuingiza mifugo wilayani humo kwa maelezo kuwa mifugo iliyoko ndani ya wilaya hiyo inatosheleza maeneo yaliyotengwa.

Alisema ongezeko la mifugo kwenye wilaya hiyo linaweza likasababisha migogoro ya wakulima na wafugaji kama inavyotokea kwenye maeneo mengine nchini.

"Wenyeviti wa vijiji, watendaji wa vijiji na kata tumeshawapa maelekezo ya kutoruhusu uingizaji wa mifugo, kiongozi yeyote atakayebainika kushirikiana na wafugaji kuingiza mifugo wilayani kwetu tutamchukulia hatua kali," alisema Mayeka.

Alisema baadhi ya wafugaji wanaingiza mifugo kinyemela kutoka katika Wilaya ya Mbarali na Wilaya ya Songwe na kusababisha matatizo kwenye maeneo wanayokwenda kuchungia.





# Mafanikio elimu kwa watoto yanatokana na ufuatiliaji wazazi

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

WAZAZI na walezi ili wafanikishe ndoto za watoto wao kielimu wanatakiwa kufuatili kwa karibu maendeleo yao.

Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi wa Shule ya Msingi na Awali ya Maki Brilliant, Dk. Godfrey Magoti, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wazazi na walezi kwenye hafla ya ugawaji wa vyeti kwa wanafunzi waliofanya vizuri kitaalamu shuleni hapo.

Dk. Magoti alisema ni muhimu wazazi na walezi wakahakikisha wanatoa ushirikiano kwa watoto na walimu ili kufikia malengo waliojiwekea kwenye maisha yao.

"Bado kuna changamoto kwa baadhi ya wazazi na walezi ambao wamekuwa wakiwakwamisha watoto wao kwa kushindwa kuwasaidia kitaaluma hali ambayo imekuwa ikiwasababishia walio wengi kushindwa kufikia ndoto walizojiwekea kwenye maisha yao," alisema.

Pia aliwataka walimu kuwajibika kwa watoto katika kuwasimamia kiroho na kijamii ili kuwajengea uwezo katika masomo yao badala ya kuwaacha wakijisimamia wenyewe na kujikuta wakijiingiza kwenye makundi maovu.

Naye Mkuu wa Shule ya Maki Brilliant, Shaibu Beya, aliwataka wazazi kuacha tabia ya kuua vipawa vya watoto wao kwa kuviendeleza ili wafikie malengo yao.

Alisema, watoto walio wengi wana vipawa vya aina mbalimbali, lakini wanakwamishwa na wazazi wao kufikia malengo yao.

Diwani wa Kata ya Buigiri, Keneth Yindi, akizungumza na wazazi na walezi, aliwataka waweke elimu kwa watoto wao ili kuwasaidia katika maisha yao ya baadaye.

Alisema wakiwekeza kupata elimu watoto wao kuna faida kubwa inayoweza kupatikana ikiwamo kuwapata viongozi wenye maadili ya kiroho na kijamii watakao watumikia watu kwa kufuata misingi ya haki na sheria.



Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Sarah Chizingwa, akizungumza kwenye kongamano la wadau wa elimu jumuishi (hawapo pichani), lililowakutanisha wazazi, walezi, watendaji kutoka serikalini na taasisi binafsi lililofanyika Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ataka utafiti mbegu zinazoendana mabadiliko tabianchi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. John Jingu, amesema watafiti wa kilimo nchini wanapaswa kutumia matokeo ya utafiti wanaofanya kuboresha mbegu za mazao zinazoendana na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Jingu aliyasema hayo jana jijini hapo kwenye kikao cha kuelimisha wadau kuhusu kazi za muunganiko wa taasisi za kimataifa za utafiti wa kilimo (CGIAR), ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili (ASDP II) kwa kuboresha utaratibu wa miradi ya One CGIAR.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuzingatia utafiti utakaongeza uzalishaji.

"Kupitia mkakati wa utafiti na ubunifu wa mwaka 2030 CGIAR, imeanzisha mkakati unaojulikana kama OneCGIAR ambao unalenga kufanya utafiti na maendeleo sasa ili tukuze sekta zetu za kilimo, mifugo na uvuvi lazima tuwekeze katika utafiti na maendeleo hivyo mkakati huu utasaidia katika uzalishaji na tija," alisema.

Alihimiza utafiti wa mbegu unaofanyika unapaswa kusaidia kuleta tija na faida katika shughuli za wakulima, wavuvi na wafugaji pamoja na kuendeleza ugunduzi wa mbegu mpya hasa katika kipindi cha mabadiliko ya hali ya hewa.

"Hivi karibuni kumekuwa na mabadiliko ya hali ya hewa hivyo utafiti tunaoufanya uendane na hali ya hewa ya kipindi husika ukizingatia sasa hivi misimu ya mvua imebadilika kwa hiyo tunahitaji mbegu zinazoendana na mazingira na namna ya kukabiliana na wadudu waharibifu," alieleza.

Alisisitiza ushirikishwaji wa vijana katika sekta ya kilimo kwa kuwa ndiyo yenye ustawi na matokeo chanya kwa wananchi.

Aidha, alishauri uwapo wa ushirikiano kati ya wizara za kisekta na wadau wa maendeleo kwa kuanzisha miradi mikubwa itakayoleta matokeo chanya katika sekta hizo muhimu kupitia mkakati huo.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Dk. Geoffrey Mkamilo, alibainisha kuwa kufanyika kwa utafiti wa mbegu kunasaidia kubaini hali ya mbegu, kero na namna ya kuboresha uzalishaji wake utakaoendana na kipindi husika.

"Warsha hii inatuweka pamoja kama wataalamu na wizara za kisekta kubalishana uzoefu na namna ya kufanya utafiti wenye manufaa katika sekta zote za kilimo. Mifugo na uvuvi kubaini mbegu bora na wakati husika wa kuzifanyia kazi ziweze kuzalisha mazao bora kwa ajili ya kuimarisha lishe na kipato," alisema.

Naye mtaalamu kutoka OneCGIAR, Dk. Regina Kapinga, alifafanua kuwa licha ya kufanya utafiti unaowezesha mazao kuhimili mabadiliko ya tabianchi pia unazingatia uboreshaji wa virutubishi katika mazao ya uvuvi, mifugo na mimea.

# 'Mabadiliko tabianchi yameathiri wanawake, watoto zaidi'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISA programu wa Shirika lisilo la kiserikali la FORUM CC, linalojihusisha na mapambano dhidi ya mabadiliko tabianchi, Msololo Onditi, amesema maeneo mengi nchini yameathirika na mabadiliko hayo huku wanawake na watoto wakiwa katika hatari zaidi.

Onditi alibainisha hayo juzi alipokuwa akitoa taarifa ya shirika hilo kwa wabunge kuhusu mradi unaotekelezwa katika Wilaya ya Singida wa kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi kwa wanawake na watoto.

"Hali ilivyo sasa inaonesha kuwa waathirika wakubwa katika janga hili la mabadiliko tabianchi ni kundi la wanawake na watoto ndiyo maana tumeamua kutekeleza mradi huu wa miaka mitatu wa kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi kwa wanawake na watoto," alisema.

Onditi, alisema mabadiliko hayo yanapotokea yanasababisha ukame na kuwapo upungufu wa chakula wanawake na watoto ndiyo wanakuwa katika hatari zaidi.

"Unapotokea ukame maji yanakosekana hivyo wanawake ndiyo wanalazimika kwenda umbali mrefu kutafuta maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya familia lakini zipo familia ambazo zimeamua kuozesha watoto wao katika umri mdogo ili kupata fedha za kutunza famila kutoka na athari za mabadiliko tabianchi," alisema.

Kadhalika, alisema kukosekana kwa chakula cha kutosha kutokana na athari za mabadiliko tabianchi kunaathiri makuzi ya mtoto kimwili na kiakili.

Aidha, alisema ili kukabiliana na tatizo hilo mradi huo utahusika katika utoaji wa elimu kwa jamii ili kupunguza shughuli za kibinadamu zinazosababisha kwa kiasi kikubwa mabadiliko tabianchi.

"Pia kutoa elimu kwa wananchi kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa ambayo imekuwa sababu kubwa ya mabadiliko tabianchi," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum, Dk. Thea Ntara, alilishauri shirika hilo kuandaa programu za kutoa elimu katika maeneo ambayo bado hajaathirika sana na mabadiliko tabianchi.





# Soko Kuu Darajani kukarabatiwa kuwa na hadhi ya kimataifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum Serikali ya Mapinduzi, Masoud Ali Mohamed, amesema serikali imeanza ukarabati wa soko kuu la Darajani lililoko katika eneo la mji Mkongwe ili kurudisha haiba ya mji huo ambao upo katika hadhi ya miji ilioko katika urithi wa kimataifa.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalumu Wanawake, Mwanaidi Kassim Mussa, aliyetaka kujua maendeleo ya ukarabati wa soko hilo umefikia hatua gani.

Alisema ukarabati huo ni sehemu ya mikakati ya serikali unaotokana na utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 ya kuimarisha maeneo ya biashara ya wajasiriamali.

Alisema Soko la Darajani limo katika orodha ya masoko ya kihistoria ambalo kwa bahati mbaya halijafanyiwa matengenezo makubwa kwa muda mrefu tangu lilipojengwa miaka 100 iliyopita. Alisema ukarabati unaofanywa utaliwezesha soko hilo kufikia viwango na hadhi ya kimataifa katika utalii kwa wageni.

"Tumeanza ukarabati wa soko la Darajani ili kulifanya kuwa na hadhi ya kimataifa ya miji iliopo katika urithi wa mambo ya kale ambapo tunaamini ukarabati huo utakidhi vigezo muhimu vya usanifu wa majengo ya kale," alisema.

Aidha, alisema ukarabati huo unatarajiwa kukamilika mapema mwakani na wafanyabiashara wote waliokuwapo awali ndiyo watakaopewa kipaumbele na kurudi katika maeneo hayo.

"Ukarabati wa soko la Darajani unatarajiwa kukamilika mwakani ambapo wafanyabiashara waliokuwapo awali watapewa kipaumbele cha kwanza kufanya shughuli za biashara," alisema.

Pia alisema serikali inaendelea na kazi za kujenga masoko mengine makubwa matatu ikiwamo Chuwini, Mwanakwerekwe pamoja na Jumbi ili kuwawezesha wafanyabiashara kufanya shughuli zao kwa ufanisi mkubwa.

Alisema kazi za ujenzi wa masoko hayo matatu unafanywa na vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya awali kupewa sekta binafsi na kushindwa kufanya kazi hiyo.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Mwinyi Talib, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Z'bar yajipanga kujitosheleza chakula kilimo umwagiliaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo imesema imejipanga kuhakikisha Zanzibar inajitosheleza kwa chakula ikiwamo mpunga kwa kujenga miundombinu ya usambazaji maji katika mashamba ya wakulima.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Sulubu Kidongo Amour, katika kikao cha Baraza hilo, aliyetaka kujua serikali imejipanga vipi kuona inajitosheleza kwa chakula na kuacha kuagiza mchele nje ya nchi.

Khamis alisema serikali inatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mashamba ya wakulima wenye ukubwa wa hekta 1,053 katika mabonde sita ya Unguja na Pemba. Aliyataja mabonde ya mpunga yaliyoimarishwa kwa kujengwa miundombinu ikiwamo Cheju, Kilombero, Chaani, Kinyasini na Mlemele.

Alisema bonde la Cheju lenye ukubwa wa hekta 314, Kinyasini lenye hekta 184 Mlemela lenye hekta 44 yamekabidhiwa kwa wakulima. Alisema jumla ya wakulima 4,796 tayari wamekabidhiwa mashamba hayo kwa ajili ya kuanza shughuli za kilimo cha mpunga baada ya kukamilika ujenzi wa miundombinu.

"Napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa ujumla kwamba Wizara ya Kilimo imejipanga kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji ili kuiwezesha Zanzibar kujitosheleza na chakula na kupunguza kuagiza nje ya nchi," alisema. Waziri huyo alisema mkandarasi aliyepewa kazi hiyo anamalizia marekebisho madogo katika bonde la Kilombero, Chaani na Kibokwa ili yaweze kukidhi mahitaji ya wakulima katika kuendeleza kilimo hicho.

Alisema sekta ya kilimo cha umwagiliaji maji kwa Zanzibar inachangia pato la taifa kwa asilimia 30.5 huku kilimo cha umwagiliaji maji mashambani ikiwamo mpunga kipo kwa asilimia tano.

# KMKM yaanza kuvua samaki bahari kuu kuingiza mapato

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KIKOSI Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM), kimeanza kutekeleza malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuvua samaki katika eneo la bahari kuu ili kuingiza mapato.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Idara Maalumu ya Vikosi vya SMZ, Masoud Ali Mohamed, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani Pemba, Abdalla Kombo, aliyetaka kujua maendeleo ya kikosi cha KMKM katika uvuvi wa bahari kuu.

Alisema uvuvi wa bahari kuu ndiyo kipaumbele cha Serikali ya Zanzibar katika kuelekea sera ya uchumi wa buluu ambayo lengo lake ni kunufaika na rasilimali za baharini katika uchumi wa buluu.


Alisema Kikosi cha KMKM kimeanzisha uvuvi wa bahari kuu kwa kuvua samaki mbalimbali katika eneo hilo kwa kushirikiana na kutiliana saini makubaliano na Kampuni ya Tijara.

Alitaja samaki ambao tayari wameanza kuvuliwa na kikosi hicho na kuingiza mapato ikiwamo Jodari na Mbasi ambao wameanza kuuzwa kwa taasisi mbalimbali zikiwamo hoteli za kitalii na wananchi.

"Kikosi cha KMKM tayari kimeanzisha uvuvi wa bahari kuu kwa kushirikiana na kampuni ya Tijara hatua ambayo matarajio yetu makubwa hayo ndiyo malengo ya uchumi wa buluu," alisema.

Aidha, alisema Kikosi cha KMKM kupitia kambi zake kimeanzisha kilimo cha mazao ya baharini ikiwamo matango bahari ambayo soko lake kimataifa ni kubwa lenye tija kwa wakulima.

Alikipongeza kikosi hicho kwa kutekeleza kwa vitendo sera ya uchumi wa buluu ambayo ni kujikita na kunufaika na rasilimali za uvuvi wa baharini pamoja na mazao ya baharini ikiwamo mwani na matango pori.





# Sungusungu wadaiwa kumvunja mkono mtuhumiwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la jadi la Sungusungu linatuhumiwa kumpiga Veronica Magembe, mkazi wa Lyabukande wilayani Shinyanga na kumvunja mkono wa kulia wakimtuhumu mwizi.

Akizungumza na vyombo vya habari juzi, Veronica alisema siku ya tukio alikuwa ameenda mjini baada ya kurudi katika shughuli zake mjini Shinyanga, alikuta Sungusungu wakimsubiri nyumbani na kumuamuru alale chini ili apewe adhabu ya viboko.

Alisema alipowahoji kosa lake ni nini, walimwambia kuwa ni mwizi wakidai amemuibia mwanamke mmoja tisheti tatu, kitenge na viatu dukani kwake, bila kumsikiliza upande wake waliendelea kumpiga hadi kufikia hatua ya kumvunja mkono.

"Niliporudi nyumbani kutoka Shinyanga mjini nikawakuta Sungusungu wakiwa wananisubiria wakinituhumu nimeiba tisheti tatu, kitenge na viatu, wakaniambia dondoka chini wakaanza kunipiga fimbo, nikawaambia nina operesheni wakasema leo ndio itapona," alidai.

"Wakati nikiendelea kuwasumbua wasinipige wakaitwa sungusungu wengine sita jumla wakawa 11 wakanishika miguu na mikono, wakaanza kunipiga fimbo za juu juu bila ya kujali mimi ni mgonjwa wakaniumiza vibaya na kunivunja mkono."

Mtendaji wa Kata ya Lyabukande, wilayani Shinyanga, Shadrack Maduhu, alisema mwanamke huyo amekuwa na kesi nyingi za madai ya wizi, huku akieleza kuwa sungusungu wana utaratibu wao wa kutoa adhabu kwa wananchi.

Kiongozi wa sungusungu, Raphael Tabaro alisema mwanamke huyo amekuwa akijihusisha na vitendo vibaya vikiwamo vya wizi na amekuwa akilalamikiwa na wananchi.

Baadhi ya wananchi wa eneo hilo walisema tabia za Veronica sio nzuri na zinakera kwa sababu amekuwa akiiba vitu mbalimbali.

Waliomba achukuliwe hatua zaidi za kisheria pamoja na kumchunguza akili yake kama ni mzima.



Meneja mradi wa uimarishaji wa mabaraza ya watoto kutoka Shirika la Rafiki-SDO, Tangi Clement, akizungumza na viongozi wa Baraza la Watoto katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, kuhusu kupaze sauti zao juu ya vitendo vya ukatili ambavyo wanafanyiwa juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wavuvi 'waiangukia' serikali waongezewe muda

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wavuvi na wamiliki wa mitumbwi wanaofanya shughuli zao katika Ziwa Victoria, wameiomba serikali kuwaongezea muda ili kuachana na matumizi ya taa za betri kwa ajili ya shughuli za uvuvi wa dagaa.

Wavuvi hao wanatakiwa kutumia taa za mwanga wa jua (solar), badala ya taa zinazotumia betri katika shughuli zao za uvuvi.

Walisema ikiwa wataacha kutumia betri hizo kwa sasa bila kujiandaa watapata hasara kutokana na kutumia fedha nyingi kuzinunua.

Pia agizo hilo limekuja ghafla kutokana na baadhi ya wavuvi kufanya uwekezaji katika taa hizo na kusitisha matumizi yake kunaweza kuwasababishia hasara.

"Tunaomba kuongezewa muda hata kufikia mwezi wa sita mwakani ili na sisi tuweze kujiandaa kwani hata hivyo utafiti wa kubaini madhara yake bado haujafanyika kikamilifu maana hatujaambiwa ukali wa mwanga wa taa tunazozitumia kwa sasa na zile wanazotaka tutumie," alisema Mandondo Maro, mmiliki wa mtumbwi.

Edward Manna, mvuvi wa dagaa akizungumzia hatua hiyo alisema alikuwa amechukua mikopo na kuwekeza katika taa hizo.

Alisema alikuwa hajui kama taa hizo ni haramu na kuzisitisha ghafla kutamsababishia aingie kwenye madeni ambayo uwezo wa kulipa ni mdogo.

Akitoa ufafanuzi kuhusu marufuku hiyo, Kaimu Ofisa Mfawidhi ulinzi na usimamizi na rasilimali za wavuvi Kanda ya Ziwa, Laurent Mbujiro, alisema matumizi ya taa hizo ni ukiukwaji wa kifungu namba 16 kifungu kidogo (ii) cha sheria za uvuvi.

Novemba 17, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akiwa mkoani Mwanza, alitoa muda wa miezi miwili kwa wavuvi wanaotumia taa za umeme wa jua zinazotumia betri kuacha kwa kuwa zinadaiwa kuwa kichocheo cha uvuvi haramu na kuharibu mazalia ya samaki katika Ziwa Victoria kutokana na kuwa na mwanga mkali.

Aidha, aliwataka wavuvi wa dagaa kutumia taa zenye mfumo wa umeme jua moja kwa moja badala ya zinazounganishwa na betri kutokana na kubainika kuwa na madhara.

# Jamii yashauriwa kuwekeza malezi ya watoto

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

JAMII imeshauriwa kuwekeza kwenye malezi ya watoto wao ili kuwasaidia kutimiza ndoto zao katika maisha yao.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini hapo na Ofisa Ustawi wa Jamii Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Loata Molel, wakati akizindua jarida la Mbeleko ambalo linafundisha namna bora ya kulea watoto.

Alisema watoto ni kundi linalohitaji kulindwa na kujengewa misingi bora kwao na taifa kwa ujumla.

"Wazazi, walezi muda mwingi wamewekeza kwenye utafutaji wa riziki, lakini suala la malezi ya watoto wamewaachia wafanyakazi wa nyumbani, nawasihi wazazi kuweka ratiba ya kusoma majarida mbalimbali yanayohusu malezi ya watoto likiwamo la Mbeleko ili waweze kuwalea watoto vizuri na kuwajengea misingi bora," alisema Molel.

Alisema malezi na makuzi ya watoto ni eneo linalohitaji mkazo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa elimu ya namna bora ya kulea watoto.

"Sayansi na teknolojia imeleta mapinduzi makubwa katika kujua mambo mbalimbali, lakini imeleta tatizo kwenye malezi ya watoto kutokana na vitu vinavyokuwa vikioneshwa kwenye runinga, hivyo wazazi wanatakiwa kuwa makini ili kuwanusuru watoto wao ni ukweli usiopingika watoto wengi wanalelewa zaidi na runinga pamoja na mitandao ya kijamii, kuliko sisi tulivyolelewa miaka 50 iliyopita ambapo tulikuwa tunapata fursa ya kukaa na wazazi na kutusimulia hadithi za mafunzo," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la TAHEA lililoko mkoani Mwanza, Mary Kabati, akizungumza katika uzinduzi wa jarida hilo, aliwataka wazazi na walezi kupata mwongozo mzuri wa kuwalea watoto wao.

Alisema suala la malezi kwa watoto ni muhimu, lakini wazazi wengi hawana nafasi ya kukaa na watoto wao wala kujua maendeleo yao ya kimasomo na kwamba wataendelea kuihamasisha jamii kuweka mazingira rafiki kwa watoto hususani kwenye malezi.

Mratibu wa Miradi ya Elimu kutoka TAHEA, Peter Matyokoalezi, alisema malezi na makuzi bora ya mtoto yanaendana na lishe.

Alisema jarida hilo lina safu maalumu ya mapishi ya vyakula mbalimbali vya kitanzania kwa ajili ya lishe ya mjamzito, anayenyonyesha, mtoto na familia kwa ujumla.

Alisema jarida hilo linatumia mifano halisi ya utoaji malezi inayoonekana katika familia na jamii na kukosoa, kusisitiza na kuboresha malezi hayo kwa kutumia simulizi ambazo zimetoka kwa watu mbalimbali, vibonzo katika kuonyesha matukio yanayojitokeza kwenye familia na mitaani.

Mmoja wa wazazi waliohudhuria uzinduzi huo, Anamaria Mwenge, alisema kituo hicho kitasaidia wazazi na walezi kujua namna bora ya kuwatengenezea misingi mizuri watoto wao tangu wakiwa wadogo.

**HABARI KIMATAIFA**

# Rais wa Ghana akemea Afrika kuombaomba

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Ghana, Nana Akufo-Addo, amesema kuwa mataifa ya Afrika lazima yajiondoe kwenye utaratibu wa kuomba nchi za Magharibi ili kupata heshima ya kimataifa na kubadili mitazamo duni kuhusu bara hilo.

"Tukiacha kuwa ombaomba na kutumia pesa za Kiafrika ndani ya bara hili, Afrika haitakuwa na haja ya kuomba heshima kutoka kwa mtu yeyote, tutapata heshima tunayostahili. Tukifanikisha hilo basi, heshima itafuata," alisema Akufo Ado.

**Waafrika wanastahimili zaidi nje ya bara kuliko ndani.**

Aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa viongozi wa Marekani na Afrika unaofanyika mjini Washington DC. Rais Akufo-Addo alihimiza mshikamano zaidi miongoni mwa Waafrika ili kushughulikia malengo ya pamoja.

"Waafrika wanastahimili zaidi nje ya bara kuliko ndani. Lazima tukumbuke kwamba kwa ulimwengu wa nje, hakuna kitu kama Nigeria, Ghana au Kenya, sisi ni Waafrika tu. Hatima yetu inategemea kila mmoja," alisema.

Kiongozi huyo alisema kuwa bara hilo lilikuwa na ujuzi na wafanyakazi lakini lilihitaji utashi wa kisiasa wa kufanya Afrika ifanye kazi.

Matamshi ya Addo yalikuja siku ambayo Shirika la Fedha la Kimataifa kukubali kuipa Ghana mkopo wa dola bilioni 3 ili kupunguza mtikisiko wa kiuchumi ambao haujawahi kushuhudiwa katika nchi hiyo ya Afrika Magharibi.

Makumi ya viongozi wa Afrika wako mjini Washington kujadili ushirikiano na Marekani huku kukiwa na ongezeko la ushawishi wa China na Urusi katika bara hilo. **BBC**

## Waghadhibishwa binti wa Rais kuwa na ofisi

**NAIROBI,** Kenya

WANANCHI wa Kenya wamepigwa na butwaa baada ya kusikia kuhusu kuwapo kwa ofisi ya binti wa Rais Willium Ruto, katika Ikulu ya nchi hiyo.

Katika video inayosambazwa mtandaoni, mtoto wa kiongozi huyo, Charlene Ruto, anaonekana akizungumza na hadhira katika mkutano wa kilele nchini Tanzania ambapo anatambulisha timu yake kutoka Kenya kuwa wanatoka katika ofisi ya binti wa rais.

Waliotambulishwa ni mshauri wake na mwingine ambaye ni mkuu wa biashara na uwekezaji katika ofisi ya binti wa rais.

Waliohudhuria walionekana kujibu kwa sauti kubwa kwa kupiga makofi na baadhi wakiangua vicheko.

Sheria za Kenya hazina ofisi ya binti wa rais na hakuna tangazo lolote la umma la kuanzishwa kwa ofisi kama hiyo.

Wakenya wengi katika mitandaoni ya kijamii wamekuwa wakipinga kile ambacho wengine wanakiona kuwa matumizi mabaya ya pesa za walipa kodi. **BBC**

## Russia yashambulia mji wa Kyiv

**KYIV,** Ukraine

MASHAMBULIZI ya ndege za Russia zisizoruka na rubani yameharibu majengo matano katika mji mkuu wa Ukraine, Kyiv.

Maofisa wa Ukraine hata hivyo walisema mifumo ya ulinzi wa mashambulizi ya kutokea angani iliharibu makombora mengi na hakuna vifo vilivyoripotiwa wala majeruhi.

Rais wa Ukraine, Volodymr Zelensky, alisema magaidi walifyatua makombora 13 yaliyobebwa na ndege zisizoruka na rubani zinazotengenezwa Iran, na yote yakaharibiwa.

Mji huo mkuu Kiev umesalia na utulivu kwa kiasi kikubwa baada ya shambulizi hilo, ambalo lilitokea mapema jana kabla ya kuanza shughuli za siku.

Mashambulizi hayo yanadhihirisha jinsi mji huo mkubwa kabisa wa Ukraine ulivyo katika hatari ya kushambuliwa na mashambulizi ya mara kwa mara ya Russia ambayo yameharibu miundombinu na maeneo mengine ya makaazi, hasa mashariki na kusini mwa nchi hiyo katika wiki za karibuni. **DW**



Baadhi ya nyumba na mali zilizoathirika na mafuriko katika mji mkuu wa DRC, Kinshasa juzi. **PICHA: BBC**

# Mafuriko yaua watu zaidi ya 120 DRC

**KINSHASA,** DRC

WATU zaidi ya 120 wameuawa katika mafuriko mabaya zaidi kuwahi kutokea na kuukumba mji mkuu wa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wa Kinshasa.

Wengi wa waliokufa walikuwa katika maeneo ya milimani ambao walikumbwa na maporomoko ya ardhi kutokana na mvua kubwa.

Mwandishi mmoja wa habari aliripoti kuona miili ya watu tisa wa familia moja ambao nyumba yao ilikuwa imeporomoka.

Hata hivyo serikali ya DRC imetangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa zilianza jana.

Waandishi wa habari walisema kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaohamia Kinshasa katika miaka ya hivi karibuni na jiji hilo linakabiliwa na upungufu wa mifereji ya maji na mipango duni ya mijini.

Uharibifu huo uliacha theluthi moja ya jiji bila maji na umeme, kulingana na mamlaka.

Wengi waliofariki walikuwa katika maeneo ya milimani, ambayo yalikumbwa na maporomoko ya ardhi.

Kinshasa ina wakazi wapatao milioni 15 na ni mojawapo ya miji mikuu yenye watu wengi zaidi barani Afrika.

Waziri Mkuu, Sama Lukonde, alitembelea vitongoji vilivyoathiriwa Jumanne pamoja na Gavana wa jiji hilo Gentiny Ngobila.

Gavana huyo alisema serikali ya mkoa italipa gharama zote za mazishi ya marehemu.

**RAIS KUKATISHA ZIARA**

Wakati huo huo, Rais wa nchi hiyo, Félix Tshisekedi, alisema kuwa atakatiza safari yake nchini Marekani, ambako anahudhuria mkutano wa kilele wa viongozi wa Marekani na Afrika, kutokana na mafuriko hayo.

Katika ujumbe wake wa Twitter, Tshisekedi alisema atarejea nyumbani leo baada ya mkutano wake na Rais Joe Biden.

Katika mkutano na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, katika mkutano huo, Rais Tshisekedi alilaumu mafuriko hayo kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, shirika la habari la AFP linaripoti. **BBC**

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**PASTORY M.KAZERI** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S1470-0130** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya KIARA mwaka 2017,na cheti cha **DIPLOMA** na **TRANSCRIPT** chenye index namba **18030602016 kozi ya ELECTRICAL AND BIOMEDICAL ENGINEERING** iliyotolewa na chuo cha **ARUSHA TECHNICAL COLLEGE (ATC)** mwaka 2021,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **MWA/IGO/RB/472280/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**PASCHAL EDWARD KITABOMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 3042/0093** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KANGAYE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHU/RB/466764/2022**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Ndugu REMIGIUS LWEYONGEZA BAITAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Bajaj Boxer yenye namba za usajili **MC806 CFE,** injini **Na. DUZWKM63201** na Chassis **Na. MD2A18AY9KWM93630.** Kadi hiyo ina majina ya **MOHAMMED ENTERPRISES (T) LTD.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/480340/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0767227019.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba**
**Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa Kagera**
**Usimamizi wa mirathi Na 69 2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU Frank Theophil Muganyizi wa Nyamkazi**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**Na Mixon F Muganyizi**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni ya Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote / maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11/01/2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 08/12/2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MTWARA**
**MKOA WA MTWARA**
**MAOMBI NA 74/2022**
**HAJIRA ALLY KAMPEHA............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**HABIBA DAIMA FUNDI...........MJIBU MAOMBI NAMBA**

**KUITWA SHAURINI**

**HABIBA DAIMA FUNDI POPOTE ULIPO,FAHAMU** kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 16 Januari,2022 saa 02:30 asubuhi.
UNAAMRIWA kuhudhuria mbele ya Baraza lililopo katika jengo la Baraza Idara Ya Ardhi Manispaa ya Mtwara siku hiyo bila kukosa,wewe au mwakilishi wako kisheria.Hati ya madai pamoja na vielelezo vingine vyote kuhusiana na shauri hili utavipata kwenye masjala ya Baraza.
FAHAMU KWAMBA kushindwa kuhudhuria Barazani siku hiyo shauri litapangwa kusikilizwa upande mmoja na kuamriwa dhidi yako.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe 13,Disemba,2022

**NGUKULIKE,N.O**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)MTWARA.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.154 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GODFREY KAROLO ALBANO**
**AND**
**IN THE MATTER OF ADMINISTRATION OF THE ESTATE OF THE LATE GODFREY KAROLO ALBANO**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION OF THE ESTATE OF THE LATE GODFREY KAROLO ALBANO**
**BY THOMAS ALBANO PANGANI**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 27 Day of 12,2022.

**Dated at Dodoma this 05TH day of 12, 2022.**

RESIDENT/DISTRICT MAGISTRATE COURT
RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT


# OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, Website: www.ippmedia.com


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

## OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA VIFAA VYA KUPAKA MIPAKO/ KUFUNIKIA CHUMA

## KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0107

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakia mafuta katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Kampuni zenye uzoefu kueleza nia yao kwa:

**Ugavi wa Vifaa vya Kupaka Mipako / Kufunikia Chuma.**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.
Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yasiyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA**:
BBN inahitaji nyenzo/vifaa vya kununua ili kufanya shughuli za kufanya mipako (in-situ coating) kwenye nguzo za chuma, ikihusisha kuandaa na kupaka rangi chuma sehemu zilizochomelewa au kufanyiwa ukarabati;

- Kwa utayarishaji wa chuma, BBN inahitaji mashine za kulipua ombwe (Vacuum Blasting Machines), isiyo na vumbi kwa kutumia steel angular abrasive hadi Sa 3 (ISO 8501-1) & Medium G profile (ISO 8503-2). Ikiwa kuna pembe/taswira ndogo ya chuma BBN inahitaji zana za Bristle Blaster brush.
- Kwa mipako, BBN inahitaji rangi ya kupuliza ya kushika mkononi isiyo na hewa (airless handheld spray) na kifaa cha kunyunyizia rangi kisicho na hewa kwenye magurudumu (airless spray unit on wheels)

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika maombi kwa kuonyesha:

- Wafanyakazi waliohitimu na kuidhinishwa kufanya kazi za Kuthibitisha Ubora / Kudhibiti Ubora (QA/ QC);
- Muda wa dhamana ya kazi wa miezi 24 na miaka 5 juu ya kasoro fiche baada ya kumalizika kwa muda wa dhamana;
- Wasifu wa kampuni ulio na uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa kifedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa kusimamia kandarasi husika,
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi / rekodi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza huduma kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa,
- Sera ya Ubora wa Kampuni na mipango ya Afya, Mazinginra na Usalama eneo la kazi na vyeti vya ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018) au vyeti sawa ;
- Kuzingatia kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com** . **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe katika lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **29 Disemba 2022 saa 12 jioni majira ya Tanzania.**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji yaliyo ainishwa hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

17195701

## NGOMENI ENTERPRISES

### NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **benki ya crdb** makao makuu Dar es salaam, tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) tu ili uweze kulipa deni lako ote pamoja na gharama za dalali. Kukaidi kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoiweka benki kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA / MAHALI | TAREHE/MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | PAUL MREMI LYIMO | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO REGENT ESTATE - KINONDONI | 30.12.2022 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2. | AVIT DAMACEN MLINDA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIMARA STOP OVER DAR ES SALAAM | 29.12.2022 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3. | ANJELA BIUS MKUMBWA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIBAGA – KINYEREZI DAR ES SALAAM | 29.12.2022 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4. | FLORA BERNARD HINJUSON | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO GEZAULOLE DAR ES SALAAM. | 16.01.2023 KUANZIA SAA 4 NA KUENDELEA |
| 5. | PASCAL PAUL SAMBAI | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO BUYUNI – CHANIKA DAR ES SALAAM | 11.01.2023 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 6. | THAMES VALLEY COMPANY LIMITED | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO BUNJU WILAYA YA KINONDONI DAR ES SALAAM. | 31.12.2022 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELA |
| 7. | IRENE SPARTA MAMKWE | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MSONGOLA - DAR ES SALAAM | 30.12.2022 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 8. | ARNOLD DOMINIC NYANGE& FORTUNATA ALPHAXED MAGOMA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO GOBA MTAMBANI, DAR ES SALAAM. | 29.12.2022 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 9. | JOYCE GUNTRAM LYASSA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MAKONGO DAR ES SALAAM. | 31.12.2022 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 10. | PILI STANLEY MMAJE | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KILEMELA KEREGE BAGAMOYO | 9.01.2023 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 11. | ABEL HENRY VEGURA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO BOMBA LA ZAMBIA KINGOLWILA -MOROGORO | 05.01.2023 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 12. | TITUS LAZARO MGIMBA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO PUGU BOMBANI , DAR ES SALAAM. | 11.01.2023 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 13. | KENNEDY CHRISTOSIA MATHEMU | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MADAFU – UKONGA DAR ES SALAAM | 18.01.2023 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. DHAMANA ITAUZWA KAMA ILIVYO
2. MNUNUZI ATALIPA MALIPO YA 25% YA BEI ITAKAYOFIKIWA SIKU YA MNADA NA ASILIMIA 75 ATALIPA NDANI YA SIKU 14.
3. MNUNUZI ATAKAYESHINDWA KULIPA KUMALIZIA 75% KATIKA MUDA ULIOPANGWA HAPO JUU, HATARUDISHIWA FEDHA LIZOLIPA AWALI NA MNADA UTARUDIWA SIKU NYINGINE UTAKAYOPANGWA.
4. GHARAMA ZOTE ZA KUBADILISHA HATI MILIKI, KUTWAA NYUMBA NA GHARAMA NYINGINEZO ZITAKUWA JUU YA MNUNUZI.
5. WATEJA WOTE MNAKARIBISHWA KUONA NA KUKAGUA NYUMBA MUDA WOTE ISIPOKUWA USIKU.

**MAWASILIANO**
**CRDB BANK PLC HEADQUARTER, NGOMENI ENTERPRISES DSM, SIMU : 0719974916/0753575752**

217196302


Kwa Habari Moto-moto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Zari kumzalia mpenzi wake mpya

**Na Mwandishi Wetu**

MREMBO Zarina Hassan amefunguka juu ya uwezekano wa kuongeza watoto na mpenzi wake wa sasa, Shakib Lutaaya, baada ya kukutana na wazazi wake.

Mpenzi huyo wa zamani wa nyota wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, ameweka wazi kuwa yuko tayari kupeleka mahusiano yake mapya katika kiwango cha juu zaidi.

"Shakib alinipeleka kuwaona wazazi wake na ilikuwa nzuri sana," alisema Zari.

Mahusiano ya Zari na Shakib yamekuwa yakikosolewa sana hasa mitandaoni, suala kuu likiwa tofauti zao za umri.

Zari ana umri wa miaka 42 wakati mpenzi wake huyo alitimiza miaka 31 hivi majuzi.

Mama huyo wa watoto watano alibainisha kuwa wazazi wa Shakib hawakuashiria tatizo lolote na mahusiano yao na kubainisha kuwa mkutano wao ulikuwa mzuri.

"Alinipeleka kuonana na wazazi wake na walikuwa wazuri sana, na sikumbuki hata kidogo wakilalamika kuhusu uhusiano huo," alisema raia huyo wa Uganda.

Zari pia alifichua kuwa anapanga kuongeza watoto zaidi na Shakib, lakini akabainisha kuwa si kwa sababu ya shinikizo la umma.

Haya yanajiri takriban miezi mitatu baada ya kudokeza kufunga pingu za maisha na Shakib baada ya kufichua kuwa mpenzi huyo sasa anapanga kupeleka posa kwa baba yake nchini Uganda.

"Shakib aliniambia jana kuwa anataka kukutana na baba yangu. Anataka kutoa posa kwa ajili ya ndoa, yuko tayari kunioa," aliongeza Zari Kiganda katika video ambayo iliwekwa kwenye Snapchat.





# MWIJAKU: WEMA USIJE KUMWACHA WHOZU

**Na Mwandishi Wetu**

MTANGAZAJI Mwijaku Burton, ametumia kisa cha Kajala Masanja kumwacha Harmonize na kumshauri nyota wa kike wa Bongo Muvi, Wema Sepetu, asifanye hivyo kwa mpenzi wake Whozu.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Mwijaku amemwambia Wema kuwa asidhubutu kumfanyia hivyo mtoto wa watu Whozu, kwani atashtuka kumkuta amelazwa mochwari kama gogo lisilo na uhai wala pumzi.

"Wema nakuombea dua usije ukafuata nyayo za Kajala. Maana huyu Whozu utamkuta mochwari ukimwacha.

"Kijana kajisahau hata akipigiwa simu hapokei, najua ni kwa sababu ya...Kama vipi hebu mmwage tuone kama ana moyo wa ustahimilivu kuishi bila Wema," aliandika Mwijaku.

Kuachana kwa Kajala na Harmonize kunaonekana kumgusa Mwijaku ambaye sasa ameonekana kumtetea Harmonize.

# *Diamond azindua studio Zanzibar*

**Na Mwandishi Wetu**

BOSI wa Lebo ya WCB, Diamond Platnumz, amezindua studio mpya za Wasafi FM visiwani Zanzibar.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alikuwa mgeni rasmi katika hafla ya uzinduzi wa studio hizo ambayo ilifanyika Jumanne asubuhi katika eneo la Migombani, Mnara wa Mbao.

"Ni baraka ya kipekee kupata bahati ya kuzinduliwa studio zetu za Wasafi FM na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi.

"Asante rais kwa kuendelea kuwanyanyua vijana. Wazanzibari na Watanzania wote tunawakaribisha katika uzinduzi wa studio yetu ya Wasafi FM Zanzibar," Diamond alisema.

Pia aliahidi kuwainua wasanii kadhaa kutoka Zanzibar kadri siku zinavyokwenda.



# MANDONGA AJA NA 'AKIPIGWA 'OYAOYA, AKISHINDA OYAOYA'

**Na Saada Akida**

BONDIA Karim Mandonga, amesema sasa amekuja na staili mpya kumkabili mpinzani wake, Ali Baba, katika pambano la Usiku wa Mabingwa linalotarajiwa kufanyika Desemba 26, mwaka huu katika Ukumbi wa AICC Lake Nyasa jijini Arusha.

**Akizungumza na gazeti hili jana, kuelekea pambano hilo la Usiku wa Mabingwa litalowakutanisha Mfaume Mfaume dhidi ya Iddi Pialali, Mandoga alisema ataingia na staili mbili ikiwamo ya 'Mtumbwi wa kifahari juu ya bahari' na 'Akipigwa Oyaoya na akishinda Oyaoya'**

Alisema safari hii amejipanga vizuri kuhakikisha anamtwanga mpinzani wake mapema katika pambano hilo la kufunga mwaka 2022.

"Ali Baba ajiandae, nimefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kufunga mwaka vizuri, nimeachana na staili zote sasa hivi atakutana na ngumi ya mtumbwi wa kifahari juu ya bahari," alisema Mandonga.

Mapambano mengine yatakayosindikiza usiku huo ni bondia wa kike, Zawadi Amos, ambaye atachapana na Halima Vunjabei huku Batuli Yassin akipanda uligoni dhidi ya Loveless Kokha.

Wengine ni Said Faraji dhidi ya Osama Arabi, Hassan Ndonga dhidi ya Ramadhan Kumbele, Haidary Mchanjo atakayezipacha na Yolanda Mchanja na Shaban Kaoneka dhidi ya Shaban Ndaro.



## *Kibu apewa ushauri Simba*

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Simba, Dua Said, amemtaka mchezaji wa timu yake hiyo, Kibu Denis, kucheza kwa staili yake ileile ambayo ilimfanya kusajiliwa kutoka Mbeya City badala ya kuwaiga kina Mosses Phiri na Clatous Chama, kitu ambacho kinamsababishia matatizo yote yanayomkuta.

Dua, aliyetamba kwenye miaka ya mwanzoni mwa 1990 hadi mwisho mwa miaka hiyo, huku akiichezea pia timu ya Taifa, Taifa Stars, jana alisema kuwa, Kibu si mchezaji mbaya kama ambayo watu wengi wanavyomsakama kwa sasa, ila tatizo lake ni kutaka kuiga wachezaji mastaa kwenye kikosi hicho ambacho wanauwezo wa kuuchezea mpira, wakati yeye hata kipaji hicho hana.

"Kibu ana matatizo, kinachomsumbua ni kutaka kuiga anavyocheza Phiri au Chama, ndicho kinachomtoa kwenye mchezo, yeye alipaswa acheze kwenye staili yake ambayo alikuwa anacheza kule alikokuwa Mbeya City na alivyokuwa anacheza msimu uliopita akiwa Simba akafunga mabao manane, lakini akitaka kucheza kama Phiri, hawezi yeye ana aina yake ya uchezaji, tofauti na hao anaowaiga na ndiyo iliyomleta pale.

"Hicho ndicho kinachomsumbua, akiacha hilo atarudi kwenye kiwango chake cha kawaida kilichozoeleka," alisema Dua ambaye pia alikuwa akicheza nafasi ya winga.

Kwa sasa wanachama na mashabiki wa Simba wamekuwa wakimlaumu mchezaji huyo karibuni kila mechi anayocheza kwa madai ameshuka kiwango, huku wengine wakimshutumu kukosa mabao ya wazi.

Mchezaji huyo mkongwe pia ameishauri timu yake hiyo ya zamani kuongeza nguvu kwenye baadhi ya maeneo kipindi cha dirisha dogo la usajili ili kukifanya kikosi kuwa imara.

**MAZOEZI...**



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini juzi katika Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, wakijiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Geita Gold itakayopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza. **PICHA: SIMBA**

## Dirisha dogo lafunguliwa, vikumbo vyaanza

**Na Adam Fungamwango**

DIRISHA dogo la usajili kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship na Daraja la Pili limefunguliwa leo na Shirikisho la Soka nchini (TFF), huku klabu zikiwa zimeshaanza kuhaha huku na kule kusaka wachezaji watakaoongeza nguvu kwenye vikosi vyao.

Taarifa kutoka ndani ya TFF imesema dirisha hilo linatarajiwa kufungwa Januari 16, mwakani, huku ikitarajiwa kutoa taarifa kamili leo juu ya mchakato mzima wa usajili utakavyokuwa.

Wakati klabu zikisubiri kufunguliwa dirisha hilo, kwa muda mrefu zilishaanza michakato ya kusaka wachezaji wa kuwasainisha mikataba kabla ya kuingiza majina yao katika mfumo rasmi wa usajili TFF dirisha hilo litakapokuwa wazi.

Tayari klabu mbalimbali zimeshajinasibu kuwa zinakwenda kuongeza wachezaji ili kuziba mapungufu ambayo yamebainishwa na mabenchi yao ya ufundi.

Klabu ya Simba ambayo mapema tu ilitangaza kufanya usajili kipindi hiki, ndiyo inaonekana huenda ikafanya usajili mkubwa kuliko zingine kutokana na mahitaji yao kwenye Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Tayari inahusishwa kumsajili Saido Ntibazonkiza kutoka Geita Gold na Cesar Manzoki kutoka Dalian Professional ya nchini China.

"Tunakokwenda ni kugumu kuliko tulikotoka kwa hiyo ni lazima tulete watu kweli, watu wenye ushindani, kwenye hili dirisha dogo tutafanya maboresho kidogo kwa ajili ya kuongeza nguvu na chachu kwenye michuano iliyo mbele yetu, Ligi Kuu inaelekea duru la pili ambalo ni gumu zaidi kwa hiyo ni lazima uwe na kikosi imara.

"Tunaelekea pia kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, lazima uwe na kikosi cha watu ambao watakuwezesha kushindana, kwa hiyo tutafanya maboresho kuelekea kwenye ubora tunaoutaka," alisema Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu ya Simba, Ahmed Ally.

Afisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema mapendekezo yote ya kuongeza wachezaji kipindi cha dirisha dogo yatapelekwa kwa Afisa Mtandaji Mkuu, Andre Mtine.

"Mwalimu Nasreddine Nabi amewasilisha mapendekezo yanatoka kwenye idara yake na kwenda kwa Afisa Mtendaji Mkuu, na yakitoka huko yatapelekwa kwa uongozi, na viongozi wa Yanga ni makini watayafanyia kazi na tunaamini tutapata wachezaji na kutengeneza kikosi cha kuleta heshima kwenye michuano ya ndani na ya kimataifa," alisema Kamwe.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM NA LIVERPOOL

KIUNGO wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, 19, amekuwa akilengwa kwa muda mrefu na Liverpool, lakini wanapanga kumnunua kiungo wa kati wa daraja la chini dirisha la Januari, ambaye anaweza kuwa mchezaji wa kawaida wa kikosi cha kwanza. ***(Football Insider)***

### REAL MADRID NAO WAMTAKA

BAADA ya kutazama uchezaji wake katika Kombe la Dunia, Real Madrid sasa wanahisi "itafanya juhudi" kumsajili Jude Bellingham kipindi cha majira ya joto. ***(Marca)***

### HAALAND HATAKIWI MADRID

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na Norway, Erling Haaland, 22, hayupo tena kwenye orodha ya wachezaji wanaolengwa na Real Madrid katika siku zijazo huku mshambuliaji wa Brazil, Endrick mwenye umri wa miaka 16, akikubali atajiunga nao kutoka Palmeiras mwaka 2024. ***(Sport)***

### MESSI HAJATETA NA BARCA

BARCELONA bado hawajafanya mazungumzo yoyote na Lionel Messi, 35, kuhusu fowadi huyo wa Argentina kurejea katika klabu hiyo mkataba wake na Paris St-Germain utakapokamilika msimu wa majira ya joto. ***(Cadena)***

### RONALDO, WAKALA WAVUTANA

MVUTANO unazidi kuongezeka kati ya Cristiano Ronaldo, 37 na wakala wake, Jorge Mendes, huku hali ya sintofahamu kuhusu mustakabali wa mshambuliaji huyo wa Ureno ukiendelea baada ya kuondoka kwake Manchester United. ***(AS)***

### GARCIA NA KUMTAKA RONALDO

KOCHA wa Al Nassr, Rudi Garcia, angefurahia nafasi ya kufanya kazi na Cristiano Ronaldo baada ya klabu hiyo ya Saudi Arabia kuripotiwa kutaka kumsajili, na Mhispania huyo amesema alikuwa "karibu sana" kurithi Ole Gunnar Solskjaer katika Klabu ya Manchester United mwaka jana. ***(AS)***

### RONALDO HATASTAAFU URENO

CRISTIANO Ronaldo hatastaafu soka la kimataifa baada ya Ureno kuondolewa kwenye Kombe la Dunia, hata kama kocha Fernando Santos atabakia kuwa kocha wa kikosi hicho. ***(Correio da Manha)***

### MOURINHO KUMRITHI SANTOS

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, yuko kileleni mwa orodha ya Ureno ya wanaowania kurithi mikoba ya Fernando Santos kama kocha wa timu ya taifa. ***(Gazzetta dello Sport)***

### SPURS KUMSAJILI ZAHA

KLABU ya Tottenham Hotspur ina nia ya kumsajili, Wilfried Zaha, 30, kwa uhamisho wa bila malipo wakati mkataba wa mshambuliaji huyo wa Ivory Coast utakapomalizika kule Crystal Palace msimu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### CHELSEA YATAKA STRAIKA

CHELSEA ipo tayari kumsajili mshambuliaji mpya katika dirisha la Januari na walijadili uwezekano huo hata kabla ya mshambuliaji wao wa Albania, Armando Broja, 21, kupata jeraha baya la goti. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI: KIPIGO CHA SAUDIA KIMEIAMSHA ARGENTINA

**LUSAIL,** Qatar

LIONEL Messi ameipongeza Argentina kwa kufaulu "kipimo cha tindikali", kwa kurejea kutoka kupoteza dhidi ya Saudi Arabia katika mechi yao ya ufunguzi na kutinga fainali ya Kombe la Dunia 2022.

**Mchezo wa Jumapili utashuhudia Argentina ikimenyana na Ufaransa au Morocco baada ya Messi kuwahamasisha vijana wa kocha Lionel Scaloni kushinda mabao 3-0 dhidi ya Croatia kwenye Uwanja wa Lusail, Jumanne.**

Messi mwenye umri wa miaka 35, alitangulia kufunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 34 kabla ya Julian Alvarez kufunga mabao mawili, moja kila kipindi kwa asisti za Messi.

Kuamka kwa Argentina ni tofauti sana na kuanza kwao kwenye Kundi C katika uwanja huo huo, wakipokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Saudi Arabia, iliyoko nafasi ya 51 kwa viwango vya ubora duniani.

Timu moja pekee Hispania mwaka 2010, ilipoteza mchezo wao wa ufunguzi kwenye Kombe la Dunia na kwenda kuchukua taji hilo.

Na baada ya kucheza mechi yake ya 25 ya Kombe la Dunia, akiifikia rekodi ya Mjerumani Lothar Matthaus na kufunga bao lake la 11 la Kombe la Dunia na kuipita rekodi ya Gabriel Batistuta, Messi alisema: "Naweza kusema kwamba mechi ya kwanza ilikuwa pigo kubwa kwetu sote, kwa sababu tulikuwa hatujafungwa katika michezo 36.

"Kuanza kwa namna hiyo kwenye Kombe la Dunia ilikuwa pigo, hatukufikiri kwamba tungepoteza kwa Saudi Arabia. Ilikuwa ni kipimo cha tindikali kwa kikosi hiki kizima, lakini kilithibitisha jinsi tulivyo imara.

"Tulishinda mechi zingine. Ilikuwa ngumu sana tulichofanya kwa sababu kila mechi ilikuwa fainali na tulijua tusiposhinda mambo yangekuwa magumu kwetu.

"Huu ni mzigo wa akili kwa sababu tulijua mambo yatakuwa magumu zaidi kwetu, tulifanikiwa kushinda fainali tano (mechi tano) na matumaini itakuwa hivi kwa mchezo wa fainali.

"Kwa ndani tulikuwa na imani kwamba tutafanikiwa kwa sababu tunajua tuna uwezo gani kama kikosi.

"Wacha tufurahie wakati huu. Inafurahisha kuona furaha kwa mashabiki wetu hapa na Argentina. Tutatoa kila tulichonacho kwenye fainali, lakini tunahitaji kufurahia tulichofanikiwa.

"Ninafurahia wakati huu sana. Tunajisikia nguvu kabla ya mchezo hata baada ya mchezo mrefu uliopita, uliopita haukuwa rahisi hata kidogo. Tulikuwa tumechoka, lakini kundi lilileta nguvu zake uwanjani kukabiliana na mchezo huu. "

Messi alithibitisha Jumanne kwamba atacheza mchezo wake wa mwisho wa Kombe la Dunia wakati Argentina itakapomenyana na Ufaransa au Morocco katika fainali Jumapili.

"Ninajisikia furaha sana, kuweza kufanikisha hili, kumaliza safari yangu ya Kombe la Dunia kwa kucheza mchezo wangu wa mwisho kwenye fainali. Ni miaka mingi ijayo na sidhani kama nitaweza. Na kumaliza hivi, ni bora zaidi," alisema nahodha huyo wa Argentina.

> Ninajisikia furaha sana kumaliza safari yangu ya Kombe la Dunia kwa kucheza fainali...

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,058,2

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 15 NA 16 DISEMBA 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 15/12/22 | 23:00 | GD Estoril vs Famalicao | 2.33 | 3.16 | 2.82 |
| 2. 15/12/22 | 23:00 | Viseu vs Tondela | 2.33 | 3.16 | 2.82 |
| 3. 16/12/22 | 11:45 | Newcastle Jets vs Brisbane Roar | 2.44 | 3.49 | 2.64 |
| 4. 16/12/22 | 15:30 | Abha vs AL Tai | 2.71 | 3.16 | 2.61 |
| 5. 16/12/22 | 21:30 | Santa Clara vs FC Arouca | 2.23 | 3.17 | 2.97 |
| 6. 16/12/22 | 22:00 | FCV Dender EH vs Jong KRC Genk | 2.45 | 3.56 | 2.52 |
| 7. 16/12/22 | 22:00 | Roda Kerkrade vs PEC Zwolle | 2.66 | 3.55 | 2.34 |
| 8. 16/12/22 | 22:00 | NAC Breda vs Almere City | 2.71 | 3.50 | 2.33 |
| 9. 16/12/22 | 22:00 | Helmond Sport vs Den Bosch | 2.32 | 3.60 | 2.66 |
| 10. 16/12/22 | 22:00 | De Graafschap vs Willem II Tilburg | 2.47 | 3.51 | 2.52 |
| 11. 16/12/22 | 23:00 | Saint Brieuc vs Villefranche Sur Saone | 2.92 | 3.21 | 2.32 |
| 12. 16/12/22 | 23:00 | Dunkerque vs Bourg Peronnas | 2.41 | 3.17 | 2.82 |
| 13. 16/12/22 | 23:00 | Nancy vs FC Martigues | 2.30 | 3.15 | 3.01 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG AUTAKA UBORA WA MAGUIRE MAN UNITED



**MANCHESTER,** England

KOCHA Mkuu wa Manchester United, Erik ten Hag, amemtaka Harry Maguire kuiga kiwango chake alipokuwa anaichezea England kwenye Kombe la Dunia ili kupambana kurejea kwenye kikosi cha kwanza kwa 'Mashetani Wekundu' hao.

Maguire alianza mechi tatu pekee za Ligi ya England kwa United msimu huu kabla ya kwenda Kombe la Dunia akiwa na England na kuonekana katika michezo yote mitano katika kufuzu kwa robo fainali.

Kocha Gareth Southgate amerudia kumuunga mkono beki huyo wa kati kwenye hatua ya kimataifa, ingawa Raphael Varane na Lisandro Martinez wamekuwa washirika wa Ten Hag wanaopendelewa na United msimu huu.

Baada ya England kuondolewa na Ufaransa Jumamosi iliyopita, Ten Hag anatumaini Maguire anaweza kurejea Old Trafford kwa kujiamini kutokana na uchezaji wake wa kuvutia akiwa Qatar.

Ten Haga amesema; "Ninaweza tu kumuunga mkono. Nimeulizwa mara nyingi kama anatosha kunichezea na ni wazi anatosha kucheza katika kiwango cha juu, na kisha ni juu yake kuonyesha ujasiri huo uwanjani na hakuonyesha hivyo katika mechi zote za United."

Kocha huyo aliendelea kusema beki huyo anapocheza kwa kujiamini kama sasa, yeye ni mchezaji muhimu sana kwao na ndivyo kila mtu anavyotarajia.

Na hicho ndicho ambacho Maguire anatarajia kutoka kwake kutokana na kuwa na kiwango cha juu zaidi.



# Ibrahimovic amuonya Leao

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic amemtaka mchezaji mwenzake wa AC Milan, Rafael Leao, raia wa Ureno kukataa nia ya klabu nyingine na kubakia hapo katika dimba la San Siro ili kutambua uwezo wake "wa kutisha".

Leao alikuwa na jukumu kubwa wakati Milan ilipomaliza kusubiri kwa miaka 11 kushinda Kombe la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Scudetto, msimu uliopita, wakati hakuna mchezaji mwingine wa 'Rossoneri' hao aliyeweza kufikia idadi yake ya mabao sita na pasi nne.

Winga huyo, ambaye alifunga katika ushindi wa Kombe la Dunia wa Ureno dhidi ya Ghana na Uswisi, amekuwa akihusishwa na Klabu za Real Madrid, Paris Saint-Germain na Liverpool katika miezi ya hivi karibuni.

Hata hivyo, Ibrahimovic amesisitiza kuwa Milan ndio
mahali pazuri zaidi kw
Leao kujiendeleza, akianga
lia hatua alizopiga tangu aj
unge na timu hiyo ya koch
Stefano Pioli.

"Bila shaka, Milan ni ma
ingira sahihi kwake," alis
ma Ibrahimovic akiliamb
La Gazzetta dello Sport.

"Angalia tu ukuaji wak
alipofika, alikuwa mbali n
mchezaji anayeamua le
Hapa yeye ni muhimu sa
kwetu, mahali pengine, a
gekuwa muhimu? Angepa
wa kuanza kutoka mwanz

HABARI MICHEZO


211,696/-


# MKAZI WA DODOMA ASHINDA MILIONI 123.6/- ZA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Ihumwa mkoani Dodoma, Peter Alfred Mbawala, ameshinda kitita cha Sh. milioni 123.6 kupitia Bet Spinner Bonus ya SportPesa kama nyongeza ya ziada katika ushindi wa mkeka wake wa multibet alioucheza wiki kadhaa zilizopita.

**Akizungumza katika Ofisi za SportPesa zilizopo Oysterbay, Dar es Salaam jana, Mbawala alisema alianza kucheza na SportPesa miaka mitano iliyopita, akivutiwa zaidi na 'odds' pamoja na bonus za SportPesa ambazo tangu wakati huo zilikuwa kubwa kuliko za washindani wao.**

Akizungumzia namna alivyoshinda kiasi hicho cha Sh. milioni 123.6, Peter alisema siku moja kabla ya kushinda hela hiyo, alishinda mkeka ambao aliweka mechi nne, ukampatia laki tatu.

"Siku iliyofuata niliweka mkeka wa pili wa mechi 15 za multibet na kuweka laki moja iliyobaki kwenye akaunti yangu ya SportPesa. Baada ya kuuweka sikufutilia sana matokeo ya mechi nilizocheza. Sikujisumbua kuangalia mkeka mpaka ilipofika usiku majira ya saa nne na nusu ambapo baada ya kufungua simu nilikutana na 'sms' iliyonishangaza sana.

"Unajua katika mkeka wangu nilitakiwa kushinda Sh. 1,400,000, sasa baada ya kupata sms ya "hongera umeshinda" ilinionyesha hela nyingi sana. Niliangalia zile tarakimu mara mbilimbili na kuhisi imekosea njia kwa bahati mbaya.

Baada ya muda si mrefu nilipigiwa simu kutoka SportPesa na mtu aliyejitambulisha ni kutoka kitengo cha huduma kwa wateja akaniambia nimeshinda Sh. 123,641,830 kama bonus ama nyongeza kupitia Bet Spinner ambayo kwa wakati ule nilikuwa bado siielewi vizuri na kunitaka nifike ofisini kwao Dar es Salaam.

"Mimi kama kijana ambaye ninajihusisha na kazi ya usambazaji ama uuzaji wa bidhaa mbalimbali, pesa hii nitaitumia kufanya biashara ambazo tayari nazijua kwa kufanya kazi ambayo nimeajiriwa," alisema Mbawala

Naye Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Sportpesa Sabrina Msuya, alisema Bet Spiner ni fursa inayopatikana kwa wacheaji wa multibet ama single bet pale wanapokuwa wanaweka mkeka kuna vigurudumu ambavyo vinazunguka na kuongezea nafasi ya kuongeza ama kupata mara mbili ushindi wako.

"Kwa mfano Mbawala alipata fursa ya ushindi wake kuzidishwa mara 100, hivyo ukichukua kiwango alichotakiwa kushinda cha Sh. 1,472,687 na ukazidisha mara 100 utapata hesabu kamili ambayo ni Sh. 147,268,700 na baada ya kodi amebakiwa na Sh. 123,641,830."




Mshindi wa Bet Spinner Bonus ya SportPesa, Peter Alfred Mbawala, kutoka Dodoma akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 123.6 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 15 za Multibet ya SportPesa.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mgunda ataka 4 wapya

INATOKA UKURASA 32

wachezaji wenye uwezo mkubwa ikiwamo safu ya ushambuliaji kuhakikisha tunaongeza nguvu," alisema kocha huyo.

Mgunda alisema katika michuano hiyo ya kimataifa wamepangwa na timu ngumu, hivyo kupitia kuboresha kikosi chao na kucheza mechi za ugenini kwa tahadhari kubwa ikiwa ni pamoja na kuwaheshimu wapinzani wao, ndiyo njia nzuri ya kuweza kusonga mbele.

"Wote ni washindani wetu hatuwezi kusema mmoja ni mgumu na mwingine rahisi, kwa kuwa wameingia katika hatua hii, lazima tuwaheshimu kwa kucheza kwa nidhamu kubwa tunapokuwa ugenini," alisema Mgunda ambaye ni mara yake ya kwanza kufanikisha timu kuingia katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba imepangwa Kundi C pamoja na Raja Casablanca ya Morocco, Horoya AC ya Guinea na Vipers ya Uganda, ambapo itaanzia ugenini dhidi ya miamba hiyo Guinea kati ya Februari 10 hadi 13, mwakani.

## *Yanga yaanza na Diarra, Aucho, Job*

INATOKA UKURASA 32

Hata hivyo, Kaze alithibitisha kwamba wanahitaji kupata mshambuliaji mmoja mwenye uwezo mkubwa hata anapokosekana Mayele.

Alisema wanaelekea katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika na wameona timu watakazokutana nazo, hivyo wanalazimika kuboresha kikosi chao kwa kuongeza nguvu katika safu ya ushambuliaji.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/12/22 | 19:30 | Aquila Montevarchi vs Rimini FC 1912 | 2.70 | 3.05 | 2.70 |
| 02. 17/12/22 | 19:30 | Olbia Calcio vs Lucchese Libertas 1905 | 3.00 | 3.10 | 2.42 |
| 03. 17/12/22 | 20:00 | SC Pisa vs Brescia Calcio | 2.34 | 3.15 | 3.10 |
| 04. 17/12/22 | 20:00 | Akritas Chlorakas vs Nea Salamina Famagusta | 2.95 | 3.25 | 2.36 |
| 05. 17/12/22 | 21:30 | Beitar Jerusalem FC vs Maccabi Netanya FC | 2.90 | 3.25 | 2.42 |
| 06. 17/12/22 | 22:00 | Estrela Amadora vs FC Penafiel | 2.48 | 3.20 | 2.80 |
| 07. 17/12/22 | 22:30 | Reggina 1914 vs SSC Bari | 2.36 | 3.05 | 3.15 |
| 08. 17/12/22 | 23:00 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.50 | 2.80 | 3.15 |
| 09. 18/12/22 | 07:00 | Western United FC vs Western Sydney Wanderers | 2.70 | 3.40 | 2.46 |
| 10. 18/12/22 | 13:30 | Bandirmaspor vs Pendikspor | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 11. 18/12/22 | 14:00 | CD Atletico Baleares vs Real Murcia CF | 2.32 | 3.10 | 3.15 |
| 12. 18/12/22 | 14:30 | Turris Calcio vs Calcio Foggia | 2.75 | 3.05 | 2.65 |
| 13. 18/12/22 | 15:45 | AO Egaleo 1931 PAE vs Chania Kissamikos | 2.33 | 2.95 | 3.30 |
| 14. 18/12/22 | 16:00 | Cosenza Calcio vs Ascoli Calcio 1898 | 2.90 | 3.00 | 2.55 |
| 15. 18/12/22 | 16:00 | Modena FC vs Benevento Calcio | 2.41 | 3.10 | 3.00 |
| 16. 18/12/22 | 20:45 | Palermo FC vs Cagliari Calcio | 2.70 | 3.15 | 2.65 |
| 17. 18/12/22 | 21:00 | Burgos CF vs SD Huesca | 2.36 | 2.90 | 3.30 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMSI - 15/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3772 | Turan Tovuz vs Neftchi Baku | 7.59 | 4.28 | 1.36 |
| 14:00 | 2191 | Gokulam Kerala FC vs Neroca FC | 1.73 | 3.40 | 4.38 |
| 14:00 | 3998 | Shijiazhuang vs Henan Jianye | 2.92 | 3.35 | 2.18 |
| 14:00 | 5894 | Miedz Legnica vs Baumit Jablonec | 2.27 | 3.75 | 2.75 |
| 14:15 | 5497 | PSM Makassar vs Persepam MU | 2.41 | 2.87 | 2.97 |
| 14:30 | 1412 | Guangzhou Evergrande vs Shandong Luneng | 8.94 | 5.63 | 1.23 |
| 14:30 | 1722 | Hangzhou NG vs Chengdu Qianbao | 2.10 | 3.25 | 3.15 |
| 14:30 | 3254 | Meizhou Kejia vs Shanghai SIPG | 4.07 | 3.59 | 1.74 |
| 15:00 | 5278 | Hebei Zhongji vs Shenzhen | 12.65 | 7.01 | 1.14 |
| 15:30 | 1058 | Al Khaleej Club vs AL Faiha | 2.64 | 3.19 | 2.64 |
| 15:30 | 5060 | Dhamk vs Al-Ettifaq | 2.10 | 3.40 | 3.35 |
| 15:40 | 1290 | AL Ain vs Al Ahli Jeddah | 9.14 | 4.37 | 1.31 |
| 15:40 | 1363 | Bahla vs Al Nasr Salalah | 2.79 | 2.70 | 2.70 |
| 15:45 | 5408 | Al Nasr Dubai vs Al Dhafra | 1.95 | 3.74 | 3.11 |
| 16:00 | 2177 | Ethiopian Medhin vs Fasil Kenema | 2.51 | 3.14 | 2.61 |
| 16:00 | 4234 | KMC vs Coastal Union | 1.94 | 2.96 | 4.07 |
| 17:00 | 5814 | Delhi Dynamos FC vs ATK Mohun Bagan | 3.02 | 3.46 | 2.08 |
| 17:30 | 3969 | Al Ahli Manama vs Al Shabbab | 2.02 | 3.26 | 3.36 |
| 17:30 | 4731 | AL Badii vs Manama Club | 5.45 | 3.75 | 1.54 |
| 18:00 | 1203 | Al Taawon vs AL Adalh | 1.61 | 3.80 | 5.40 |
| 18:00 | 1298 | El Ittihad Alexandria vs Farco FC | 2.36 | 2.69 | 3.58 |
| 18:00 | 2533 | El Daklyeh vs Smouha Club | 4.08 | 2.84 | 2.09 |
| 18:00 | 5635 | Al Wehda vs Al Fateh (KSA) | 3.00 | 3.45 | 2.24 |
| 18:10 | 5293 | AL Etihad vs Dhofar Salalah | 7.60 | 3.90 | 1.46 |
| 18:30 | 1772 | Panathinaikos vs Volos | 1.33 | 4.49 | 8.01 |
| 18:30 | 2331 | Jazira Abu Dhabi vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 2.67 | 3.40 | 2.32 |
| 18:30 | 3971 | Bouake FC vs Racing Club Dabidjan | 3.11 | 2.82 | 2.36 |
| 19:00 | 3179 | Legetafo Legedadi vs Arba Minch Kenema | 4.68 | 3.12 | 1.77 |
| 20:00 | 2161 | EN Paralimni vs AEL Limassol | 3.30 | 3.20 | 2.20 |
| 20:00 | 4463 | Apollon Limassol vs Doxa Katokopia | 1.38 | 4.60 | 7.80 |
| 20:00 | 4882 | Arab Contractors vs Enppi Club | 2.25 | 2.79 | 3.68 |
| 20:30 | 1259 | Al Shabab Riyadh vs Al Ittihad Jeddah | 2.06 | 3.45 | 3.40 |
| 20:30 | 1769 | Al Hidd Club vs Al Hala Muharraq | 2.02 | 3.07 | 3.60 |
| 20:30 | 3618 | St Lucia vs Gzira United | 6.00 | 4.50 | 1.47 |
| 20:30 | 4792 | Olympiakos vs Atromitos | 1.26 | 5.06 | 8.95 |
| 20:30 | 5104 | Bahrain Club vs AL Khalidiyah | 6.24 | 3.66 | 1.50 |
| 21:00 | 2916 | Steaua Bucuresti vs CFR Cluj | 2.40 | 3.12 | 2.92 |
| 21:00 | 4111 | Asi D Abengourou vs ASEC Mimosas | 7.57 | 3.74 | 1.43 |
| 21:00 | 5369 | Zejtun Corinthians F.c. vs Tarxien Rainbows | 1.64 | 3.98 | 4.18 |
| 21:30 | 3350 | FC Versailles 78 vs Paris 13 Atletico | 1.90 | 3.36 | 3.85 |
| 21:30 | 5090 | Bastia Borgo vs Avranches | 2.18 | 3.21 | 3.16 |
| 22:00 | 4057 | Jong PSV vs Jong Ajax | 2.25 | 3.60 | 2.76 |
| 22:15 | 2380 | Club Deportivo Huarte vs Pamplona | 1.67 | 3.69 | 4.36 |
| 22:30 | 3830 | Kifisias vs AEK Athens | 9.34 | 5.26 | 1.25 |
| 22:30 | 4077 | Ammanford vs Cambrian & Clydach Vale | 3.25 | 4.18 | 1.81 |
| 23:00 | 1895 | Viseu vs Tondela | 2.10 | 3.21 | 3.21 |
| 23:00 | 3429 | GD Estoril vs Famalicao | 2.42 | 3.12 | 2.73 |
| 23:00 | 4279 | Marsa FC vs Mtarfa FC | 1.56 | 3.74 | 5.25 |
| 23:00 | 5080 | Rangers vs Hibernian | 1.29 | 5.37 | 8.74 |
| 23:15 | 4185 | Qrendi FC vs Marsaskala FC | 2.58 | 3.36 | 2.41 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Desemba 15, 2022
Nipashe



Messi: Kipigo cha Saudia kimetuamsha UKURASA 29

FAINALI HIYOOO...



Julian Alvarez (kulia), akishangilia sambamba na Lionel Messi (kulia) pamoja na Nahuel Molina, baada ya kuifungia Argentina bao la tatu wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Croatia kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la Dunia Qatar juzi usiku. Alvarez aliyefunga bao hilo akipokea pasi ya mwisho kutoka kwa Messi, alicheka na nyavu mara mbili katika ushindi huo huku lingine likifungwa kwa penalti na mtoa pasi huyo. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yaanza na Diarra, Aucho, Job

**Na Saada Akida**

Nabi aanika ripoti yake ya dirisha dogo lililofunguliwa leo, autaka uongozi kuhakikisha kwanza...

WAKATI dirisha dogo la usajili wa timu za Ligi Kuu Bara, Championship na Ligi Daraja la Pili, likifunguliwa leo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameanika ripoti yake katika kukiboresha kikosi chake tayari kwa kutetea ubingwa wa ligi hiyo pamoja na Kombe la Shirikisho Afrika.

**Nabi akiwa na msaidizi wake, Cedric Kaze wamekutana na Mtendaji Mkuu wa Yanga, Andre Mtine, kujadili mambo mbalimbali ya usajili na ripoti nzima ya timu kwenye raundi ya kwanza Ligi Kuu Tanzania Bara na mwenendo mzima wa timu kwa ujumla.**

Katika ripoti yake, Nabi ametaka kuongezwa mshambuliaji mwingine mwenye uwezo mkubwa hata akikosekana Fiston Mayele wasiumize kichwa kusaka mbadala.

Kwa mujibu wa kiongozi mmoja ndani ya klabu hiyo, Nabi amewaomba mabosi wake kumalizana kwanza na wachezaji wao ambao wanamaliza mikataba yao hivi karibuni baada ya msimu huu kuisha.

"Baadhi ya wachezaji ambao Nabi anataka kuona wanapatiwa mikataba mipya ili kuondoa presha, kabla ya kuendelea kusajili ni pamoja na kipa Djigui Diarra, Dickson Job, Khalid Aucho na Jesus Moloko," alisema.

Alisema kwa Diara mazungumzo yanaendelea vizuri na muda si mrefu yatakamilika, lakini kwa Job ambaye anatarajiwa kupewa mkataba wa miaka miwili, watamalizana naye mapema.

Aidha, alisema kwa Aucho, kiungo mkabaji huyo amewatoa hofu na kwamba ameonyesha nia ya kuendelea kuitumikia klabu hiyo.

"Katika mkataba wa Aucho na Yanga wa sasa kuna kipengele cha nyongeza ya mwaka mmoja mbele cha kuendelea kusalia Jangwani," alisema.

Kuhusu Moloko, alisema bado mazungumzo hayajaanza rasmi ila kutoka kwa wakala wake, Nestory, amemthibitishia kupokea ofa kutoka kwa Yanga kuhitaji kuendelea kupata huduma ya winga huyo.

"Kuna wachezaji ambao wanaondoka ndani ya Yanga au kupelekwa kwa mkopo akiwamo Yusuph Athuman na David Bryson," alisema mtoa habari huyo.

INAENDELEA UK. 31

# Mgunda ataka 4 wapya Simba

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema katika ripoti yake aliyoikabidhi kwa uongozi wa Simba ili kufanyiwa kazi katika usajili wa dirisha dogo lililofunguliwa leo, ameelekeza kupatiwa nyota wapya wanne wa kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya michuano ya Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika nafasi ambazo Mgunda anataka kikosi chake kiboreshwe kwa kuongezwa wachezaji wenye uwezo mkubwa ni kiungo mshambuliaji, mkabaji na mshambuliaji.



Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema wanaelekea katika mashindano magumu na wanalazimika kufanya maboresho ya kikosi chao kulingana na nafasi alizopendekeza katika ripoti yake.

Alisema kuna nafasi lazima wapatikane watu wenye uwezo mkubwa kwa ajili ya mashindano yaliyopo mbele yao husan Ligi ya Mabingwa ambayo tayari makundi yametoka.

"Tumeona makundi na tunaanzia ugenini, ukiangalia wapinzani wetu, kuna haja ya kufanya maboresho makubwa katika nafasi nilizozipendekeza, kupata

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >